# Nipashe

Alhamisi Oktoba 24, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580057

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US




## JKT yafanya mageuzi makubwa, yafuta mpango wa ajira za vijana

UKURASA 3




UKURASA 13

# Sheria ya Ndoa kubadilishwa



• **Ni** uamuzi wa mahakama mtoto kuolewa chini ya miaka 18, yasema inaleta ubaguzi, wanaharakati, wadau wapongeza...*Uk. 2*

## YALIYOMO


UKURASA WA 2

**JAMES MAPALALA AFARIKI DUNIA DAR**

MWANASIASA na mwanaharakati mkongwe wa haki za binadamu...

UKURASA WA 7

**JELA MAISHA KUMKATA MKONO MWENYE UALBINO**

WATU wanne wamehukumiwa kifungo cha maisha jela baada ya kupatikana...


## Mdhamini wa Lissu awekwa njiapanda

UKURASA 3



Rais John Magufuli akiagana na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria wa China, Wang Liyu, Ikulu jijini Dar es Salaam jana, baada ya mazungumzo na viongozi wa Taasisi ya Mashauriano ya Kisheria kwa nchi za Asia na Afrika (AALCO). Wa pili kulia ni Makamu wa Rais wa AALCO, Prof. Mohamad Shalaldeh. **Habari Uk. 7** **PICHA: IKULU**




Scan Hapa

Fungua App ya QR code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## Wanafunzi wanane wafukuzwa shule uchomaji moto mabweni

• **Mmoja** abambwa na simu, kondomu, atimua mbio kusikojulikana...*Uk.2*


**MICHEZO** **MBAO FC YAIPA KIBURI YANGA SC** UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# James Mapalala afariki dunia

**Na Romana Mallya**

MWANASIASA na mwanaharakati mkongwe wa haki za binadamu, James Mapalala, amefariki dunia katika hospitali ya Kairuki jijini Dar es Salaam alikokuwa amelazwa.

Mapalala ni miongoni mwa wanasiasa wakongwe Tanzania ambao walikuwa mstari wa mbele kudai mfumo wa vyama vingi pamoja na kudai haki za ninadamu. Mtoto wa marehemu, Bernard James, aliliambia Nipashe jana kuwa baba yake alifariki dunia jana asubuhi.

"Baba alilazwa hospitali ya Kairuki kwa wiki mbili, alikuwa akisumbuliwa na maradhi ambayo yalimuanza muda mrefu, lakini miezi ya hivi karibuni hali ilibadilika," alisema.

Alisema msiba upo Morocco jirani ya maghorofa ya Polisi Oysterbay kwa ajili ya kupanga shughuli nzima ya mazishi.

Mapalala aliyezaliwa Februari Mosi, mwaka 1936, alikuwa miongoni mwa wananasiasa na wanaharakati waliopigania kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa, baada ya kufutwa na Rais wa kwanza, Mwalimu Julius Nyerere. Mapalala alianzisha harakati hizo mwaka 1968, wakati huo alikuwa mwalimu, na kujikuta matatizoni ikiwamo kufungwa jela katika Gereza la Uyui mkoani Tabora.

Baada ya misukosuko ndipo mwaka 1991 walianzisha Chama cha Wananchi (CCW) na baadaye kiliungana na chama cha Kamahuru cha Zanzibar na miaka miwili baadaye kuzaliwa Chama cha Wananchi (CUF).

Hata hivyo, baadaye Mapalala aliondolewa CUF katika nafasi ya uenyekiti kisha kuanzisha chama chake cha Chausta.

# Sheria ya Ndoa kubadilishwa

**Mary Geofrey na Hellen Mwango**

BAADA ya Mahakama ya Rufani kukubaliana na Mahakama Kuu ya Tanzania na kutamka kuwa vipengele 13 na 17 vya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 vinavyoruhusu watoto wa kike kuanzia miaka 14 kuolewa kwa ridhaa ya wazazi wake, wanaharakati na watetezi wa watoto wa kike, wapongeza uamuzi huo.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wameishauri serikali kuanza mchakato wa kubadili sheria hiyo mara moja.

Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa), Rose Reuben, alipongeza mahakama kwa uamuzi huo na kusema mchakato wa kubadili sheria hiyo unatakiwa kufanyika mapema.

Alisema sheria hiyo ilikuwa ikiruhusu kumuoza mtoto wa kike akiwa na miaka 14, hivyo kaunzia sasa haitaruhusiwa kwa mujibu wa sheria.

"Tuna furaha sana kama watetezi wa haki za watoto wa kike tumepata pa kusimamia. Ulikuwa ni mchakato mrefu wa kutaka kubatilishwa kwa sheria hii na 'Msichana Initiative' ilishinda, lakini serikali ilikata rufani, leo tumeshuhudia mahakama imebadilisha vifungu hivyo vya sheria," alisema.

Naye Mwanaharakati aliyewahi kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Tamwa, Ananilea Nkya, aliupongeza uamuzi huo wa Mahakama na kuitaka serikali, watetezi wa haki za binadamu na asasi za dini, kutoa elimu kwa jamii.

"Niipongeze mahakama kwa uamuzi huu ingawa naamini kwa nchi yetu tulikuwa tumechelewa kuifuta sheria kama hii kwa sababu ilikuwa ikimkosesha mtoto wa kike haki ya afya na kupata elimu," alisema Nkya.

Alisema baada ya uamuzi huo ni muhimu wadau wakaanza kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa mtoto wa kike kutoolewa akiwa na umri mdogo kwa sababu binti mwenye miaka 14 anakuwa amemaliza darasa la saba.

"Jamii inatakiwa kupewa elimu kuhusu pia fursa zilizopo hasa za shule za kata na serikali kuandaa mazingira ya kumwezesha mtoto wa kike kupata elimu katika umri huo ili kumwepusha na ndoa za utotoni," alisema Nkya.

Nacho Chama cha ACT-Wazalendo, kupitia ujumbe wa Tweeter, kilimpongeza mwanaharakati huyo, Rebeca Gyumi kwa kushinda rufani iliyokatwa na serikali katika Mahakama ya Rufani dhidi ya hukumu ya Mahakama Kuu kupinga ndoa za utotoni.

Katibu Mwenezi wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, katika ukurasa wao wa Twitter aliandika: "Huu ni ushindi kwa wasichana nchini."

Kwa upande wake, Shirika la Kutetea Haki za Wasichana la Mwanamke na Uongozi, lilipongeza uamuzi wa Mahakama ya Rufani kukubaliana na Mahakama Kuu kuwa vipengele vinavyoruhusu mtoto wa kike kuolewa akiwa na miaka 14 ni batili.

"Leo ni siku njema sana kwa mtoto wa kike Tanzania. Kama shirika la kutetea haki za wasichana tuna furaha sana kuona maamuzi haya ya Mahakama ya Rufani," ilieleza taarifa hiyo

INAENDELEA UK.8



Mkurugenzi wa Taasisi ya Dk. Ntuyabaliwe, Jacquline Mengi (katikati), akimsikiliza mmoja wa wanafunzi wa Shule ya Msingi Kinondoni, ambao waliohitimu mafunzo ya ujasiriamali ya wiki sita yaliyoendeshwa na taasisi hiyo, wakati wa hafla ya kufunga mafunzo hayo, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mwenyekiti wa shule hiyo, Swedi Twaibu (kushoto), Ofisa Elimu Kata ya Mwananyamala, Joshua Biswalo na Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Adelina Kessi. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Wanafunzi wanane wafukuzwa tuhuma kuchoma moto mabweni

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WANAFUNZI wanane wa Shule ya Sekondari Kiwanja wilayani Chunya, wamefukuzwa shule kwa tuhuma za kuchoma mabweni ya shule na kukutwa na simu na vitu vingine ambavyo haviruhusiwi shuleni.

Uamuzi wa kuwafukuza wanafunzi hao ulitangazwa jana shuleni hapo na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alipotembelea kuangalia maendeleo ya ukarabati wa mabweni hayo.

Chalamila alisema uamuzi wa kuwafukuza wanafunzi hao ulifanywa na Bodi ya Shule kabla haijavunjwa.

Mkuu huyo wa mkoa alisema wanafunzi saba kati ya waliofukuzwa, wanakabiliwa na kesi ya kuchoma mabweni ya shule hiyo mwanzoni mwa Oktoba, mwaka huu, na kuisababishia hasara kubwa serikali.

Alisema mwanafunzi mwingine amefukuzwa kutokana na kukutwa na simu na mpira wa kiume (kondomu) kwenye begi lake wakati akirejea shuleni baada ya muda waliopewa wanafunzi wa kidato cha tano na sita kutakiwa kurejea.

"Hao wote wanaokabiliwa na kesi wamefukuzwa lakini wanaunganishwa na huyo ambaye alirejea tena shuleni akiwa na simu kwenye begi lake pamoja na kondomu. Inaonyesha hii shule mnabakana sana, sasa ole wenu tuje tuwakamate," alisema Chalamila. Hata hivyo, alisema kijana huyo ambaye alikutwa na simu kwa mara ya pili, alitimua mbio na kutokomea kusikojulikana baada ya kupekuliwa kwenye begi lake na kukutwa na vitu hivyo ambavyo havitakiwi.

Chalamila pia aliwapa wiki moja wanafunzi ambao bado hawajakamilisha malipo ya fedha za kukarabati mabweni yaliyoteketea kwa moto, kuhakikisha wanafanya hivyo ili waendelee na masomo.

Alisema wanafunzi hao ambao bado hawajakamilisha malipo hayo, hawataruhusiwa kuingia darasani mpaka Novemba Mosi, mwaka huu na watatakiwa kupeleka risiti za malipo na barua ya kukiri kosa na kujieleza kwa nini wamechelewa kurejea shuleni.

Kwa mujibu wa Chalamila, endapo hawatatekeleza agizo hilo, bodi ya shule itatakiwa kukaa na kufanya uamuzi dhidi yao ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule.

Mkuu wa Shule hiyo, Elly Mnyarape, aliwataja wanafunzi waliofukuzwa shule kuwa ni Loren Msechu, Barnaba Minga, Samuel Ibrahim na Oswald Msomba wa kidato cha sita, James Kunambi na Baraka Kasisike wote wa kidato cha nne.

Alimtaja kijana aliyekutwa na simu pamoja na kondomu kwenye begi lake baada ya kurejea kuwa ni Peter Kabimilo wa kidato cha sita ambaye alidai alikimbia na hajulikani aliko. "Tunashukuru kwa hatua ambazo zimechukuliwa dhidi ya vijana hawa maana waliisababishia hasara kubwa sana serikali lakini kwa sasa ukarabati unaendelea na wamebaki wachache ambao bado hawajalipa," alisema Mnyarape.

Aliwataka wanafunzi hao kubadilika na kutorudia makosa ya aina yoyote shuleni hapo kwa kuwa yanaweza kuwasababishia na wao kufukuzwa kabisa shule.

## HABARI KITAIFA

# Mdhamini wa Lissu awekwa njiapanda

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam imemtaka Robert Katunda, mdhamini wa Mwanasheria Mkuu wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tundu Lissu, anayekabiliwa na kesi ya uchochezi, Novemba 21, mwaka huu kuwasilisha vielelezo vinavyoeleza bado yuko kwenye matibabu.

Amri hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba, baada ya upande wa Jamhuri kudai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kusikilizwa lakini mshtakiwa hajafika mahakamani.

Awali, Wakili wa Serikali Esteria Wilson, alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa jana kwa ajili ya kusikilizwa na upande wa Jamhuri ulikuwa tayari kuendelea na ushahidi.

Hakimu alimtaka mdhamini kueleza sababu za mshtakiwa kutokufika mahakamani ndipo alipodai kuwa bado anaumwa anaendelea na matibabu.

"Tarehe ijayo inapopangwa kesi ulete vielelezo kuthibitisha kama kweli mshtakiwa bado anaumwa na anaendelea na matibabu au la," alisema Hakimu Simba.

Mbali na Lissu, washtakiwa wengine ni wahariri Simon Mkina, Jabir Idrisa na mmiliki wa kampuni ya uchapishaji ya Jamana, Ismail Mehbooh.

Kwa pamoja, washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka matano ikiwamo kuandika habari za uchochezi kinyume na Sheria ya Magazeti ya Mwaka 2002.

Ilidaiwa kuwa kati ya Januari 12 hadi 14, 2016 jijini Dar es Salaam, washtakiwa Jabir, Mkina na Lissu, waliandika na kuchapisha taarifa za uchochezi zenye kichwa cha habari kisemacho, 'Machafuko yaja Zanzibar'.

Katika shtaka la pili, wanadaiwa kuwa Januari 14, 2016 walichapisha habari hizo ili kuleta chuki kwa wananchi wa Zanzibar.

Mshtakiwa Mehboob anadaiwa kuwa Januari 13, 2016 katika jengo la Jamana lililoko Manispaa ya Ilala, alichapisha gazeti la Mawio lililokuwa na taarifa za uchochezi.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa huyo pia alichapisha gazeti hilo bila kuwasilisha hati ya sheria ya kiapo kwa Msajili wa Magazeti.

# JKT yafanya mageuzi makubwa

**Na Moshi Lusonzo**

MKUU wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Brigedia Jenerali Charles Mbuge, ametangaza mageuzi ndani ya jeshi hilo, na kuwaagiza makamanda wa vikosi kuwafafanulia vijana wanaojiunga kuwa hakuna ajira badala yake ni sehemu ya kupewa mafunzo ya uzalendo, ukakamavu na uzalishaji mali.

Akizungumza na makamanda wa vikosi, wakuu wa vitengo na shule zinazomilikiwa na jeshi hilo, Brigedia Jenerali Mbuge, amesema katika uongozi wake ambao una kauli mbiu "Maneno si kazi, kazi vitendo", hautamwacha salama kiongozi atakayekwenda kinyume cha mkakati wa chombo hicho ambao ni kutoa malezi, mafunzo na uzalishaji mali kwa vijana.

Alisema katika mageuzi hayo, JKT itatekeleza kazi zake katika weledi unaokubalika, kujenga maadili kwa vijana na askari wake na uzalishaji wa chakula kwa ajili ya kuipunguzia gharama serikali.

**HAKUNA AJIRA**

Brigedia Jereali Mbuge alisema kuanzia mwaka huu wanafikiria kuongeza idadi ya vijana wanaojiunga na jeshi hilo, hata hivyo, watakaoingia katika kambi zilizochaguliwa wasiwe na fikra kwamba watapata ajira kwani hilo si jukumu lao.

"Naomba hili lieleweke na makamanda wanisaidie kutoa ufafanuzi katika jambo hili, jukumu la JKT ni sehemu ya kutoa mafunzo kwa ajili ya kuwandaa vijana kuwa wazalendo, wakakamavu, majasiri pamoja na uzalishaji mali, na si vinginevyo, sisi hatutoi ajira kama vijana wengi wanavyofikiria," alisisitiza Brigedia Jenerali Mbuge.

Alisema katika suala hilo kuna baadhi ya vijana walioopitia jeshi hilo wamechukuliwa hatua baada ya kutumia mitandao vibaya kwa kukiuka nidhamu.

"Kuna vijana hawana nidhamu walitumia mitandao ya kijamii kwa kutoa ujumbe kwa viongozi, tumewachukulia hatua stahiki. Pia kuna baadhi ya askari wanashindwa kutoa elimu na kuwafanbya viajana kuamini JKT ni sehemu ya ajira," aliongeza.

Alifafanua kwamba vijana hao watapata ajira endapo vyombo vingine vya ulinzi na usalama vitahitaji askari kutokana na vijana hao kuwa kamili katika suala la ulinzi wa nchi.

**MAGEUZI UTENDAJI WA KAZI**

Mkuu huyo wa JKT, alisema kuanzia mwaka huu watajikita katika kuboresha utendaji wa kazi kwa kila askari, kupanua wigo wa utoaji mafunzo kwa vijana pamoja na kuongeza uzalishaji wa chakula.

"Tunataka tufikishe malengo yetu ya kuzalisha chakula cha kutosha kwa ajili ya vijana wetu kwa nia ya kupunguza mzigo wa gharama kwa serikali, kuongeza idadi ya vijana kujifunza uzalendo na kupanua sekta ya michezo," alisema.

Aidha, katika kutimiza malengo ya mikakati hiyo, Brigedia Jenerali Mbuge aliwataka makamanda wa vikosi wanaoongoza idara mbalimbali kujitathmini wao wenyewe kama wanaweza kukamiliana na kasi hiyo ikiwamo kujipima kwa kazi walizofanya huko nyuma kama zimeleta tija kwa jeshi hilo.




In Loving Memory of
**JOSEPH ANICETIUS MUTABOYERWA**
**1st Anniversary**

27th October 2019 marks the first year of the passing away of our beloved Joseph. Memories continue to linger around us because there are unforgettable memories for keeps.

Joseph, it was hard to believe your passing that Saturday morning on the 27th October 2018, but we thank God for the courage he provided to us especially for our girls who have continued to be strong. Our God is such a gracious God and he gave us so much. He let us keep your memory with us.

Joseph, your life was not in vain. You have touched so many lives on earth with your love, wisdom, kindness, sound advice, laughter and generosity. All these shall continue to inspire many of us. You are no longer in our life to share, but in our hearts you are always there.

You are profoundly missed by your loving wife **Emmy,** children **Daniella** and **Damita**. Your Brothers and Sisters, relatives and friends.

Memorial and thanks giving mass shall be held on Saturday, 26th October 2019 at St Joseph Cathedral, Dar es Salaam from 10.30 am.

**Psalm 23:6**
*"Surely your goodness and love will follow me all the days of my life, and I will dwell in the house of the Lord"*

115474902



**OFISI YA RAIS,**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**MKOA WA MTWARA**

**KONGAMANO LA UWEKEZAJI NA MAONESHO YA BIASHARA MTWARA 2019**



**MGENI RASMI: WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TAREHE: 31 OKTOBA – 3 NOVEMBA 2019 | MAHALI: UWANJA WA CHUO CHA UALIMU MTWARA**

Kongamano la Uwekezaji na Maonesho ya Biashara Mtwara 2019 litahusisha uzinduzi wa Mwongozo wa Uwekezaji Mtwara na kuwa jukwaa la kuonesha fursa za uwekezaji; ambazo bado hazijatumika kwenye Mkoa kwa watu binafsi, makampuni na taasisi mbalimbali ndani na nje ya nchi. Kongamano hili litabebwa na kaulimbiu:

"Wekeza Mtwara kwa Matokeo Makubwa: Kinara wa Uchumi wa Gesi na Korosho Tanzania"
Pamoja na mambo mengine, Kongamano hilo litatoa fursa za:

- *Kufanya mawasilisho, mada na hotuba;*
- *Kupata ushuhuda kutoka kwa wawekezaji;*
- *Majadiliano ya uwili, Kampuni na Kampuni; na Serikali na Kampuni;*
- *Kuona fursa mbalimbali za uwekezaji;*
- *Kushiriki katika Usiku wa Mtwara; na*
- *Kuona fursa kubwa ya kuwekeza kwenye ufukwe wa Msangamkuu.*

Karibuni wote mshiriki na kushuhudia fursa nyingi za uwekezaji kwenye Mkoa wa Uchumi wa Gesi na Korosho Tanzania.

MTWARA Investments Forum & Expro

*Wahi Nafasi yako sasa*

Kwa taarifa zaidi tafadhali wasiliana nasi kupitia:
Simu: HOTLINE: 0677 300 500 /0754 088 461 / 0783 955 555
Barua Pepe: info@mtwarainvestmentforum.or.tz
investmentforum@mtwara.go.tz
Tovuti: www.mtwarainvestmentforum.or.tz
@mtwarainvestors mtwarainvestors

215474002

# BANK OF BARODA (TANZANIA) LTD.

## Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uonyeshaji ya Mwaka 2014)

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30.09.2019

(Kiasi kwa shilingi milion)

| | | ROBO MWAKA YA SASA | ROBO MWAKA ILIYOPITA 30.06.2019 |
|---|---|---|---|
| A. | MALI | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 3,723 | 5,016 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 23,443 | 14,819 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | 29,169 | 27,741 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 24,985 | 23,218 |
| 5 | Hundi na Mihamala ya Kushughulikiwa | 2 | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 104,343 | 103,323 |
| 12 | Mali Nyingine | 2,925 | 2,515 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,160 | 1,206 |
| **16** | **Jumla ya Mali** | **189,750** | **177,838** |
| B. | DHIMA | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 5,850 | 3,561 |
| 18 | Amana za Wateja | 140,583 | 130,884 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 397 | 137 |
| 23 | Limbikizo la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 35 | 44 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Mihamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 23 | 23 |
| 27 | Dhima Nyingine | 1,523 | 2,340 |
| 28 | Madeni | - | - |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **148,411** | **136,989** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **41,339** | **40,849** |
| C. | FEDHA ZA WANAHISA | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 10,000 | 10,000 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | 998 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 25,571 | 24,718 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 2,354 | 1,794 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 3,414 | 3,339 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **41,339** | **40,849** |
| 38 | Dhima zisizo Dhahiri | 12,954 | 15,338 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 7,138 | 6,148 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 2,227 | 1,897 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D | BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 21.79% | 22.97% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 6.69% | 5.84% |
| (iii | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 72.92% | 78.37% |
| (iv | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali | 54.99% | 58.10% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 83.53% | 86.75% |
| (vi | Ongezeko la Amana | 8.92% | -1.26% |
| (vii | Ongezeko la Mali | 6.70% | 0.17% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2019

(Kiasi kwa shilingi milion)

| | | ROBO YA MWAKA SASA 30.09.2019 | ROBO YA MWAKA LINGANISHI 30.09.2018 | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA 30.09.2019 | LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI 30.09.2018 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 3,749 | 3,441 | 10,798 | 10,320 |
| 2 | Gharama za Riba | 1,267 | 1,097 | 3,550 | 3,458 |
| **3** | **Mapato halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **2,481** | **2,343** | **7,248** | **6,862** |
| 4 | Madeni Viza yaliyofutwa | - | 1,186 | - | 1,259 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 330 | 86 | 1,110 | 412 |
| **6** | **Mapato yasiyo ya Riba:** | **180** | **287** | **1,335** | **1,363** |
| | 6.1 Faida/Hasara zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 149 | 87 | 476 | 295 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 27 | 196 | 850 | 1,055 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 4 | 5 | 8 | 13 |
| **7** | **Gharama Zisizo na Riba:** | **1,405** | **919** | **4,021** | **3,445** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 600 | 395 | 1,771 | 1,157 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 13 | 39 | 263 | 230 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 792 | 485 | 1,987 | 2,058 |
| | 7.4 Other Provision | - | - | - | - |
| **8** | **Faida/(Hasara) ya Uendeshaji** | **926** | **439** | **3,452** | **3,109** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 366 | 363 | 1,098 | 1,088 |
| **10** | **Faida/(Hasara) ya Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **560** | **77** | **2,354** | **2,021** |
| **11** | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainishi)** | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **560** | **77** | **2,354** | **2,021** |
| **13** | Idadi ya Waajiriwa | **48** | **50** | **48** | **50** |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 56 | 8 | 235 | 202 |
| **15** | **Idadi ya Matawi** | 4 | **4** | **4** | **4** |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.28% | 0.68% | 2.69% | 1.54% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 5.66% | 3.08% | 11.82% | 6.93% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 52.34% | 34.94% | 46.72% | 41.88% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 6.44% | 1.62% | 9.54% | 4.76% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO ILIYOISHIA 30.09.2019

(Kiasi kwa shilingi milion)

| | | ROBO YA MWAKA YA SASA 30.09.2019 | ROBO YA MWAKA ILIYOPITA 30.06.2019 | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA 30.09.2019 | LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI 30.09.2018 |
|---|---|---|---|---|---|
| I | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 926 | 1,151 | 3,452 | 2,743 |
| | Marekebisho kwa ajili ya: | | | | |
| | -Hasara katika Mali | 376 | 617 | 1,254 | 445 |
| | -Prior Period Adjustment | (70) | - | (70) | (639) |
| | -Badiliko Halisi Katika Mikopo | (1,351) | (5,307) | (6,879) | (2,216) |
| | -Faida/Hasara kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana | 9,700 | (4,002) | 8,425 | (698) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 1,723 | 3,526 | 5,464 | 3,811 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (2,180) | (7,341) | (6,442) | (9,157) |
| | -Kodi Iliyolipwa | (366) | (366) | (1,098) | (725) |
| | *-Mengineyo (Bainisha)* | 1,230 | (911) | 1,230 | 1,707 |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa(tumika) kwa Shughuli za Uendeshaji** | **9,989** | **(12,634)** | **5,335** | **(4,730)** |
| II | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji: | | | | |
| | -Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | -Ununuzi wa Mali za Kudumu | - | (13) | (26) | (5) |
| | -Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | -Ununuzi wa Amana zisizoshughulikiwa na Mawakala | (1,428) | 656 | (5,801) | 6,737 |
| | -Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | *-Mengineyo (ainisha)* | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(1,428)** | **643** | **(5,827)** | **6,732** |
| III | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli Kifedha: | | | | |
| | -Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | -Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | -Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | -Gawio Lililolipwa kwa Fedha Tasilimu | - | - | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | *-Mengineyo (Bainisha)* | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) Kwa Shughuli za Kifedha** | **-** | **-** | **-** | **-** |
| **IV** | Fedha tasilimu na Mali Zinazofanana na Fedha Tasilimu: | | | | |
| | -Ongezeko/ punguzo Halisi Katika Fedha Tasilimu na Mali Zinazofanana na Fedha Tasilimu | **8,561** | **(11,991)** | **(492)** | **2,002** |
| | -Fedha Tasilimu na Mali zinazofanana na Fedha Tasilimu Mwanzoni mwa Robo/Mwaka | 22,255 | 34,245 | 31,307 | 37,328 |
| | -Fedha Tasilimu na Mali zinazofanana na Fedha Tasilimu Mwanzoni mwa Robo/Mwaka | **30,815** | **22,255** | **30,815** | **39,330** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30.09.2019

(Kiasi Kwa Shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo Juu ya Bei ya Hisa | Mapato yaliyo Bakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineya (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **MWAKA WA SASA** | | | | | | | |
| **Salio la Mwanzo wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **24,134** | **3,984** | **937** | **-** | **39,055** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 2,354 | - | - | - | 2,354 |
| Mapato Mengineyo yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 570 | (570) | - | - | - |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | - | 937 | - | (937) | - | - |
| Mengineyo | - | - | (70) | - | - | - | (70) |
| **Salio la Mwisho wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **27,925** | **3,414** | **-** | **-** | **41,339** |
| **MWAKA ULIOPITA** | | | | | | | |
| **Salio la Mwanzo wa Mwaka** | 10,000 | - | 22,271 | 4,068 | 781 | - | 37,120 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 2,147 | - | - | - | 2,147 |
| Mapato Mengineyo yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 84 | (84) | - | - | - |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | - | (156) | - | 156 | - | - |
| Mengineyo | - | - | (212) | - | - | - | (212) |
| **Salio la Mwisho wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **24,134** | **3,984** | **937** | **-** | **39,055** |

**BAADHI YA MAELEKEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.09.2019**

**Katika Kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za Mwaka uliopita. (Mabadiliko katika sera za uandaaji wa taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya /mwaka wa sasa, yaelezwe kwa mujibu wa ISA 34 na ISA 8)**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Rajendra Sadashiv Mohrir (Mkurugenzi Mtendaji) | | 18th October, 2019 |
| Deogratias Edward Ndushi Mkuu wa Fedha | | 18th October, 2019 |
| Mwita Mohamed Mwita (Mkaguzi wa Ndani) | | 18th October, 2019 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasirishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya Mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Dkt. Proches Meshili Kiwango Ngatuni | | 18th October, 2019 |
| Dkt. Imanueli Daniel Mnzava | | 18th October, 2019 |

215476102

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Umuhimu NHC bado ni mkubwa

**WABUNGE** wamenusa harufu ya kukwama kwa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na kueleza mambo mengi yanayoonyesha kuwa hatima ya taasisi hiyo ya umma, si njema.

Kabla ya kuanza kuibana NHC, tunakubaliana kama taifa kuwa, nchi kuwa na shirika hilo ni njia mojawapo ya kujenga miji na kuifanya ya kisasa zaidi kupitia uwekezaji kwenye majengo na ardhi. Pamoja na kasoro zinazoibuliwa kuhusu NHC kuwa na urasimu na kushindwa kutoa ripoti za taarifa zake na utendaji kazi, wengi tunakubaliana kuwa shirika la umma kama hilo bado lina nafasi kubwa kwenye uwekezaji.

Ndilo linaloweza kuleta makazi bora kwa watu wasio na kipato, wenye kipato cha kati, kikubwa, vitega uchumi, ofisi na pia maeneo ya burudani kama hoteli. Lakini pia, tunakubaliana kuwa uwekezaji huo ni wa gharama kubwa ambao faida zake haziwezi kuonekana kwa muda mfupi na hii ndiyo hatari zaidi iwapo miradi ya NHC na usimamizi wake utafanyika bila uadilifu.

Tunakumbusha kuwa faida za taasisi kama NHC ni zile zinazopatikana baada ya muda mrefu mno kwa hiyo si lelemama.

Ni wazi kuwa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ina hoja za msingi ambazo NHC inatakiwa kuzijibu na kuzifanyia kazi. Ila pamoja na kuufuatilia ushauri wa PAC tunatoa angalizo kuwa uwekezaji kwenye majengo na ardhi (estates) ni mambo ya gharama kubwa mno ambayo faida zake huja baada ya miongo mingi hata zaidi ya mitatu lakini bila umakini unaweza usipatikane pia.

Hii ni kwa sababu eneo hili ni tofauti na masoko ya mitaji na fedha, dhamana au hati fungani za serikali.

Ndiyo maana ili shirika kama NHC liwe na tija ni lazima kuwa na uadilifu na uaminifu kwani kazi zake zinaweza pia kuhusisha, kununua ardhi, kufidia wamiliki, mikopo ya ujenzi na gharama za ununuzi wa vifaa na ujenzi. Ni wazi kuwa nyakati nyingine nyumba hizo zinahitaji kufanyiwa matengenezo, uangalizi na usimamizi wa kudumu ili ziendelee kuwa na tija na kuzalisha zaidi katika nyakati zilizopo na siku zijazo. Hata hivyo, kama taifa, ili shirika la NHC lianze kuleta faidi ni lazima kuhakikisha kuwa linakuwa na mtaji wa kutosha pamoja na uwekezaji mpana pia.

Aidha, katika mipango mojawapo ni kutekeleza jukumu la kujenga na kuuza nyumba au majengo yake kwa watu wa aina mbalimbali. Lakini, ni lazima NHC ijiendeshe kwa tija tena iwe chanzo cha mapato. Kama tulivyosema kwa kujenga nyumba na kuzikodisha wengine ambao wanazitumia kufanyabiashara. Kwa mfano, kumilika majengo ambayo hutumiwa kama hoteli, hospitali, mabweni (hosteli) au kumbi za mikutano.

Ili haya yafanikiwe ni lazima kuwa na ardhi, mtaji, wataalamu na wajuzi wa kutumia ardhi na majengo hayo kwa faida, lakini pia utambuzi wa wateja wa kimkakati kile kinachohitajika kwenye soko la nyumba kwa wakati huo.

Ripoti ya Benki ya Dunia ya Africa's Cities ya mwaka 2017, ilitaja bayana kuwa Afrika inakabiliwa na ongezeko kubwa la watu mijini lisiloendana na kasi ya huduma za makazi. Aidha, inaeleza kuwa majiji ya Afrika Dar es Salaam na Dodoma zikiwamo hayana majengo makubwa wala ofisa kutosha.

Kwa kuangalia ripoti hiyo, tunaona kuwa NHC ni muhimu mno zama hizi katika kujenga majengo ya aina mbalimbali. Kwa hiyo umuhimu wa shirika la nyumba kama hilo ni mkubwa katika mazingira ya sasa yanayohitaji uwekezaji kwenye majengo kwa ajili ya makazi na vitega uchumi.

Ripoti ya Benki ya Dunia ya Africa's Cities ya mwaka 2017, ilitaja bayana kuwa Afrika inakabiliwa na ongezeko kubwa la watu mijini lisiloendana na kasi ya huduma za makazi. Aidha, inaeleza kuwa majiji ya Afrika Dar es Salaam na Dodoma zikiwamo hayana majengo makubwa wala ofisa kutosha.

Kwa kuangalia ripoti hiyo, tunaona kuwa NHC ni muhimu mno zama hizi katika kujenga majengo ya aina mbalimbali. Kwa hiyo umuhimu wa shirika la nyumba kama hilo ni mkubwa katika mazingira ya sasa yanayohitaji uwekezaji kwenye majengo kwa ajili ya makazi na vitega uchumi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Elimu saratani ya mlango wa kizazi ni yako na yangu

Na Sabato Kasika

**MWAKA** jana, serikali ilizindua kampeni ya chanjo ya kuzuia saratani ya mlango wa kizazi, kwa ajili ya kuwafikia zaidi ya wasichana 600,000 walio na umri kati ya miaka tisa hadi 14, wapatiwe chanjo nchi nzima.

Serikali ilichukua hatua hiyo kutokana na kile kinachoelezwa kuwa saratani hiyo ni miongoni mwa magonjwa yanayosumbua wanawake nchini, hivyo kuamua kuivalia njuga kwa njia ya kutoa chanjo.

Inaelezwa na wataalamu wa afya, kwamba saratani hiyo inatokea katika chembechembe za mlango wa kizazi, ambayo ni sehemu ya chini ya mji wa mimba (uteri) inayoungana na uke.

Aina mbalimbali za virusi aina ya 'papilloma' wamethibitishwa kusababisha saratani hiyo, inayojitokeza kwa wingi miongoni mwa wanawake duniani kote, hususani wenye umri kati ya miaka 20 na 39.

Saratani ya mlango wa kizazi inatajwa kuwa ya pili miongoni mwa saratani zinazowapata wanawake na kwamba wagonjwa wapya wapatao 529,828 hugunduliwa kila mwaka, huku asilimia 85 wakiwa ni nchi zinazoendelea.

Saratani hiyo inadaiwa kuwa ya pili, baada ya saratani ya matiti kwa kusababisha vifo vitokanavyo na saratani na kwamba huchangia asilimia 10 ya vifo, vitokanavyo na saratani mbalimbali kwa wanawake.

Aidha, inakadiriwa kuwa zaidi ya wanawake 275,000 hufariki dunia kila mwaka, kutokana na ugonjwa huo, huku idadi kubwa ikiwa ni kutoka katika nchi zinazoendelea ikiwamo Tanzania.

Aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Mpoki Ulisubisya, aliwahi kukaririwa na vyombo vya habari akisema Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoongoza kwa tatizo la saratani ya mlango wa kizazi barani Afrika.

Inaelezwa, kati ya wastani wanawake 100,000, kati yao 50 wanakutwa na ugonjwa huo. Hivyo, serikali ikaamua kuanzisha kampeni ya chanjo, kwa ajili ya kudhibiti ugonjwa huo nchini.

Ni tamko la mwaka 2016 kwenye maadhimisho ya Wiki ya Chanjo Duniani, inayofanyika Aprili 27 ya kila mwaka, lengo lake ni kuhamasishwa harakati za kupunguza vifo vinavyotokana na ugonjwa huo.

Pamoja na juhudi hizo, mjadala huu umaamini kwamba bado kuna haja ya kuelimisha kwa umma kujua chanzo cha ugonjwa huo ili kuuepuka.

Ninasema hivyo, kwa sababu wataalamu wa afya wanataja visababishi ambavyo vinachangia kuwapo kwa tatizo la saratani ya mlango wa kizazi kuwa ni kuanza vitendo vya ngono katika umri mdogo.

Sababu nyingine wanazotaja, ni kuwa na uhusiano wa kimwili na zaidi ya mwanaume mmoja, maambukizu ya virusi vya HPV (Human papilloma virus). Maana hapo ni zinaa.

Wanawake wengi wanaopata ugonjwa huo, huwa na kisababishi kimoja au zaidi kinachojulikana, ambacho huongeza hatari ya kuupata baadhi ya visababishi nilivyoovitaja.

Aidha, mwanamke kuwa na uhusiano kimwili na mwanaume, mathalan mkewe alikufa kwa saratani ya mlango wa kizazi, naye ana uwezekano mkubwa wa kupata maradhi hayo.

Pamoja na chanjo, njia ambayo kwa namna moja au nyingine inaweza kusaidia juhudi za kukomesha saratani hiyo, ni elimu kwa jamii kuepuka kuharakisha kufanya ngono katika umri mdogo.

Jamii inatakiwa kutambua kuwa, saratani ya mlango wa kizazi ni tatizo na ijue na jinsi ya kuiepuka, badala ya kuingia 'kichwa kichwa' kwenye matatizo ambayo mwisho wake ni kifo.

Wataalamu wa afya, wanakumbusha kuwa muda unavyosonga zaidi, ugonjwa huo unaweza kusambaa kwenda tumboni, mapafuni au popote pale mwilini, huku dalili zikiwa ni maumivu ya mgongo.

Nyingine zinatajwa kuwa ni maumivu ya nyonga, miguu kuuma au kuvimba, uchovu, kukosa hamu ya kula, kupungua uzito, kutokwa na damu kwa wingi ukeni, kutokwa na mkojo au kinyesi ukeni na kuvunjika mifupa kwa urahisi.

Katika vita hii dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi, kuna haja kuwafikiwa wanawake vijijini na kuwapa elimu ya kutosha, kutokana na ukweli kwamba maeneo ya pembezoni yanasahaulika.

Mara nyingi, hata asasi za kiraia zimekuwa zikijikita mijini na kuwasahau watu wa vijijini, kimsingi nao wanatakiwa kuelimishwa madhara mbalimbali yanayotokana na ugonjwa huo.

HABARI KITAIFA

# Jela maisha kwa kumkata mkono mwenye ualbino

**Na Gurian Adolf,** KATAVI

WATU wanne wamehukumiwa kifungo cha maisha jela baada ya kupatikana na hatia ya kutaka kumuua mtu mwenye ulemavu wa ngozi (albino).

Mahakama Kuu Kanda ya Sumbawanga imewatia hatiani watu hao kwa kumkata mkono wake mlemavu huyo kisha kuondoka nao kwa lengo la kwenda kuuuza kwa mganga wa jadi kwa gharama ya Sh. milioni sita.

Waliohukumiwa kifungo hicho jana ni Alex Manyanza, Nogele Maliganya, Galila Malago na Shile Dalushi wote wakazi wa Mamba, Mlele mkoani Katavi.

Hukumu hiyo ilitolewa na Jaji Richard Mashauri katika Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Mkoa wa Katavi baada ya kuridhika na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka uliokuwa na mashahidi 12.

Katika kesi hiyo, upande wa mashtaka uliwakilishwa na wanasheria wa serikali Simon Peres na Dickson Makoro na washtakiwa walitetewa na mawakili Elias Kifunda na Patrick Mwakyusa.

Akisoma hukumu hiyo, Jaji Mashauri aliiambia mahakama kuwa kutokana na ushahidi uliotolewa, pasipo shaka yoyote, mahakama imeona washtakiwa wana hatia.

Jaji alisema ushahidi uliokuwa ukitolewa na upande wa utetezi wakati wa kusikiliza kesi hiyo, umekuwa ukitofautiana hali ambayo haiwezi kuifanya mahakama kushawishika na kuwaona washtakiwa hawana hatia. Pia alisema wazee washauri wa mahakama wote kwa pamoja walisema kwenye maoni yao kuwa washtakiwa hao walikusudia kuua.

Kwa mujibu wa Jaji Mashauri, kutokana na washtakiwa kupatikana na kosa hilo, Mahakama imewahukumu kutumikia jela kifungo cha maisha na kama hawajaridhika na hukumu hiyo wanayonafasi ya kukata rufani.

Haha hivyo, mahakama hiyo hiyo ilimwachia huru mshtakiwa wa sita, Masunga Kashindye, ambaye baada ya kuachiwa alitimua mbio na kutokomea kusikojulikana. Pia mshtakiwa wa tano, Michael Samuel, alifariki dunia wakati akiwa mahabusu.

Awali, waendesha mashtaka walidai kuwa washtakiwa wote kwa pamoja walidaiwa kutenda kosa hilo Mei 14, 2015 katika Kijiji cha King'anda Tarafa ya Mamba majira ya saa 6:00 usiku.

Walidai kuwa siku ya tukio, watuhumiwa walikwenda nyumbani kwa mtu mwenye ulemavu wa ngozi, Lime Luchoma, ambaye alikuwa amelala chumbani, ndipo walipojaribu kumuua kwa kumkata

INAENDELEA UK. 8

# JPM, viongozi wa AALCO wateta

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amekutana na kufanya mazungumzo na viongozi wa Taasisi ya Mashauriano ya Kisheria kwa nchi za Asia na Afrika (AALCO) ambao wanahudhuria mkutano wa 58 unaofanyika.

Rais Magufuli jana alikutana na viongozi hao wanaohudhuria mkutano huo wa siku tano ukiwakutanisha wajumbe kutoka nchi wanachama 49 na mashirika mbalimbali.

Viongozi wa AALCO waliokutana na Rais Magufuli ni Rais wa AALCO aliyechaguliwa katika mkutano huu, Balozi Dk. Augustine Mahiga (Waziri wa Sheria na Katiba, Tanzania), Makamu wa Rais wa AALCO aliyechaguliwa katika mkutano huu Prof. Mohamad Shalaldeh (Waziri wa Sheria wa Palestina), Katibu Mkuu wa AALCO Prof. Kennedy Gastorn (Tanzania) na Naibu Makatibu Wakuu wa AALCO watatu ambao ni Yukihiro Takeya (Japan), Wang Liyu (China) na Dk. Ali Garshasbi (Iran).

Rais Magufuli aliwashukuru na kuwakaribisha nchini na aliwahakikishia kuwa serikali inatambua kazi inayofanywa na taasisi hiyo tangu ijiunge nayo mwaka 1965, na kuwa mwanachama kamili kuanzia mwaka 1973.

Rais Magufuli alisisitiza umuhimu wa AALCO kutekeleza malengo ya taasisi hiyo kama alivyoelezwa na viongozi hao na alitoa wito wa kuendelea kuzitetea nchi wanachama hasa zinazowekewa vikwazo mbalimbali.

Alitolea mfano wa Zimbabwe ambayo imewekewa vikwazo kwa miaka mingi hali inayosababisha wananchi wa Zimbabwe kuteseka.

Balozi Mahiga na Prof. Gastorn walimshukuru Rais kwa kupata fursa ya kukutana nae na wameahidi kuwa AALCO itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa maslahi ya Asia na Afrika.

Mazungumzo hayo yalihudhuriwa na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Sheria na Katiba Amon Mpanju.

Wakati huo huo, Rais Magufuli amekutana na kufanya mazungumzo na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Kikomunisti cha China (CPC), Guo Yezhou, Ikulu jijini Dar es Salaam.

Rais Magufuli alimshukuru Yezhou kwa kutembelea Tanzania kwa mara ya pili na pia aliishukuru China kwa kuendeleza ushirikiano na uhusiano mzuri na Tanzania ikiwamo mchango mkubwa wa chama cha CPC ambacho kinajenga Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Julius Nyerere katika Wilaya ya Kibaha mkoani Pwani kwa ajili ya kutoa mafunzo ya uongozi kwa nchi 6 zenye vyama vya ukombozi vilivyoshirikiana na CPC ambazo ni Tanzania (CCM), Afrika Kusini (ANC), Zimbabwe (ZANU-PF), Msumbiji (FRELIMO), Angola (MPLA) na Namibia (SWAPO)}.

Rais Magufuli pia alimwomba Yezhou kufikisha shukrani zake kwa Rais wa China na Mwenyekiti wa CPC Xi Jinping kwa kutoa tuzo kwa Waziri Mkuu mstaafu wa Tanzania, Dk. Salim Ahmed Salim ikiwa ni kutambua mchango wake katika kuiwezesha China kuwa mwanachama wa Umoja wa Mataifa.

Rais Magufuli amemhakikishia kuwa Sera za Tanzania kuhusu China hazijabadilika, na kwamba Tanzania itaendelea kushirikiana na China katika jitihada mbalimbali za maendeleo.


The United Republic of Tanzania
President's Office – State House
TANZANIA SOCIAL ACTION FUND

## REQUEST FOR EXPRESSIONS OF INTEREST

Assignment Title: Consultancy Services to Conduct Impact Evaluation of the Introduction of Electronic Payment of PSSN Transfers

**Reference No.** IE/011/2017-18/HQ/C/04

Date: 24th October, 2019

1. The United Republic of Tanzania has received a grant from the Bill & Melinda Gates Foundation toward the cost for Productive Social Safety Net Project for Digitizing cash transfers and financial services for social protection in Tanzania project and the executing agent for this project is the Tanzania Social Action Fund (TASAF). TASAF intends to apply part of the proceeds of this grant for Consultancy Services to Conduct Impact Evaluation of the Introduction of Electronic Payment of PSSN Transfers.

2. The Tanzania Social action Fund now invites eligible consulting firms to indicate their interest in conducting:
   i. Baseline study to carried out before households receive ePayments.
   ii. Midline study after recipients have been receiving ePayments for 18 months/9 payments
   iii. Endline study after recipients have been receiving ePayments for 30 months/15 payments to understand the impact of the introduction of ePayments. The impact will be measured at different levels. Firstly, for individual recipients and beneficiaries (including for the unconditional cash transfer, conditional cash transfer and livelihood interventions) and, secondly, at the administrative system level (TASAF TMU, PAA, CMC). We have a third level of interest in the spill-over effects within villages where ePayments have been introduced.

3. Interested firms must provide information indicating that they are qualified to perform the services by submitting consultant's profile, description of similar assignments, experience in similar conditions, and availability of appropriate skills among staff.

4. The attention of interested Consultants is drawn to paragraph 1.9 of the Consulting services will be selected in accordance with the World Bank's Guidelines: Selection and Employment of Consultants under IBRD Loans and IDA Credits& Grants by World Bank Borrowers, January 2011 ("Consultant Guidelines"), setting forth the World Bank's policy on conflict of interest.

5. Consultants may associate with other firms in the form of a joint venture or a subconsultancy to enhance their qualifications.

6. A Consultant will be selected in accordance with the selection based on consultant qualifications method set out in the Consultant Guidelines.

7. Further information can be obtained at the address below during office hours 0900 to 1600 hours East African Time.

8. Expressions of Interest (EoI) must be addressed to Executive Director, Tanzania Social Action Fund, Jakaya Mrisho Kikwete Road, P. O. Box 2719, Dodoma, TANZANIA delivered to Tanzania Social Action Fund sub-office, Old Kilwa /Malindi Road, Main building, Third Floor, Room No. 20, Dar es salaam, Tanzania at or before 10.00 a. m East African time on **6th November, 2019.**

**Executive Director,**
**Tanzania Social Action Fund,**
**Jakaya Mrisho Kikwete Road,**
**P. O. Box 2719,**
**Dodoma, Tanzania**

215474502



Wakazi wa Kitunda Kivule, wakiangalia basi la wanafunzi lililoanguka na kuingia katika Mto Mzinga jijini Dar es Salaam jana likiwa na wanafunzi. Baadhi ya wanafunzi walijeruhiwa. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Sheria ya Ndoa kubadilishwa

**INATOKA UK. 2**

iliyochapishwa kwenye ukurasa wa Instagram.

Naye Ofisa Mipango wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Deogratius Temba, alisema sheria hiyo waliipigia kelele kwa muda mrefu na ni miongoni mwa mapendekezo waliyokuwa wakiyawasilisha serikali kila mara.

Alisema sheria hiyo ya ndoa ilikuwa kikwazo kwa watoto wa kike kushindwa kupata elimu, na kwamba walitarajia ingebadilishwa miaka iliyopita, lakini haikuwa hivyo.

"Tunawapongeza wenzetu Msichana Initiative kwa kazi nzuri waliyofanya na ushindi huu ni wa wanaharakati wote watetezi wa haki za wasichana kwa sababu ilikuwa ni kilio chetu cha muda mefu," alisema Temba.

**NDANI YA MAHAKAMA**

Mapema jana, Mahakama ya Rufani iliselima serikali ifuate maelekezo ya Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam ya kubatilisha sheria inayowabagua watoto wa kike kuolewa chini ya miaka 18, na kuamuru ifanye marekebisho ya Sheria ya Ndoa ili umri wa ndoa uanzie miaka 18.

Uamuzi huo ulitolewa baada ya rufani ya Jamhuri kupinga uamuzi wa Mahakama Kuu dhidi ya mlalamikiwa, Gyumi.

Alisoma uamuzi huo, Naibu Msajili, Eddie Fussi, baada ya kusikilizwa na jopo la majaji watatu, likiongozwa na Jaji Agostine Mwarija, Winifrida Korosso na Dk. Marry Lavila.

Kesi hiyo ya kikatiba ilifunguliwa na Gyumi na kutolewa hukumu ya kubatilisha sheria hiyo Julai, 2016.

Gyumi alikata rufani Mahakama ya Rufani ili ikaze hukumu ya Mahakama Kuu baada ya serikali kutotekeleza hukumu iliyoagiza kubatilishwa Sheria ya Ndoa za Utotoni kwamba ililenga kumlinda mtoto wa kike akimaliza darasa la saba kumwepusha na vitendo vya ndoa heri ajihifadhi kwa kuingia kwenye ndoa.

Mlalamikaji alidai kuwa kwa sababu mtoto wa kike anapevuka mapema kwa hiyo sheria namba 13 na 17 ya mwaka 1971 ilikuwa inamkinga.

**NJE YA MAHAKAMA**

Gyumi akiwa nje ya mahakama hiyo, alisema anafikiri hukumu hiyo ni maamuzi muhimu kwa wasichana wa Tanzania, na kwamba kama sehemu ya wadau waliokuwa wanafuatilia shauri hilo, imekuwa siku muhimu katika maisha yao.

"Kwetu kama shirika tunaona kuwa huu ndio ulikuwa uamuzi sahihi kulingana na vigezo ambavyo tulikuwa tumetoa... Tuna furaha sana kwa sababu tutasimamia kitu sahihi, lakini ni mshindi mzito kwa watoto wa kike," alisema Gyumi.

Alisema wana kazi mbili ya kusimamia utekelezaji wa hukumu hiyo katika kuhakikisha sheria inabadilishwa. Alisema mbali na sheria hiyo, walikuwa wanapigania haki ya mtoto wa kike kupata elimu na kujiendeleza na kuondokana na fikra za jamii za kuwakandamiza watoto wa kike.

"Sisi pamoja na watetezi wa haki za wasichana tutaendelea kufanya kazi na muhimili wa Bunge katika kuhakikisha wanaelewa umuhimu wa sheria hiyo ili iweze kubadilishwa," alisema Gyumi.






# Jela maisha kwa kumkata mkono mwenye ualbino

**INATOKA UK. 7**

mkono wake wa kulia kisha kuondoka nao kwa lengo la kuuuza kwa mganga wa jadi kwa Sh. 6,000,000.

Baada ya kuchukua mkono huo mzima, walidai kuwa washtakiwa waliondoka nao kisha kwenda kuubanika kwenye moto ili iwe rahisi kwao kuusafirisha na kwenda kuuza kwa mganga wa jadi aliyekuwa amewaagiza wamtafutie.

Katika utetezi wao mahakamani hapo, washtakiwa hao waliiomba mahakama iwaachie huru kwa madai kuwa maelezo waliyoyatoa mbele ya mlinzi wa amani katika Mahakama ya Mwanzo ya Mpanda Mjini, ambayo walikiri kufanya kitendo hicho, walikubali kosa hilo kwa kuwa walikuwa wamepata mateso baada ya kupigwa na polisi.

Wakili wa washtakiwa wa kwanza na wa pili, Kifunda, aliiomba mahakama imwachie huru mshtakiwa kutokana na kuwa na familia kubwa inayomtegemea na toka kipindi ambacho amekaa mahabusu cha miaka minne sasa, familia yake imekosa mlezi.

Pia aliomba kuwa mshtakiwa huyo bado ni kijana mwenye umri wa miaka 28, hivyo akipewa nafasi ya kusamehewa anaweza kujirekebisha na hatorudia kutenda kosa kama hilo.

Mshtakiwa wa pili aliiomba mahakama iangalie kutoa adhabu ambayo inaweza kuwa na nafuu kwake kutokana na yeye kuwa na umri mkubwa wa miaka 44 na familia yake bado inahitaji malezi kutoka kwake.

Wakili Mwakyusa aliyekuwa akiwatetea mshtakiwa wa tatu na wa nne, aliomba huruma ya Jaji kwa kuwa mshtakiwa wa tatu kwa kuwa ana watoto tisa wanaomtegemea na kwa sasa wanaishi na babu yao baada ya mama yao kuwakimbia baada ya mshtakiwa kuwa mahabusu kwa muda mrefu.

Mshtakiwa wa nne binafsi, aliomba mahakama imwachie huru kwa kuwa ana umri mdogo wa miaka 31 na mke wake amefariki wakati akiwa mahabusu na ameacha watoto watatu. Pia aliomba kuachiwa huru kwa kuwa kosa hilo ni la kwanza kwake.

Baada ya utetezi huo, Wakili wa Serikali Peres, aliiambia mahakama hiyo kuwa matukio ya ukataji wa viungo kwa watu wenye ulemavu wa ngozi ni vitendo vya ukatili ambao hauvumiliki kwa watu wa dunia nzima.

Alidai kuwa vitendo hivyo vinawafanya watu wenye ulemavu kutoishi kwa amani katika dunia hii waliopewa na Mungu, jambo ambalo limesababisha kuwa wakimbizi kwenye makazi na familia zao na kuishi kwenye maeneo tengefu.

Pia alidai kuwa jambo hilo ni la kusikitisha, hivyo kuiomba mahakama itoe adhabu kali inayostahili kwa watuhumiwa kwa mujibu wa sheria.

## HABARI KITAIFA

# Wamiliki hoteli wakaidi kikaangoni

**Na Frank Monyo**

BODI ya Maji Bonde la Wami/Ruvu, imesema itawapeleka mahakamani wamiliki wa hoteli 73, kampuni 13 na vituo vya mafuta 14 ambao wamekaidi kulipa ada ya mwaka ya watumia maji ya visima jumla ya Sh. 32,8,53,000.

Ofisa wa Bonde la Wami/ Ruvu, Simon Ngonyani, alisema ofisi yake imetoa notisi ya madai kwa wamiliki hao 100 ambapo baadhi yao walilipa Sh. 49,230,000.

Alitaja waliopelekwa mahakamani ni Dar Self Hotel, Mapumziko Hoteli, G&P Hoteli, Simba Oil, Manyangwe hotel, Iceland Hoteli na Lunch Time Hoteli.

"Tulikuwa na jitihada za kuwatafuta watu ambao walikuwa hawalipi ada za matumizi ya maji ya visima, na wapo wachache ambao tumewapeleka mahakamani kwa kukaidi takwa la kisheria la kulipa ada za watumia maji ya visima na wakalipa, huku wengine wakiahidi kulipa pasipo utekelezaji," alisema Ngonyani.

Baadhi ya hoteli ambazo zinadaiwa ni BnB , Confidence, Don Lodge na Grand Villa. Kwa upande wa vituo vya mafuta ni TSN Oil, Gapco (T) LTD, Mantrac (T) LTD na Lake Group (Lake Oil) zote za Dar es Salaam. Ngonyani alitoa tahadhari kwa wamiliki wa hoteli, kampuni na vituo vya mafuta kuwa katazo la Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa juu ya wamiliki wa visima vya majumbani kutolipa ada ya mwaka haiwahusu wao.

"Kumekuwa na sintofahamu baada ya tamko la serikali mwaka huu juu ya kufuta tozo za matumizi ya maji ya visima majumbani, hivyo kusababisha watumia maji kukaidi ulipaji wa tozo za maji za visima," alisema Ngonyani na kuongeza: "Tozo iliyofutwa ni ada za mwaka za matumizi ya maji ya visima majumbani iliyokua Sh. 100,000 kwa mwaka kwa kila kisima kwa shughuli za nyumbani tu na sio kuuza maji. Aidha, tozo zinazotakiwa kulipwa kwa matumizi ya nyumbani ni; gharama za usajili wa kisima Sh. 60,000, gharama za kuomba kibali ya kuchimba kisima Sh. 150,000." Kwa mteja ambae hajachimba kisima na gharama za upimaji wa ubora wa maji ni Sh. 241,000, na mwenye biashara na anatumia maji ya kisima ni lazima alipe tozo za maji za mwaka.

Alisema ulipaji wa ada hizo ni muhimu kwani husaidia bodi kutekeleza shughuli za utunzaji wa rasilimalli za maji zitakazohakikisha upatikanaji wa maji kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi na kutimiza azma ya nchi kufikia uchumi wa viwanda.

Aliongeza kuwa ulipaji wa ada za matumizi mbalimbali ya maji ni takwa la kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na.11 ya mwaka 2009 kifungu cha 43 (1) ambacho kinamtaka mtu yeyote anayetaka kuchepusha, kukinga, kuhifadhi, kuchukua na kutumia maji kutoka kwenye chanzo cha maji juu ya ardhi au chini ya ardhi au kujenga miundombinu yoyote lazima aombe kibali cha kutumia maji.

Alisema kuwa watu ambao wanachimba visima kiholela hasa kipindi hiki cha mvua wanakuwa katika hatari za kupata magojwa ya mlipuko kwani uchafu unaosombwa na maji ya mvua unaweza kupelekwa hadi kwenye visima kutokana na kutochimbwa kitaalamu.



Mchuuzi wa mbwa, akiwa amemfunga kamba mguuni ili asitoroke huku wakiwa 'wameuchapa' usingizi wakati akisubiri wateja, kando ya Barabara ya Bagamoyo, eneo la Victoria, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Umeme waahirisha hukumu ya 'Tereza'

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

MAHAKAMA ya Wilaya Mkoa wa Kigoma, imeahirisha hukumu ya kesi inayomkambili mkazi wa Mwanga Vamia Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Hussein Rajabu 'Tereza' hadi Oktoba 29, mwaka huu kwa ajili ya kusomewa hukumu.

Mshtakiwa huyo anakabiliwa na makosa mawili ya kuvunja nyumba na kumchoma kisu shingoni Shukran Almas, na kumsababishia majeraha shingoni.

Mshtakiwa huyo alipandishwa kizimbani jana mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Kenneth Mutembei. Awali aliposomewa mashtaka, alikana na yuko mahabusu katika Gereza la Bangwe kwa kukosa wadhamini.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Benedict Kivuma, ulidai kesi hiyo imekuja hapo mahakamani kwa ajili ya hukumu, huku na upande wa utetezi ukidai uko tayari kusikiliza hukumu.

Hakimu Mutembei alisema hukumu hiyo haijachapwa kutokana na kukosekana kwa umeme, hivyo kuiahirisha hadi wiki ijayo.

Awali hakimu huyo aliyataja masharti ya dhamana ni kuwa na wadhamini wawili wenye barua ya utambulisho kutoka kwa ofisa mtendaji wa kata na mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. milioni moja.

Awali akisoma hati ya mashtaka Kivuma alidai Mei 20, mwaka huu majira ya usiku maeneo ya Mwanga Vamia, mshtakiwa alivunja nyumba ya Shukrani Almasi na kuingia ndani kisha kumchoma kisu shingoni na kumsababishia majeraha shingoni.

# Sababu kibano makandarasi Dar

**Na Beatrice Moses**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, amewapa siku tano makandarasi wanaosuasua kwenye miradi ya ujenzi wa miundombinu, na kuwa atawakamata na kuvunja mikataba yao.

Makonda aliyasema hayo kutokana na hali ya kusuasua kwa baadhi ya makandarasi waliopo kwenye Mkoa wa Dar es Salaam kutokana na nyaraka za uongo walizoziwasilisha wakati walipoomba zabuni ya miradi waliyokabidhiwa ambayo ipo inayotimiza miezi mitatu lakini bado haijaanza kutekelezwa.

Uongo uliouonyesha kwenye maombi kupitia nyaraka ulizojaza pesa walizoonyesha wewe ni 'class one', una pesa za kutosha, una vifaa vya kutosha na baadhi ya makandarasi nimebaini hata vifaa hawana hata hizo fedha walizozionyesha kwenye makaratasi hawana fedha wala vifaa.

Alisema baadhi ya makandarasi hao wamekuwa wakizungusha fedha za '[mobilization' kwenye miradi mingine kwa kuwa hawana fedha, hivyo wamekuwa wakikwamisha kukamilisha kwa miradi tofauti na muda uliopangwa.

Alizionya bodi zote katika Mkoa wa Dar es Salaam zinazotoa zabuni kwa makandarasi wasio na uwezo nao watashughulikiwa ikiwamo kufukuzwa kazi.

Aliitaja baadhi ya miradi hiyo ni ujenzi wa barabara ya Kivule, Buguruni Kisiwani, Mto Ng'ombe na barabara ya Kawe.

"Mnafahamu uwezo wangu na sina kigugumizi kwenye hatua, makandarasi wanafanya mchezo kwa sababu aidha walipata kazi kwa kuhonga na waliowahonga wanashindwa kuwasimamia.

Alisema alishawaeleza makandarasi wenye changamoto ya malipo ofisi yake na ya Katibu Tawala wa Mkoa ipo wazi wafike ili wasaidiwe kukamilishiwa malipo yao, lakini kumekuwa na ukimya.

Makonda alibainisha atashughulika na makandarasi wote wanaotekeleza miradi katika mkoa wake, hata kama waliingia mikataba na wizara mradi miradi hiyo inahusu mkoa wa Dar es Salaam, atatumia mamlaka aliyonayo kuwabana ipasavyo.

# Watoa leseni kwa madereva washauriwa

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MAMLAKA zinazohusika na utoaji wa leseni kwa madereva zimetakiwa kutoa kwa kuzingatia sheria na vigezo vinavyohitajika, ili kupunguza ajali zinazoweza kuepukika.

Akizungumza na Maofisa Usalama Barabarani katika wilayani Chakechake, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Bima Zanzibar, Abdulnassir Ahmed Abdulrahman, alisema ipo haja kwa mamlaka zinazohusika kuangalia upya suala la utoaji wa leseni hasa kwa vijana.

Alisema ni vyema kwa mamlaka zinazohusika na utoaji wa leseni kwa madereva zihakikishe wanaowapa leseni hizo wanastahili kupewa, hatua ambayo itapunguza ajali zisizo za lazima.

"Kwa kweli hizo leseni zinavyotolewa siku hizi ni mtihani, anapewa mtu asiyestahili pia.... tumeona leseni mpaka ya miaka mitano, hivyo tunaomba iwepo sheria kwamba ili mtu apewe leseni, angalau awe na umri wa miaka 30," alisema mkurugenzi huyo.

Aidha, aliwataka maofisa hao wasimamie gari inapopata ajali isifunganishwe na kitambaa au kamba na gari lingine, kwani inaweza kusababisha ajali nyingine.

Akiwasilisha mada katika mkutano huo, Mkurugenzi wa Kanda kutoka Shirika hilo, Imam Ali Makame, alisema kuna changamoto mbalimbali zinajitokeza kipindi cha kushughulikia madai ya wateja, ikiwa ni pamoja na ucheleweshwaji wa taarifa za ajali kutoka kwa wadai.

"Changamoto nyingine ni ucheleweshwaji wa vielelezo muhimu vya madai, uandishi wa bima usiofuata uweledi na misingi ya bima, madai ya udanganyifu, kukosa imani na kutokuwa na subira kwa wadai," alisema.

Alieleza ili kupunguza ajali, aliziomba mamlaka zinazohusika kuweka sheria kali kwa wanaendesha vyombo kwa kasi, vyombo vya baharini visiruhusiwe kubeba abiria mpaka vipate kibali maalum na madereva wanaosababisha ajali mara kwa mara wanyang'anywe leseni na wapewe adhabu kali.

Naye Mkuu wa Kituo cha Shirika la Bima Unguja, Amina Mzee Ibrahim, aliwaomba maofisa hao kutoa taarifa inapotokezea ajali, ili kushughulikiwa madai kwa haraka.

"Ripoti za polisi zinachelewa na ndio maana wateja hukaa muda mrefu, hivyo tushirikiane katika kuhakikisha vielelezo vinafika kwa haraka ili kuepusha changamoto," alisema.

Mratibu Msaidizi wa Polisi, Yasin Ali Haji, aliliomba shirika hilo kuandaa mikakati ya kutoa elimu zaidi hasa vijijini ili na wao wajifunze, kwani ameelewa kuwa bima ni akiba.

"Kuna siku tulifanya msako na kukamata madereva wenye bima feki na zilikuwa na vielelezo vyote vya shirika lenyewe, ingawa hatukuona mtendaji yeyote wa shirika hilo kuwajibishwa, lakini madereva waliambiwa wakate nyingine, tunataka kujua nani anayetoa bima feki," alifahamisha Nassor Juma, Polisi kutoka Mkoani.

Naye Polisi Ali Nasib kutoka Wete, alisema ipo haja ya kufanyiwa marekebisho ya sheria, ili wote wakate bima, kwani faini ni ndogo na ndio maana wanadharau.



Baadhi ya vijana wakimsaidia mwenzao kumbebesha mkungu wa ndizi ili kujipatia riziki katika kivuko cha Kamanga jijini Mwanza juzi. **PICHA: ELIZABETH FAUSTINE**

# Madaktari watoa mimba wanafunzi sasa kukiona

**Na Gurian Adolf,** NKASI

WILAYA ya Nkasi mkoani Rukwa, imesema itaanza kuwachukulia hatua kali baadhi ya madaktari wanaowatoa mimba wanafunzi kwa kuwa ndiyo wanaosababisha wanafunzi kuendelea kujihusisha na vitendo vya mapenzi na kuendelea kubeba mimba. Mkuu wa Wilaya hiyo, Said Mtanda, alitoa onyo hilo wakati akifungua kikao cha wajumbe wa kamati ya mkakati wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto wilayani Nkasi. Alisema wapo baadhi ya watumishi wa afya ambao ni madaktari, ambao wamekuwa wakipokea fedha kutoka kwa watu wanaowapa mimba wanafunzi na kuwatoa, hali inayosababisha wanafunzi kuendelea kujihusisha na mapenzi kwa kuwa wanajua wakipata ujauzito watatoa. Mtanda alisema serikali haitawafumbia macho watumishi hao wa umma, na itaandaa mkakati wa kuwabaini na kuwachukulia hatua kwa kuwa utoaji mimba ni kinyume cha sheria.

"Nachukua nafasi hii kuwaonya baadhi ya madaktari wanaojihusisha na vitendo vya kuwatoa mimba wanafunzi kwa lengo la kujipatia fedha... atakayebainika tutamchukulia hatua kali za kisheria, kwani hao ndio wanaorudisha nyuma jitihada za kupambana na mimba kwa wanafunzi," alisema.

Mratibu wa Taasisi isiyo ya Kiserikali ya Community Economic Empowerment and Legal Support (CEELS), Godbless Konga, alisema wameamua kukutana na wajumbe hao ili kuweka mikakati ili kukomesha vitendo hivyo.

Alisema kuwa wilaya ya Nkasi inakabiliwa na tatizo la mimba za ututoni ambapo katika Januari hadi Agosti mwaka huu, wanafunzi 24 wa shule za msingi wamepata ujauzito, na katika kipindi hicho, wanafunzi 75 wa shule za sekondari wamepata ujauzito.

# Tuhuma rushwa zawaweka matatani mwanajeshi, polisi

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

MWANAJESHI na askari polisi ni miongoni mwa watu wanne waliotiwa mbaroni na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Kagera, kwa tuhuma za kuomba na kupokea rushwa.

Taasisi hiyo imesema imewakamata watu hao wanne kwa tuhuma mbalimbali wilayani Biharamulo mkoani humo.

Mkuu wa Takukuru mkoani Kagera, John Joseph, aliwaambia wanahabari jana kuwa Oktoba 12, mwaka huu, walimkamata askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Koplo Nyambita Magoma, ambaye ni mkufunzi ofisi ya Mgambo katika Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo.

Alisema akiwa katika Kijiji cha Nemba, askari huyo alikamata ng'ombe wa mkazi wa wilaya hiyo kwa madai ya kuwa wameingia katika msitu wa akibai na kuomba rushwa ya Sh. milioni 3 ili asimchukulie hatua za kisheria.

"Askari huyo aliomba Sh. milioni 3 kutoka kwa mwananchi huyo kwa madai kuwa ng'ombe wake wameingia katika hifadhi kinyume cha sheria," alisema Joseph.

Aliongeza kuwa askari huyo alishikilia mifugo hiyo hadi alipopatiwa Sh. 1,800,000 kisha kumwanchia mwananchi huyo.

Aidha, Takukuru inashikilia watu wengine wawili akiwamo askari polisi wa kituo cha Runazi, Koplo Nassor Maulid, kwa tuhuma za kushirikiana na ofisa misitu wa halmashauri hiyo kuomba rushwa ya Sh. 700,000.

Kwa mujibu wa Joseph, wawili hao waliomba fedha hizo kutoka kwa mfanyabiashara ya mkaa aliyekuwa amebeba magunia 50. Alisema Koplo Maulid alipokea fedha hizo kwa awamu mbili, ambapo ya kwanza alipokea Sh. 250,000 na kupokea tena Sh. 148,000 kabla ya kukamatwa.

Katika hatua nyingine, Joseph alisema kuwa ofisa wa halmashauri hiyo, Audax Norbert, anatuhumiwa kwa kuomba rushwa kutoka kwa mfanyabiashara ya bucha Sh. 200,000 ili asimfungie bucha baada ya kumkuta na makosa katika shughuli za ukaguzi.

Aliongeza kuwa mfanyabiashara huyo alimpatia ofisa huyo shilingi 50,000 kwa hofu ya kufungiwa bucha yake.

Joseph alieleza kuwa uchunguzi wa tuhuma hizo ukikamilika, watuhumiwa hao watafikishwa mahakamani.

# Mtambo kuchuja hewa magari, viyoyozi watua

**Na Allan Isack,** ARUSHA

KATIKA hatua za kukabiliana na uchafuzi wa mazingira na hewa, kituo cha umahiri cha utafiti wa maji cha Wise-Future kwa kushirikiana na wadau wengine kumegundua mtambo wa kusafisha hewa kwenye injini za magari na viyoyozi.

Wise Future amefanyakazi hiyo ikishirikiana na taasisi za Kotra Art plus na Koica kutoka Korea Kusini.

Akizungumza wakati wa kuzindua mtambo huo, kiongozi msaidizi wa kituo cha umahiri cha utafiti wa maji cha Wise-Future, Yusufu Jande, alisema mashine hiyo, itatumika kufanya majaribio ya vichujio vya hewa kwenye magari na viyoyozi.

Alisema lengo la kuanzishwa kwa mtambo huo, ni kuhakikisha hewa inayotumika kwenye mazingira ya binadamu inakuwa salama na haina virusi wala bakteria.

Alisema kuzinduliwa kwa mtambo huo, kutakuwa na manufaa kwenye jamii kwani hata wanafunzi wataweza kujifunzia kwa vitendo. "Wanafunzi wetu katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST) ya Arusha, wataweza kutumia mashine hii kufanya tafiti mbalimbali na kuzalisha malighafi mpya,"alisema Jande.

Alisema katika majaribio wanafunzi watatumia mashine hizo, kufanya utafiti wa kutambua aina za virusi na bakteria ambao wanaleta madhara kwenye jamii kupitia mfumo wa hewa.

Alisema kupitia mtambo wa mashine hiyo watafanya majaribio kwa vitendo vichujio vipya ambavyo vinazalishwa na kampuni mbalimbali ili kuthibitisha kwamba vichujio hivyo vina ubora unaotakiwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Kotra Hong Kyun Lee, alisema kuzinduliwa kwa mashine hiyo kutachangia na kuongeza kufanyika kwa tafiti mbalimbali hususani za uchafuzi wa mazingira.

"Dunia inakabiliwa na tatizo la utandawazi na mabadiliko ya tabianchi na ukiangalia nchi zinazoendelea kamaTanzania zinatatizwa na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi kutokana na miradi mingi ya ujenzi wa nyumba kubwa yanayoendelea kujengwa, viwanda, magari na mitambo yote haya husababisha uchafuzi wa hali ya hewa, lakini mashine hizi kwa kiasi itaweza kusaidi kupima hewa na kutoa tahadhari,"alisema Lee.

"Kwa mujibu wa takwimu za shirika la afya duniani "WHO" za mwaka 2018, zinaonyesha watu 1,000,000 Afrika kila mwaka wanapoteza maisha kutokana na uchafuzi wa mazingira, aliongeza Lee.



Mhifadhi na mwakilishi kutoka Hifadhi ya Taifa ya Arusha, Tegemea Exaudi, aking'oa gugu karoti, wakati wa mkutano wa kujadili udhibiti wa gugu karoti katika makao makuu ya Taasisi ya kudhibiti viuatilifu Tanzania (TPRI), hivi karibuni. **PICHA: DANIEL SABUNI**

## Taasisi ya kidini yamshukuru Mghwira kwa kuwapa ardhi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

TAASISI ya Kiislamu ya Waviqatal Qadiriya Jailaniya Arazaqiya (TWARIKA), imemshukuru Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, kwa kuwaahidi kuwapatia ardhi kwa ajili ya ujenzi wa shule, hospitali na msikiti.

Aidha, imemshukuru Meya wa Manispaa ya Moshi, Raymond Mboya, kupitia Chadema kwa kuwapatia mabati 100 na kuahidi mengine 150 kwa ajili ya ujenzi huo.

Msemaji Mkuu wa taasisi hiyo, Sheikh Haruna Hussein, akizungumza jijini hapa, akiwa amembatana na Shekhe wa Mkoa wa Kilimanjaro, Amini Mushi, alisema ardhi waliyopewa ni ekari 50, kwa ajili ya ujenzi wa msikiti mkubwa wa kisasa, hospitali ya mama na mtoto pamoja na ujenzi wa shule yenye madarasa 12, kuanzia chekechekea hadi shule ya msingi na ukumbi wa mikutano wa kimataifa.

"Taasisi ya Twarika Tanzania ina malengo makubwa, tulikuwa na wazo la kukusanya Sh. 100 kwa kila muumini hadi tupate fedha za kununua ekari 50, tunajua zoezi hilo lingechukuwa muda, lakini tumeshukuru viongozi wetu kwa kutusaidia," alisema.

Alisema wameshakwenda Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ajili ya kupeleka barua ya kuomba eneo hilo ambalo watalitumia kwa ajili ya ujenzi. "Tuliporudi Moshi makao makuu ya taasisi yetu, Julai mwaka huu na Mkuu wa Mkoa alisema atatusaidia kupata eneo hilo," alisema sheikh Haruna.

"Kipekee nimshukuru Mstahiki Meya wa Manispaa ya Moshi, Raymond, kafanya jambo kubwa sana na Waislamu tunatakiwa tuige, kutoa tulichopewa kusaidia msikiti kama ambavyo Meya amechangia milioni tano pamoja na mabati."

Alisema viongozi wanatakiwa kuwa mfano katika jamii kwa sababu wanaiongoza jamii inayowazunguka na hawapaswi kuangalia dini wala kabila wala rangi ya mtu.

Sheikh huyo alisema wameandaa kongamano kubwa la kimataifa ambalo washiriki watatoka Rwanda, Burundi, Kenya na wenyeji Tanzania.

Kongamano hilo, litafanyika mkoani Kilimanjaro na kauli mbiu yake itakuwa 'amani ya Watanzania mwaka 2020, uchaguzi upite salama'.

"Tunahitaji uchaguzi upite salama kwa sababu Watanzania wanahitaji amani kwa maslahi ya kizazi kijacho na kupinga viashiria vyote vya machafuko," alisema Sheikh Haruna.

# 'Wasichana jamii za kifugaji waambiwa someni kwanza'

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WASICHANA wa jamii ya kifugaji wametakiwa kusoma kwa bidii hadi kufikia malengo ya kimaisha, badala ya kukimbilia kuozeshwa wakiwa wadogo hali inayowakwamisha kimaisha.

Hayo yalisemwa na Meneja wa Benki ya NMB Tawi la Ngaramtoni ,Lembris Lession, wakati akizungumza na wazazi na wanafunzi wakati wa mahafali ya 13, ya Sekondari ya Mwandeti ambayo wanafunzi 320 wanahitimu kidato cha nne .

Alisema nyakati hizi wanafunzi wanatakiwa kusoma kwa bidii ili kutimiza ndoto zao na kuziweka kando mila potofu za kuozwa wakiwa na umri mdogo badala yake wajikite zaidi katika elimu na mambo mengine yatafuata baadaye.

Aidha, aliongeza kuwa,umefika wakati sasa wa watoto kutambua umuhimu wa elimu na kuhakikisha kila mmoja anafikia malengo waliyojiwekea na hatimaye kupata kazi bora au kujiajiri watakapohitimu elimu ya juu.

Aidha aliwataka wanafunzi hao, kuchukua tahadhari ya kuondokana na makundi yasiyofaa watakapokuwa mtaani na waishi maisha bora waliyolelewa na walimu wao wakiwa shuleni, wazazi na walezi nyumbani sambamba na kumtanguliza Mungu na kuwa na nidhamu.

Mkuu wa shule hiyo, John Massawe alisema pamoja na kuwepo kwa mafanikio makubwa kwa wanafunzi hao, kufanya vizuri katika matokeo ya kidato cha nne na cha sita bado wanakabiliwa na changamoto kubwa ya upungufu wa nyumba za walimu na kwamba zilizoko ni tisa .

Changamoto hiyo imesababisha mahudhurio ya waalimu kwenye vipindi kuwa madogo kwani wengine wanatembea umbali mrefu hadi kufika shuleni hapo, na wakati wa mvua wanashindwa kuingia darasani kufundisha kwa kuhofia kunyeshewa na mvua barabarani au kuvuka mito njiani.

" Nyumba za waalimu ni chache mara nyingi huchangia nyumba moja na walimu wengi wanashindwa kufika shuleni kwa wakati kutokana na umbali uliopo na usafiri ni wa shida hadi kufika shuleni. Kipindi cha mvua makorongo hujaa maji hivyo wanashindwa kuwahi au kuhudhuria vipindi." Ali omba serikali pamoja na wadau mbalimbali kusaidia kutatua changamoto hiyo ambayo inasumbua kwa muda mrefu. Aidha, alizungumzia suala la maadili akisema: "Wazazi tunaomba sana msikatishe ndoto za watoto wenu kwa kuwaachia uhuru wa kujichanganya na vijana wasiokuwa na maadili ambao wataweza kuwapotosha ,pia nawasihi sana wahitimu muwe makini na mitandao ya kijamii ambayo mkiitumia vibaya itawapotosha na kuwapotezea ndoto zenu."

Akisoma risala kwa niaba ya wahitimu wengine, Japhet Simon, alisema pomoja na changamoto hizo, shule hiyo imekuwa ikifanya vizuri katika mitihani.

Mwanafunzi huyo aliishukuru serikali kwa kuleta mpango wa sera ya elimu bure ambayo imehamasisha wazazi na walezi wengi kuwa na mwamko wa kupeleka watoto shuleni.

# Uhaba wa chakula waibua kampeni

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

UHABA wa mazao ya chakula uliozitikisa baadhi ya wilaya mkoani Kilimanjaro msimu uliopita wa masika, umeisukuma Ofisi ya Umwagiliaji ya Kanda ya Kaskazini, kuanza kampeni ya kuhamasisha wakulima kutumia wataalamu wa ughani hasa vijiji vinavyotegemewa kwa kilimo cha umwagiliaji.

Mhandisi wa umwagiliaji Mkoa wa Kilimanjaro, Said Hussein, alisema kampeni hiyo inalenga kuamsha hisia za wakulima kutumia wataalamu, badala ya kuendelea kuwaza kilimo cha mazoea.

Alikuwa akizungumza jana na Nipashe katika mahojiano maalum kuhusu idadi ndogo ya wakulima wanaowaza kujikita katika sekta ya umwagiliaji.

"Tumeamua kwenda vijijini lakini kupitia vyombo vya habari tuna mkakati maalum wa kuhamasisha kilimo cha umwagiliaji ni lazima kizingatie kanuni za kilimo kama kutumia maafisa ughani ili kutoa elimu. Kiwango cha mazao kinachopatikana hakilingani na eneo lililotumika au nguvu kazi inayotumika," alisema Mhandisi Said.

Ofisi hiyo imeeleza kuwa wakati umefika sasa kwa wakulima kujishughulisha na kilimo cha umwagiliaji, badala ya kuelekeza nguvu katika kilimo cha kutegemea mvua.

Alitaka wilaya zinazojihusisha na kilimo cha umwagiliaji kuanza mchakato wa kuwaondoa ofisini maofisa ughani kwenda vijiji na kwamba kwa sasa upo mpango mkakati wa kutengeneza mabwawa kwa ajili ya kuvuna maji.

Kwa upande wake, Mtaalamu wa Mimea na Udongo kutoka Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, Martin Izidory Francis, aliwataka wakulima kuhakikisha wanapata maelekezo kutoka kwa wataalamu wa kilimo kabla ya kufanya shughuli hiyo ili kuepusha madhara ikiwamo kupata hasara.

Joshua Ayoub Semwenda ni Ofisa Elimu kutoka Tume ya Umwagiliaji Kilimanjaro, yeye alisema jambo la muhimu linalofanywa kwa wakulima ni kuelimishwa ili wafahamu namna bora ya kufanya kilimo cha umwagiliaji lengo likiwa ni kuinua pato la mkulima mmoja mmoja na taifa.

# Tozo za ardhi zampa wasiwasi Mabula

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

USIMAMIZI mdogo wa halmashauri za wilaya nchini katika tozo zinazohusiana na utatuzi wa migogoro ya ardhi ambayo hutozwa na mabaraza ya ardhi ya vijiji na kata, unampa wasiwasi Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula.

Mabula alionyesha wasiwasi huo jana, baada ya kukamilisha ziara yake ya kutembelea wilaya za Hai na Rombo, mkoani Kilimanjaro na kuzungumza na watendaji wa idara za ardhi na kufanya mkutano wa hadhara na wananchi.

"Kama kuna tatizo lingine kubwa lipo hivi sasa ni mabaraza ya ardhi ya kata na vijiji. Naliona kabisa tatizo bado lipo kwa wakurugenzi. Nikiuliza hapa mna bajeti kiasi gani ya mabaraza ya ardhi ya kata na vijiji, je, mnajua wanatoza kiasi gani katika zile kesi wanazozisimamia, kwa mfano anatoka anakwenda site (eneo lenye mgogoro) kuangalia mgogoro wa mpaka wanatoza kiasi gani?

"Wanachotoza ni kiwango ambacho kinafahamika au ni wao wenyewe (mabaraza) wanaamua kwa kumwangalia huyu amevaa suti nzuri, huyu tutamtoze Sh. 50,000 huyu tumtoze Sh. 100,000. Lakini mnajua wanakusanya kiasi gani?

Hata kama zinatakiwa zitumike kule, wilaya kama wilaya inajua? Je, mnawawekea bajeti ya shajara au nazo wanajipangia wenyewe?"Alihoji Naibu Waziri Mabula. Mfumo wa utatuzi wa migogoro ya ardhi, unatokana na maoni yaliyotolewa na Tume ya Profesa Issa Shivji ya Mwaka 1992, yaliyofuatiwa na Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995.

Sera inasisitiza kuanzishwa kwa vyombo maalum vitakavyohakikisha kuwa utatuzi wa migogoro ya ardhi unakuwa wa haraka na wa haki. Sera ilipelekea kutungwa sheria mbili za ardhi mnamo mwaka 1999 yaani Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Sura ya 114 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002.

Katika vikao vyake na watendaji wa ardhi, Naibu Waziri huyo kwa nyakati tofauti alisema mabaraza hayo ni kama hayasimamiwi, kwa sababu unakuta mkurugenzi wala hajui, hawapati semina, hawapi elimu wasimamieje mabaraza, hajui tozo lao ni kiasi gani, hivyo kusababisha kesi zinazokwenda kwenye Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya zitakuwa nyingi.

Kwa mujibu wa Mabula, "Appeals" ni nyingi (rufani), malalamiko ni mengi lakini ukiwawezesha huku chini kesi zitaishia kwenye vijiji, zitaishia kwenye kata. Watakuwa wamewezeshwa kwenye elimu, kwenye shajara lakini na viwango wanavyotoza vitakuwa vinafahamika kwa mwananchi yeyote."

Kutokana na udhaifu huo, amezitaka halmashauri zote nchini kuangalia umbali na eneo na kuweka wastani wa tozo hizo kwa viwango rafiki, na watendaji wa kata wapewe maelekezo ya kuangalia au kusimamia zoezi la utatuzi wa migogoro katika mabaraza hayo ili isitokee mwenye nacho, akahonga fedha nyingi na wajumbe wakaegemea kwa aliyewapa nyingi nyingi.

Alisisitiza wizara hiyo inayo taarifa za mabaraza mengi kupitwa na wakati na halmashauri hazijatoa msukumo wa kuyahuisha na wala hayapewi semina.



Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga (wa pili kushoto), akikata utepe kuzindua vitabu vya Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania (TACRI), kwa ajili ya kutoa elimu kuhusu kanuni bora za utunzaji wa kahawa aina ya Arabika na Robusta, pamoja na mitaala ya mafunzo, katika eneo la Lyamungo, mkoani Kilimanjaro juzi. Wa pili kulia ni Mkuu wa Mkoa huo, Anna Mghwira. **PICHA: WIZAYA YA KILIMO**

# Wachangia kituo cha wenye ulemavu

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MWASISI wa kituo cha elimu na makazi ya yatima na jamii ya watu wenye ulemavu cha Mawela Rehab Centre, Padri Apollianaris Ngao, amesema wahisani waliojitokeza kusaidia ujenzi wa mradi huo wametoa kiasi cha Euro 375.

Taarifa ya Padri Ngao aliyoichapisha jana katika ukurasa wake wa moja ya mitandao ya kijamii, inaeleza kuwa idadi ya watu waliokuwa wameombwa kuchangia pia mradi huo walikuwa ni 2,896. Kituo hicho ambacho ni jengo la ghorofa mbili, kinajengwa katika Kijiji cha Okaseni, Kata ya Uru Kusini, Moshi Vijijini.

Mwasisi huyo anaishi nchini Ujerumani, akifanya kazi za kichungaji na Muungano wa Parokia tano za zikiwamo za St. Paul, St. Joseph na Konrad zinazosimamiwa na Jimbo Katoliki la Ausburgy.

"Tunamshukuru Mungu na wote ambao wamevutwa kuchangia mradi huu wa kuwasaidia wenye uhitaji na hasa wanaokosa makazi ya kudumu, kutelekezwa na familia zao na wengine kufukuzwa na wazazi wao kutokana na kupata ulemavu. Hii ni sadaka pekee kwa Mungu wao," alisema.

Mwezi Februari mwaka huu, baadhi ya wafadhili kutoka nchini Ujerumani waliounga mkono ujenzi huo ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Uhandisi ya Bauunternehmen XGERBL, Franze Gerbl na wakurugenzi wenza wa Kampuni ya Bureau Veritas 1828, Vitus Lenz na Waltraud Lenz. Kwa mujibu wa Padri Ngao, ujenzi wa kituo hicho hadi kukamilika kwake unatarajiwa kugharimu zaidi ya Sh. bilioni 1.2

Wazo la kuanzishwa kituo hicho, lilitokana na Padri Ngao aliyepata malezi ya kiroho katika Parokia ya Mawela ya Jimbo Katoliki la Moshi ambaye aliteswa na ndoto ya kutafuta mwarobaini wa tatizo la yatima na jamii ya watu wenye ulemavu kukosa makazi ya kudumu, kutelekezwa na familia zao na wengine kufukuzwa na wazazi wao kutokana na kupata ulemavu.

"Sijakurupuka naijua Mawela, nimezaliwa hapa, ndio maana nimeguswa sana kuanzisha huduma hii kwa ajili ya kusaidia yatima na wenzetu wenye ulemavu ambao nakumbuka wako Rau na wengine Mawela," alieleza Padri Ngao katika taarifa yake.

# ama

ALHAMISI OKTOBA 24, 2019

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 18

## Ujuzi Muhimbili na wema uliotukuka kuwatenganisha pacha walioungana



Ukurasa 14

## Wanaozaliwa miezi mitano wanaishi



## Aliyepata watoto 5 kupitia mkunga jadi afunguka kilichompeleka huko

Ukurasa 16



# Simulizi wavuvi walivyonusurika 'kasheshe' siku 4 baharini Pemba

Ukurasa 14

# Wanaozaliwa miezi mitano wanaishi

**Na Mwandishi Wetu**

MIONGOZO ya kiafya kwa muda mrefu imekuwa ikitafsiri mtoto anayezaliwa katika umri chini ya wiki 23, kupona kwao ni majaliwa.

Wataalamu wamekuja na hoja ya kitabibu kwamba, mtoto anaweza kuzaliwa katika umri hadi wiki 22 (miezi mitano na siku nne) na akapona, ingawaje hatakiwi, maana moja ya kasoro za mtoto katika umri huo, mapafu yake yanakuwa hayajajengeka vizuri.

Kanuni ya kawaida kiafya mtoto anazaliwa katika umri wa wiki 40 (miezi) tisa au ikipungua ni wiki 38 (miezi minane na nusu), hapo anakuwa katika mazingira ya afya njema.

Lakini, mara nyingi binadamu anayezaliwa katika umri huo wa wiki, kunakuwapo sababu za ziada zinazoangukia katika mtazamo wa matatizo na uhai wao kudumu unakuwa ni mtihani.

Profesa Dominic Wilkinson, mtaalamu bingwa wa afya, anasema, juhudi za kitabibu na usimamizi wa afya, zimeibua ushahidi wa uhai kwa wanaozaliwa wakiwa na umri wa wiki 22 wanapona, ingawaje ni mtihani kunusuru maisha hayo.

Hata hivyo anaongeza: "Ni hatari kubwa kwamba kila mara si sahihi kuwa na ufuatiliaji wa karibu kitabibu."



Mtoto mchanga. **PICHA: MTANDAO**

MAZINGIRA

# Simulizi wavuvi walivyonusurika 'kasheshe' siku 4 baharini Pemba

## • Wimbi liliwapindua...ikawa kufa, kupona • Meli 'yapotezea'; waokoaji wavuvi Kenya



Wavuvi katika msukosuko wa kuzama Pemba. **PICHA: MTANDAO**

**Na Suleiman Rashid Omar,** PEMBA

UVUVI ni shughuli inayoleta ajira kwa vijana, wazee na inawakimu kinamama wengi wanaofanya biashara ya kukaanga samaki katika maeneo mbalimbali mijini na vijijini.

Pia ina umuhimu wake katika kusaidia chakula, kwani kuna baadhi ya jamii kiuchumi, pasipokuwapo samaki, maisha hayaendi.

Hiyo inajidhihirisha katika minada ya samaki, kunapokuwapo mkusanyiko unaowasubiri wavuvi kuwaletea bidhaa za baharini. Lakini, upande wa pili wa simulizi hiyo inakuwa ni kazi inayowaweka roho mkononi hata katika hatari za kudhurika baharini.

Tafakari ya uzuri na ubaya wa kazi ya uvuvi, sasa iko katika familia kadhaa za hapa kisiwani Pemba, zinapogugumia machungu na majeraha ya kupoteza ndugu zao baharini waliokuwa wakivua.

> "Mimi nilijifunga mpira wa mashine ya boti kiunoni ukanikaa kisawasawa. Nikajua hapa sitoki.

### KILICHOTOKEA

Nipashe ilifika eneo la Shumba Mjini Wilaya ya Micheweni, ambako wavuvi wanane walizama baharini, kati yao watatu walifariki, walipokuwa katika nyendo za uvuvi wa samaki.

Mmoja wa manusura, Rashid Othman, anasimulia mkasa wa siku nne alizoishi baharini katika sura 'nusu duniani' na 'nusu bahari' akirejea ni changamoto walizo nazo wavuvi wote wa samaki.

"Ni takriban siku nne tumekaa baharini bila ya kula, kusinzia, siwezi kulala, tukiwa nusu mwili umo ndani ya maji bahari, mawimbi upepo na baridi ikawa ni sehemu ya maisha yetu kwa siku hizo, ingawa njaa tulizihisi ila ilikuwa vigumu kupata chakula," anatamka na anaendeleza simulizi:

"Maji yalituteka. Baada ya wimbi kubwa, lilirusha chombo chetu tukiwa baharini na kutupeleka yatakapo mkondoni, maana nguvu zilituishia tukawa hatuna ujanja.

"Maji yakatupeleka tusikokujua, huku mawimbi kila dakika hayakutuhurumia, yalitulewesha kila muda tukawa kama jiwe au kitu kisicho na uhai baharini, tukidonolewa na samaki wadogo miguuni bila kuhisi utadhani miguu sio yetu."

Ni simulizi za mvuvi Rashid aliyepotea baharini kwa siku nne akiwa na wenzake wanne, waliofariki baada ya boti lao kupigwa na dhoruba ya wimbi kubwa, lililoipindua na kuizamisha.

Rashid anayejitambuisha kuwa mvuvi aliyeiva katika taaluma hiyo ya uzoefu wa muda mrefu, akisema binafsi hakuptia shule na muda wake wote katika kujifunza tangu umri mdogo alijikita kwenye uvuvi kwa kutumia mishipi mtoni na kadri umri ulivyoongezeka, alisogea baharini na hata alipofikia umri wa miaka 20, alijitosa baharini kwa kutumia ngalawa.

"Mimi katika maisha yangu haya ya uvuvi ambayo ndio sehemu ya maisha yangu kazi inayonipa riziki ya kupata mke, ninahudumia watoto sita na nyumba na kila kitu changu kinatokana na uvuvi. Tayari nimeshazama baharini mara tano ambazo zote nimeokolewa," anaeleza.

### MIKASA YAKE

Rashid anafafanua kwamba, katika matukio hayo yote, mikasa yake ilikuwa mizito, lakini mara zote hakuwahi kuzama na kulala baharini waliokolewa mapema, isipokuwa la karibuni imekuwa ya kihistoria na aina yake, kwani walikwama siku nne baharini.

Anasema, mara ya kwanza alizama akiwa umbali wa mita 80 kutoka bandarini, lakini haikuchukua muda wa saa mbili tu alikaa baharini wakaja wavuvi wenzao waliowaokoa

Rashid anaendelea kwamba, ni tukio lililomtia hofu lakini baadaye ndipo alipopata ujasiri wa kuendelea na kazi yake hiyo ya uvuvi.

Akiwa amesheheni simulizi uya mikasa yake, asema, baada ya mwaka mmoja ilimtokea mkasa wa pili ambao alipinduka kwenye mkondo wa maji ya bahari, lakini aliokolewa haraka ma wavuvi wenzake.

Mara ya tatu, Rashid anasimulia alipokuwa kazini akivua katika mwambao anaoutaja wa Songosongo (Kilwa) majira ya saa 12.00 asubuhi, chombo chao cha uvuvi kilizama na kilibaki kwenye maji hadi saa 12 jioni wakiwa katika msukosuko wa maji mengi, ndipo walitokea wavuvi wenzao waliowaokoa.

"Mara ya nne tulikuwa na ngalawa mkondoni nikazama, ngalawa ikakokotwa na maji tukaogelea mpaka majira ya saa 12 tukafika bandarini Tumbe," anasema Rashid.

"Mara hii ya tano tuliokoka Kenya. Katika maisha yangu sitaisahau, kwani nikiulizwa tamu na machungu ya uvuvi yote na

MAZINGIRA

# Simulizi wavuvi walivyonusurika 'kasheshe' siku 4 baharini Pemba

nayasamehe, ila hii ukiniuliza basi, hata moyo wangu huhaghabika kwani tulikuwa katika shida kubwa," anaeleza.

**MKASA MZITO**

Ilikuwaje? Anaanza kusimulia kwa kwamba waliondoka bandarini Pemba majira ya saa tisa usiku, ikiwa ni safari ya kwenda kuvua kwa kutafuta chambo na mnamo majira ya saa 10 siku, walielekea baharini kwa ajili ya kuvua.

Rashid anasimulia kwamba, walipokuwa baharini, ghafla nahodha wao aliwaamuru kuvuta nanga, iliwa ondoke sehemu waliokuwapo. Anasema ilikuwa umbali wa wastani wa maili 200 kutoka bandarini.

Anaendelea kusimulia kwamba, ghafla waliona wimbi kubwa mithili ya nyumba linakuja bila na likapiga boti lao na wakazamishwa katika maji ya bahari.

"Tukiwa tunatapatapa hatujui pa kuazia, mara niliona boti letu imeibuliwa na wimbi kwa mbali. Nikawaambia wenzangu 'tushapona, boti yetu ile tuifuate.' Tukaifata, tulipofika ilikuwa inaelea 'kimgongo mgongo.' Tukajitahidi 'kuibirukisha' (kuibinua) na kufanikiwa, lakini ikawa imejaa maji yote nzima," anasema.

Anaeleza kuwa, baada ya chombo chao kupigwa na wimbi na kuzama, nanga haikuonekana na wakawa wanahangaika baharini huku mawimbi yakiwapiga kuwazamisha na kuibuka kwa muda uliyochukua wastani wa saa mbili.

Ni msukosuko anasema walishtukia kwamba, wamebaki watatu, mwenzao mmoja akawa ametoweka na kwa mbali anasema alimuona, akiendeleza simulizi: "Nikamwita, alianza kupoteza nguvu. Nikaenda kumchukua hadi kilipo chombo nikamkamatisha, ila alishindwa ghafla likapiga wimbi tukapoteana."

Anasema, baada ya kuzama chombo hicho cha uvuvi kikaanza kuja juu na alipojitahidi kumtafuta alishindwa, wakati huo walikuwa wamekwishaingia kwenye boti lililojaa maji, ikiwa inapelekwa na mkondo wa maji, hawana nanga wala kasia mashine ziligoma kuwaka. Huku hisia zikiwaweka katika nafasi mwenzao tayari alishawatoka, pia ikawa mwanzo wa maisha ya siku nne baharini, wakikosa mweleko, hawali wala kunywa chochote.

Anasema, walichofanya ni kukata vipande vya mishipi waliotumia kuvua, huku wakiwa katika hasara kubwa ya kupoteza vitu lukuki, katika thamani ya haraka anaikadiria Sh. milioni tatu.

Rashid anasema, wakati wote wa msukosuko wao, boti lao lilielea huku limejaa maji yaliyowafikia tumboni na walishindwa kuyatoa, huku akisisitiza mara zote walinusuru kichwa tu.



Picha za wavuvi wa Pemba, wakiwa kazini.



Sehemu ya Bandari ya Wete, Pemba. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> **Kuna wenzao wanne ambao katika msukosuko wa hali ya siku hiyo, hawajaonekana na imani iliyopo ni kwamba walishapoteza maisha.**

"Sisi tuliamua kujifunga ndani vya boti hivyo hivyo tikitaraji tukifa boti ikifika juu namaiti zetu zionekane ndani ya boti hivyo kila moja alijifunga kamba madhubuti ikawa wimbi linapiga kurusha na kutua ila hatutoki ndani ya boti," anasema.

"Mimi nilijifunga mpira wa mashine ya boti kiunoni ukanikaa kisawasawa. Nikajua hapa sitoki," anasema Rashid.

**DALILI KUOKOLEWA**

Rashid anaendelea pasipo kujua wanakoelekea, siku ya tatu waliona meli kubwa zikiwapitia karibu, lakini hayakushughulika.

Anasema, siku ya nne ndipo, walifanikiwa kupeperusha vitambaa na wakaja wavuvi wa Kenya waliwaokoa.

Mvuvi Kombo Ali, anasimulia siku ya mkasa, kwamba tangu mwanzo kulikuwapo na upepo mkali baharini na kazi yao kwa jumla ilikuwa ngumu.

"Ila kwa kuwa ni kazi yetu tulioizoea wenyewe, mvua, jua ilitubidi tuendelee ila hali ilikuwa inatisha," anakumbuka siku ya mkasa.

Kombo anasimulia kwamba walipofika umbali mita 250 kutoka bandarini walitia nanga na siku hiyo upepo na mawimbi yalikuwa makubwa kuliko ilivyozoeleka na kilichowakuta kwenye mkasa huo, hawakuwa na imani ya kuokolewa.

Kombo anarejea uzoefu wake wa uvuvi, kwamba alishawahi kuzama mara tatu baharini, lakini aliokolewa, jambo lililompa imani ya kuendelea na kazi ya uvuvi inayomwezesha kugharamia maisha yake na familia ya mke wake na watoto sita walioko.

Anasema, kuna wenzao wanne ambao katika msukosuko wa hali ya siku hiyo, hawajaonekana na imani iliyopo ni kwamba walishapoteza maisha.

Kombo anasema, licha ya wao kinusurika ni kwamba wameumia sana na hata hali zao kiuchumi majumbani si za kuridhisha, huku akaenda mbali; kuielekeza jamii kutafakari mara mbili, familia za kujiunga na fani hiyo ya uvuvi, katika mazingira duni.

AFYA

# Aliyepata watoto 5 kupitia mkunga jadi afunguka kilichompeleka huko

• Darasa shule limejaa 'zao' la mkunga • Kote anakopita ni kelele...'Mama Ibra'

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

***ALHAMISI iliyopita ilikuwa sehemu ya kwanza ya makala hii katika jarida la AMA, ikibeba historia na stadi za Mkunga Ziada Ngwere maarufu Mama Ibra wa Ilemela Mwanza, alikohudumia kinamama zaidi ya 1,900 katika ukunga wa jadi na wengine zaidi ya 700 katika miaka nane katika kituo cha afya alikoajiriwa, baada ya kuonyesha makuu mtaani, ambako hajastaafu. Ameweka alama iliyosababisha aajiriwe bila kuomba kazi. Fuatilia mwendelezo wa simulizi:***



Wanafunzi wa shule ya msingi iliyoko Ilemela, zao la kazi ya mkunga Ziada Ngwere. **PICHA ZOTE: ANTHONY GERVAS.**

INAPOZUNGUZIWA Kata ya Shibula wilayani Ilemela, Mkoa wa Mwanza, mazingira ya fursa zake kijiografia ni Kaskazini imezungukwa na Ziwa Viktoria, hivyo moja ya shughuli zake kiuchumi jirani ni uvuaji samaki na kilimo kwa kiasi kidogo sana.

Hata hivyo, suala la ubovu wa miundombinu yake, huduma duni za afya, ukosefu wa usafiri na maisha duni kwa wanajamii, ni mambo yanayotajwa kuwa vikwazo vinavyowakatisha tamaa wajawazito kwenda kujifungua katika vituo vya afya.

Inaelezwa kwamba, ingawa kinamama wengi wanapenda kujifungulia katika vituo vya afya na kupata huduma nzuri, lakini changamoto walizokabiliana nazo wanaitaja mojawapo ni kukosekana usafiri, jambo linalowakwaza mno, wajawazito wengi wakatumia mbadala wa baiskeli.

Ni hali wanaiyoifafanua kwamba imewakatisha tamaa kufuata huduma hizo za kiserikali na wanawake wengi wamevikana vituo vya afya na kuajitosa katika mbadala, ambao ni wakunga wa jadi.

**MAMA WATOTO 5**

Akizungumza na Nipashe, Pili Ibrahimu (42), mama mwenye watoto watano, anasema kutokana na changamoto hizo, aliamua kujifungua watoto wote watano nyumbani, kwa kuwatumia wakunga wa jadi.

Pili, mkazi wa Mtaa wa Semba A katika Kata ya Shibula, wilayani Ilemela, anasema ni matukio mfululizo katika miaka 16 kuanzia mwaka 1997 hadi 2013. Anafafanua: "Wakati huo barabara ilikuwa mbovu, hapakuwapo na usafiri wa daladala, hapakuwa na umeme, huduma za afya zilikuwa duni.

"Kulikuwa na zahanati ambayo haikuwa na uwezo wa kutoa huduma hiyo. Hivyo, tulilazimika kusafiri umbali wa kilomita tano kwenda katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mwanza -Sekou Toure," anasema.

Anataja changamoto nyingine iliyomkatisha tamaa asijifungulie hospitalini, ni suala la ukosefu wa usafiri kwenda kupata huduma ya kujifungua.

> **Napenda kusoma hadi chuo kikuu ili baadaye niwe Padri, nipenda somo la Uraia- Maadili, Maarifa ya Jamii na Kiingereza, ndiyo rahisi kwangu kuliko Hisabati, Sayansi na Kiswahili.**

Pili, anaeleza tathmini ya maisha yake awali yalikuwa duni, lakini anamsifu mkunga wa jadi kwamba alimwezesha kupata huduma nzuri ya uzazi, akimtaja mhusika kwa jina la Ziada Ngwere au Mama Ibra, ambalo ndilo maarufu katika mitaa yao ya Ilemela.

Mama huyo anasimulia wasifu wa mkunga Ziada, akidai 'huduma zake ni za kipekee' zinazomkweza zaidi, hadi serikali ilipomtambua na kumwajiri, wakati huohuo katika huduma za mtaani hajang'oa mguu.

Pili anasema, alijifungua mtoto wa kwanza kwa mkunga na akaendeleza hadi wa tano, mhusika akiwa mkunga huyo huyo; Mama Ibra, pasipo kukanyaga ama kituo cha afya au hospitali.

Anamtaja wa kwanza ni mwanaume mwenye umri wa miaka 22 sasa, anayesoma katika chuo kiichopo jijini Dar-es Salaam na mwingine, msichana mwenye umri wa miaka 16, anayemaliza kidato cha nne mwaka huu, katika shule ya sekondari iliyoko wilayani Ilemela.

Anawataja wengine mbali na msichana wa mwisho kuzaliwa mwenye umri wa miaka sita na hajaanza darasa la kwanza, ni wavulana wawili walioko jijini Mwanza; mwenye miaka 14 aliyemaliza darasa la saba mwaka huu, na anayesoma darasa la tano.



Mkunga Ziada Ngwere (kushoto), akiwa na Pili Ibrahim, mama wa watoto watano, wote, wamehudumiwa na mtaalamu huyo wa afya. Katikati ni mtoto mmojawapo, Raham Sharifu.

Mkazi huyo wa Ilemela, anasimulia makuu aliyofanyiwa na kushuhudia kutoka kwa mikunga huyo akitamka "sina uwezo wa kuyasimulia."Anamsifu kuokoa maisha ya wanawake wenzake wengi mtaani kwake kata ya Shibula 'wasiohesabika' pindi walipojifungulia nyumbani.

"Kwa jinsi alivyoweza kusaidia kuokoa maisha ya kinamama wajawazito kujifungulia nyumbani, tungeweza tungemwita Muumba. Makubwa aliyoyafanya, hayana mfano kwenye jamii inayomzunguka mtaani," anaeleza Pili.

Kwa mujibu wa Pili, mkunga Ziada amekuwa akitoa huduma bora inayompaisha umaarufu katika kila kona mtaani, kwa jamii ya rika zote.

**WANAFUNZI 'WAKE'**

Kama ilivyo umaarufu wake mitaani, mkunga Ziada anapokanyanga ndani ya uzio wa shule za msingi zilizomo ndani ya Kata ya Shibula zinasikika kelele mbalimbali za 'kiuanafunzi' kushangilia kwa staili tofauti.

Nipashe ilipokuwa hapo, ilishuhudia jina 'Mama Ibra' ambalo ndilo limezoeleka zaidi kutoka kwa wanafunzi hao, mwenyewe akirejea kwa asilimia kubwa ni zao lake la taaluma ya ukunga wa jadi.

Hapo, mwandishi wa makala akakutana na ushuhuda kutoka kwa wanafunzi wanne waliozaliwa kupitia huduma ya mkunga nyumbani, sasa watoto hao ni wanasoma katika Shule ya Msingi Mhomnze, katika Kata ya Shibula wilayani Ilemela.

Nao kila mmoja anafunguka kuhusu ndoto zao za baadaye za kuendelea na masomo, huku hawachoki kumshukuru mkunga huyo, kutokana na kazi ya kuokoa maisha ya wazazi wao.

Ibrahim Sharifu, ni mwanafunzi wa darasa la tano katika Shule Msingi Mhonze, akiwa miongoni mwa waliozaliwa kupitia huduma za mkunga, anaeleza ndoto yake kufikia ngazi ya chuo kikuu, akiwa mtaalamu mhandisi wa magari, meli na ndege.

Ibrahimu anaeleza utashi wake wa baadaye ni kusaidia watu katika sura ya fadhila, kama alivyofanya kuhudumia kuzaliwa kwake

Mwanafunzi Emmanuel Ibrahim, anayesoma darasa la tatu katika shule hiyo, anasema ndoto zake katika ngazi ya elimu ni kufikia ngazi ya mtangulizi wake. Anaendelea:

"Napenda kusoma hadi chuo kikuu ili baadaye niwe Padri, nipenda somo la Uraia- Maadili, Maarifa ya Jamii na Kiingereza, ndiyo rahisi kwangu kuliko Hisabati, Sayansi na Kiswahili," ananeleza Emmanuel.

Elisalia Mkodemo, ni mwingine anayesoma darasa la nne katika shule hiyo, anaeleza matarajio ya ndoto zake kuwa anapenda kusoma zaidi, ili baadaye awe rubani wa ndege, ingawa anakiri somo la Maarifa ya Jamii, lilikuwa linamsumbua.

Ndoto ya Janeth Thomson wa darasa la sita, ananuia katika maisha ya baadaye kusoma awe muuguzi, awasaidie kinamama na wagonjwa kama anavyosaidia mkunga Ziada. Kwa lugha nyigine amnafuata nyayo za Mama Ibra.

> **Kwa jinsi alivyoweza kusaidia kuokoa maisha ya kinamama wajawazito kujifungulia nyumbani, tungeweza tungemwita Muumba.**

Kwa ujumla, kazi ya ukunga imemkweza sana Ziada ajulikane kote katika mitaa ya wilaya yake ya Ilemela na Kituo cha Afya Karume anakotumikia, huku binafsi anakiri kazi hiyo anaifanya kwa 'moyo mweupe' wakati wote anapotumikia, kwani ameipenda tangu zama za muda mrefu.

Ama kweli ni historia ndefu, yenye mnyororo wa urithi aliyohusudu akiwa na umri wa miaka sita kutoka kwa bibi yake aliyekuwa mkunga kabla ya kifo chake mwaka 1978. Ziada alianza kujifunza akiwa na miaka sita, zama hizo mwaka 1975.

## Maisha ya mwanamama mwenye ndevu tele





Harnam Kore katika picha tofauti. **PICHA : MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

HARNAM Kore (28) ameishi maisha yake yote tangu akiwa msichana mdogo ana ndevu mithili ya mwanaume. Hiyo ni tangu alipokuwa na umri wa miaka 16 pekee. Ilimkera na kumnyima raha sana.

Kwa sasa, ni mama mkubwa na mwanaharakati, akiwa mzungumzaji fasaha katika kampeni kadhaa zinazolenga kuwasaidia watu kukubali maumbile yao na kujiponya dhidi ya uonevu na unyanyasaji.

Harnam anajivunia uso wake uliojaa ndevu, akijifunza kujivunia tofauti yake kwa njia anayoamini inampendeza yeye na jamii, akiangazia uzoefu wake, mafanikio na kwanini anastahili akiwa namna alivyo.

Anajitambulisha kuwa maisha yake ya usichana kwamba amekua na ndevu. Anasimuli kwa matamshi: "Nikiwa na umri wa miaka 12, nilipatwa na hali inayojulikana kama 'Polycystic Overy Syndrome'ambayo husababishwa na ukosefu wa usawa wa homoni mwilini, hatua ilionifanya ndevu kuota."

Mwanamke huyo anasema, hata hivyo hakuruhusu ndevu zionekane, kutokana na manyanyaso yaliyomkuta kwa miaka kadhaa kutoka kwa watu asiowajua barabarani na hata wanafunzi wenzake shuleni.

"Nilikabiliwa na changamoto wakati nilipokuwa kijana kuhusu kujiamini kwangu na mwili wangu, kutokana na umbo langu lisilo la kawaida. Sijawahi kuona mtu anayefanana nami katika runinga," anasema.

Anasema, alianza kujihisi kasoro za kimwili pale anapojiona ni msichana mdogo, lakini ana ndevu na kile alichotaka. Mara zote alipigana aonekana ni mtu wa kawaida sana.

Harnam anasema, baada ya kutetereka sana kisaikolojia, aliamua kujikaza na akagundua kwamba jamii inahitaji kubadili tabia kuhusu dhana ya urembo, nafasi ya mwanaume na mwanamke au mtu yeyote.

Anaendelea: "Niligundua kwa haraka kwamba nguvu zangu zinatokana na kujiamini...jamii hii inahitaji mtu mwaminifu aliye mkweli ili kuendelea. Hivyo basi, niliamua kuachia ndevu zangu na kupambana na dunia jinsi ilivyo."

Anasema, hiyo ndio ikawa ngumu zaidi katika maisha yake na anaongeza: "Kila siku, nilijiambia inaua kichwa chako, tabasamu na uwe mtu mzuri."

Mwanamke huyo anasimulia kwamba, mwili wake ulimsaidia kuishi na kuwasaidia kinamama wengine wenye shida za kijinsia.

**SIRI KUJIPENDA**

Inaelezwa na wataalamu wa saikolojia kwamba, kwa kawaida msingi ni kujipatia shinikizo kali ya kuafiki kiwango ambacho wanajipenda, japokuwa mtu anachohitaji kufanya ni kuwa mkarimu na kwa wengine, kujiamini na mwili anaoupenda na kisha aufurahie .

Kanuni nyingine ni kuwaondoa wale waliopo katika orodha ya marafiki katika mitandao ya kijamii, wanaodhani kwamba haifai kuishi maisha anayoishi na wale ambao katika maisha ya kawaida, wanahisi anahitaji kubadilika na sio kubaki alivyo.

Pia, inaelezwa kwamba mtu akipata uzoefu kutoka katika kile unachosoma, ni vyema akazungumza na mwingine anayemwamini kuhusu matatizo utakayokabiliana naye, yawe makubwa au madogo.

Hata hivyo, vilevile inajukulikana ugumu wa kuzungumzia kuhusu maumbile ama masuala ya afya kama ya kiakili.

Sambamba na hilo, kuna nafasi ya kuzungumza na daktari au mtaalamu wa afya, hali inayoweza kuwaunganisha watu unaowahitaji kusaidia kubadili maisha binafsi.

AFYA

## KISICHOWEZEKANA, KIMEWEZEKANA...

# Ujuzi Muhimbili na wema uliotukuka kuwatenganisha pacha walioungana

- Bingwa Dk. Ngiloi adadavua walichokifanya
- Mama alihisi laana, madaktari wakamjibu

**Na Mary Geofrey**

WATOTO wanakuja na riziki yao. Ndivyo ninavyoweza kusema kwa watoto mapacha waliozaliwa wilayani Kisarawe, Mkoa wa Pwani wakiwa wameungana maini na tumbo.

Mama yao mzazi, Ester Simon (23), anasema alijihisi mwenye mkosi baada ya kuambiwa watoto aliyojifungia wameungana kuanzia kwenye maini hadi tumboni.

Lakini, hali hiyo ilibadilika na kuwa baraka kwa mwenye familia hadi ukoo mzima, baada ya jukumu hilo la kitabibu kufikishwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), ikiendana na sadaka za kijamii kwake na zimebeba picha ya kitaifa.

Ester anasema alijifungua mnamo Julai 12 mwaka jana; watoto wawili wa kiume (Gracious na Precious) walioungana eneo la maini hadi tumboni. Nyumbani kwao ni umbali wa kilomita 40 kutoka mjini Kisarawe.

Anasema, akiwa nyumbani alijihisi uchungu na uzazi wakati akijiandaa kwenda hospitali. Hakuweza kuwahi huko, alijifungulia nyumbani na mama mkwe wake ndiye aliyebeba jukumu la ukunga.

Mwanamke huyo anasema, baada ya mama mkwe wake kumzalisha watoto hao pacha, waligundua wameungana, hivyo walilazimika kuwahi hospitali kwa ajili ya kupata msaada wa wataalamu.

"Mama mkwe alinichukua na tukawahi zahanati ya jirani na walitupa huduma ya kwanza na kutusihi tuwahi Hospitali ya Kibaha, mkoani Pwani, kwa sababu wasingeweza kutusaidia," anasema.

Kwa mujibu wa Ester, baada ya kukimbia na kuwahi hospitalini Kibaha, huko nako baada ya ukaguzi wa kitaalamu mara moja waliwaelekeza waende hospitalini kubwa zaidi Muhimbili.

Kama ilivyokuwa Kibaha, huko mara moja walionana na daktari na kuanza kufanyiwa vipimo na Ester anafafanua: "Madaktari walisema wataanza kuwatibu kwanza, kwa sababu walikuwa wamechoka, hivyo tulikaa Muhimbili mwezi mmoja tukiendelea na matibabu kabla ya upasuaji."

Anasema, baada ya hapo ndipo watoto walifanyiwa upasuaji wenye mafanikio kwa kutenganishwa salama na baada ya madaktari kujiridhisha na afya zao njema, watoto waliruhusiwa kurudi nyumbani.

### MAKAZI MAPYA

Pamoja na ruhusa hiyo, mama anasimulia kwamba uongozi wa hospitali hawakuridhishwa na makazi yao, akifafanua: "Tukiwa tayari kurudi nyumbani, madaktari walitembelea makazi yetu na kusema watoto hawa hawatakiwi kuishi pale, kwa sababu si salama kwa afya zao."

Anaeleza, baada ya hapo walianza kutafutaa wafadhili kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe na MNH na ikapatikana benki ya UBA (United Bank of Africa).

"Nawashukuru Muhimbili kwa kuokoa maisha yangu, pia kujali na kuona umuhimu wa kuwa na nyumba bora itakonifanya niishi kwa usalama zaidi na hawa watoto," Ester anasema.

Anasema, mazingira hayo yalimlazimike kuishi kwa ndugu yake, Kibaha mkoani Pwani, wakati wakisubiri kukamilika kwa utaratibu wa kujengewa nyumba.



Ni siku ya hafla ya watoto mapacha kukabidhiwa nyumba yao Kisarawe.

> **Walizaliwa wakiwa wameungana maeneo ya tumboni, lakini eneo waliloungana kwa ndani ni ini na sehemu kidogo ya mfupa wa kifua.**

### LILILOMSHITUA NYUMBANI

Ester anasema, tangu aliporuhusiwa kurudi nyumbani na watoto wake hakuwahi kupata tatizo, lakini siku moja mtoto wake mdogo ghafla aliugua ugonjwa uliomchanganya mno.

"Sitasahau siku hiyo. Mtoto wangu mmoja alianza kuvimba mwili wote na kupata homa kali ambazo hazikauki. Nilipata shaka sana na nilipompeleka zahanati, walinielekeza kwenda Muhimbili ambako walibaini amepungukiwa damu," anasema Ester.

Kwa mujibu wa Ester, huko mtoto alipatiwa matibabu na akarejea hali ya kawaida na hadi anazungumza hivi karibuni, hajashuhudia mabadiliko, mapacha hao wakiwa katika hatua ya kutembea na wakiwa na afya nzuri.

### MABINGWA KAZINI

Daktari Bingwa wa Upasuaji Watoto Hospitali ya Muhimbili, Patronila Ngiloi, anasema walifanya upasuaji huo Septemba 16 mwaka jana, kazi iliyojumishwa madaktari bingwa 10.

Anasimulia ni jopo linaloundwa na wataalamu sita mabingwa wa upasuaji watoto; wanne wa usingizi na wauguzi wanne.

"Walizaliwa wakiwa wameungana maeneo ya tumboni, lakini eneo waliloungana kwa ndani ni ini na sehemu kidogo ya mfupa wa kifua," anasema Dk. Ngiloi.

Anaongeza: "Tuliwapokea mama na watoto wakiwa wamechoka sana na watoto walionekana kuwa na tatizo kwenye kitovu, kutokana na namna ukataji ulivyofanyika. Hivyo tulianza kuwapa tiba haraka."

Daktari huyo anasimulia kwamba baada ya watoto kukaa sawa kiafya, ndipo walipoanza kuwahudumia kwa alichokitaja kwa jina 'tiba lishe' kwa ajili ya mama wa watoto, ili kuwasaidia kupata maziwa mengi ya kutumiwa na watoto.

"Watoto walifika Muhimbili wakiwa na kilogramu mbili kila mmoja, lakini tulivyoanza kumpa mama uji wa lishe na vyakula vya kuongeza maziwa, waliongezeka na kufikia kilogramu nne kwa mmoja na mwingine kilogramu tano," anaeleza.

Anatoa ufafanuzi wa kazi hiyo, kwamba inalenga hitaji la mtoto kufanyiwa upasuaji anapaswa kuwa na uzito walau kilogramu nne na nusu, hivyo mapacha hao baada ya lishe walifikia hapo, ndipo walipoingizwa katika maandalizi ya kufanyiwa upasuaji.

Hatua ya kwanza, anaeleza ilichukua vipimo ya X-ray, CT-Scan na MRI kufahamu namna walivyoungana na wajue aina ya wataalamu wanaotakiwa kuwafanya upasuaji.

"Tulivyowafanyia uchunguzi, tulibaini wameungana kwenye eneo la ini na mfupa kidogo kwenye kifua. Hivyo, tuliwasiliana na Mkurugenzi wa Hospitali (MNH) kwa ajili ya kuanza taratibu za upasuaji," anasema.

Dk. Ngiloi anaeleza kwamba waliamua kufanya upasuaji huo kwa sababu kulikuwapo na daktari bingwa wa upasuaji wa ini kwa watoto ambaye hufika nchini kujitolea, akitokea nchini Ireland.

Anasema, upasuaji huo ulifanyika kwa mafanikio na baadaye watoto waliwekwa katika chumba cha uangalizi maalum (ICU) kwa siku mbili, ndipo wakarudishwa wodini.

### UPASUAJI ULIVYO

Dk. Ngiloi anasema, si kila watoto walioungana wanaweza kufanyiwa upasuaji wa kutengenishwa, kwa sababu wengine wanaungana maeneo ambayo ni magumu kutenganisha na viumbe hao wakabaki salama.

Anataja hatari zilizopo ni pamoja na kupoteza maisha ya mmoja wa




Watoto mapacha wakiwa nje ya nyumba waliyopewa. **PICHA ZOTE: NA MARY GEOFREY**

viumbe walioungana na ili kujihami na athari za namna hiyo, kuna mikasa ambayo kunalazimika kuundwa na jopo la madaktari hata 50, kulingana na maeneo walioungana.

"Kila kiungo walichoungana watoto kunatakiwa kuwa na madaktari wake bingwa, mfano ini, mfupa, mkojo, mishipa ya fahamu, moyo na kifua na maeneo yote yanayoguswa na upasuaji," Dk. Ngiloi anasema.

Akizungumza sababu za watoto kuzaliwa wameungana, Dk. Ngiloi anadokeza mojawapo ni hitilafu wakati wa uundaji wa mbegu za baba na mama, katika wiki nane za mwanzo kutungwa mimba.

**KWA NINI WALISAIDIWA?**

Dk. Ngiloi anasema, watoto hao waliofanyiwa upasuaji mkubwa wanahitaji kuishi mazingira salama, ndio jambo lilochangia hoja ya kutafutiwa msaada wa malazi waendelee kulinda maisha yao yakiwa salama, huku akisisitiza nyumba waliyoishi haikuwa salama.

"Kupitia waandishi wa habari na Meneja Mawasiliano wa MNH, tulianza kutafuta watu wa kuwasaidia. Benki ya UBA ilijitokeza kuwajengea nyumba ya kuishi," Dk. Ngiloi anasema.

**USHUHUDA WA MWAKA**

Mkurugenzi Mtendaji wa MHN, Profesa Lawrence Museru, anasema baada ya kufanyika upasuaji huo kwa mafanikio, hospitali imeshajenga vyumba viwili vya upasuaji watoto, kukabili hali kama hiyo.

Kwa mujibu wa Profesa Museru, kukamilika vyumba hivyo kunawezesha kufanyika upasuaji wa aina hizo mara 10 kwa wiki, tofauti na awali waliofanya mara nne

**"Kila kiungo walichoungana watoto kunatakiwa kuwa na madaktari wake bingwa, mfano ini, mfupa, mkojo, mishipa ya fahamu, moyo na kifua na maeneo yote yanayoguswa na upasuaji.**



Mapacha kabla ya kutenganishwa. Picha nyingine, baada ya kutenganishwa.



ndani ya kipindi hicho.

"Hatua hii ni utekelezaji wa agizo la Rais Dk. John Magufuli, aliyetutaka kutoa huduma ambazo hazitolewi nchini katika kuboresha hospitali yetu na leo tunafuraha kuwaeleza kuwa tumefanikiwa kufanya upasuaji mkubwa wenye mafanikio," anasema Profesa Museru.

Mwaka mmoja baada ya upasuaji, madaktari bingwa wa MNH walipanga kuwatembelea watoto hao kutathmini afya zao, huku bingwa wa watoto wa MNH aliyeshiriki kazi hiyo ya upasuaji, Dk. Zaituni Bokhari, anasema baada ya mwaka mmoja wamewakuta na afya njema.

Anafafanu kwamba, waliwafanyia upasuaji wa kuwatenganisha maini na kuwatengeneza kitovu na kwamba hali zao zinaendelea vizuri.

"Tuna furaha kubwa kabisa kuona hali za watoto hawa zinaendelea vizuri. Wamepona vizuri, ngozi imeunga vizuri na wanaenda haja bila shida yoyote," anasema Dk. Zaituni.

**WAKABIDHIWA NYUMBA**

Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo, katika hakfa ya kukabidhi nyumba yao Septemba 24 mwaka huu, anasema ilijengwa na UBA kwa gharama ya Sh. milioni 18 na ilishakabidhiwa kwa wazazi wa watoto.

Jokate anasema, ni ujenzi uliokamilika ndani ya siku 28, baada ya maandalizi ya muda mrefu kutafuta eneo lililo karibu na huduma za kijamii, kama vile shule na kituo cha afya.

Anasema, eneo lililonunuliwa na Balozi wa Visiwa vya Shelisheli Maryvonne Pool na Benki ya UBA, waligharamia ujenzi wa nyumba hiyo na kuweka umeme.

" MNH kwa kushirikiana na ofisi yangu, tulijitahidi kuhakikisha mama huyu anapata huduma za malazi salama kwa ajili ya kuangalia afya za watoto hawa," anasema Jokate.

Pia Jokate alimwelekeza Ofisa Tarafa wa Mzenga wilayani Kisarawe, waliko watoto hao ahakikishe hati ya nyumba inapatikana na kuwekwa majina ya watoto hao, ili kuepuka migogoro ya kifamilia.

**WAFADHILI**

Mkurugenzi Mkuu wa UBA, Usman Isiaka, anatoa siri ya kusukumwa kufadhili kwamba, ofisi yake ilivutiwa na huduma zilizotolewa na Hospitali Muhimbili kuwatenganisha na kubeba gharama yote ya matibabu hayo, Sh. milioni 34 hivyo wakaona ni muhimu nao wakawasaidia mchango wa makazi.

Anasema, pia wamewakatia bima ya matibabu ya miaka 10 na kuwafungulia akaunti kuweka akiba ya Sh. milioni mbili.

"Tumefurahi kuona nyumba hii imejengwa eneo zuri karibu na huduma za jamii kama shule na kituo cha afya.UBA pia tunaendelea kuwasaidia watoto hawa kwa kuwapa bima ya matibabu ya miaka 10 kuanzia mwaka jana (mwezi uliopita nyumba ilipokabidhiwa)," Isiaka anasema.

Balozi wa Visiwa vya Shelisheli nchini, Maryvonne Pool, aliahidi kuwajengea uzio na kuwapa kitanda na godoro la kulalia watoto hao.

AFYA

MFAMASIA WA SERIKALI:

# Umezaji dawa holela unaleta usugu wa tiba kwa mgonjwa

• Dk. Ndugulile aainisha kanuni ugawaji dawa

**Na Yasmine Protace**

HIVI sasa kuna ushauri unaotolewa na wataalamu wa zahanati, vituo vya afya na hospitali kuhusu umezaji dawa unaotakiwa kuzingatiwa, ili kuepuka kupata matatizo ya kiafya.

Kama mtu hatofuata ushauri wa kitaalamu na kuamua kumeza dawa kiholela, anajiandaa kuathirika kiafya.

Daudi Msasi ni Mfamasia na Mkurugenzi wa Huduma za Dawa, kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, anayeshauri jamii kuzingatia maelezo yanayotolewa na wataalamu, ili kuepuka athari za changamoto za kiafya, ikiwamo usugu wake.

Msasi akizungumza katika mkutano uliowashirikisha wadau wa afya wa ndani na nje ya nchi, kwamba lengo kuu ni kujadili mnyororo wa ugavi na kuibua hoja, pia kuchangia uzoefu na kutafuta majibu sahihi ya matatizo yaliyopo.

"Malengo ya mnyororo wa ugavi ni kuhakikisha wananchi wanapata dawa kwa wakati," anasema Msasi, huku akisisitizia mkazo uko katika kuanzisha vyanzo vya fedha kusaidia upatikanaji dawa.

Anasema, ili kufanikiwa lazima takwimu ziwe sahihi wanachukua hatua ya kuwafundisha watu masuala ya takwimu, ili wajua jinsi ya upatikanaji dawa na mahali zinakoenda.

Msasi anaongeza kwamba mfumo wa dawa utapelekwa mara sita na kila mwezi watakuwa wanapata taarifa zake, katika matarajio kwamba utasaidia upatikanaji taarifa na serikali kufahamu dawa zinakopelekwa.

Anakumbusha kwamba, takwimu zisipotolewa kwa usawa ni hali inayoathiri mahitaji na kwamba yanaweza kuonekana mengi, ilhali madogo, au kuonekana madogo, wakati ukweli mahitaji ni mengi. Hatima ya sintofahamu hiyo ni kuathiri upatikanaji dawa kitaifa.



Huduma ya uuzaji dawa ikiendelea dukani. **PICHA ZOTE: MTANADAO**

### DAWA 30

Akizungumzia aina 30 ya dawa muhimu, Msasi anasema zilianzishwa kwa kiwango cha asilimia zaidi ya 80 na wagonjwa wakifika katika kituo cha afya, wanatibiwa.

Pia kwa upande wa magonjwa makubwa, anasema kunahitajika kutafutwe dawa kutoka sehemu nyingine na kwa sasa serikali imeongeza aina ya dawa 312 ambazo upatikanaji wake unafikia asilimia 76 ya mahitaji yaliyoko.

Msasi anasisitiza hali iliyopo sasa, ni dunia nzima inapambana na usugu dhidi ya dawa na ili kunusuru usugu huo, wananchi wanatakiwa kufuata kanuni za umezaji dawa kwa mujibu wa ushauri wanaopewa na daktari.

> **Ili kufanikiwa lazima takwimu ziwe sahihi wanachukua hatua ya kuwafundisha watu masuala ya takwimu, ili wajua jinsi ya upatikanaji dawa na mahali zinakoenda.**

### NAIBU WAZIRI

Naibu Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, anasema wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) zimechagua Bohari Kuu ya Dawa (MSD) kuwa chombo msimamizi wa mnyororo wa ugavi katika nchi hizo.

Dk. Ndugulile anasema wataalamu mbalimbali, wamekusanyika kuujadili uundaji mnyororo wa upatikanaji dawa na vifaa tiba, mafanikio na changamoto za mnyororo huo.

Anasema, hivi sasa Tanzania imepiga hatua kwa kuangalia mnyororo wa dawa unavyopatikana, ikiwamo upatikanaji dawa katika vituo vya afya, huku kukiwapo ongezeko la bajeti katika sekta ya afya, inayoongezea MSD uwezo wa kununua magari mapya 180.

Naibu Waziri ambaye kitaaluma ni daktari, anasema mnyororo huo umezaa matunda ya dawa zinatolewa ndani ya kipindi cha miezi miwili, badala ya miezi mitatu kama ilivyokuwa awali.

Anasisitiza pamoja na mafanikio yaliyopo, kuna haja ya kuwapo mfumo utakaosaidia kuonyesha matumizi ya dawa yanavyofanyika katika vituo vya afya na anasisitiza kunapokuwapo mfumo wa kuwasaidia, hata hesabu za fedha za serikali zinakwenda vizuri.

Alitoa wito kwa jamii, endapo watu watanunua dawa madukani isiyo na chata ya MSD, anashauri watoe taarifa ili wauzaji wachukuliwe hatua, kwa sababu maduka ya dawa hayaruhusiwi kuuza dawa isiyo na chata tajwa.



Vidonge vya aina mbalimbali.

### DENGUE

Kuhusu ugonjwa wa dengue na tishio la ebola, anasema serikali imejipanga kukabiliana nazo, kwa kuweka wataalamu mipakani wenye vifaa vya kuwapima watu wanaoingia nchini na anatetea kwamba, nchini hakujawahi kuwapo ebola.

Pia anazungumzia dengue, kwamba ilipoingia nchini, wataalamu walipambana nao, pia katika utoaji dawa na elimu ya kujikinga nayo.

Anatoa wito kwa jamii, kwamba endapo watauziwa dawa katika maduka ya dawa na kukuta hayana chata ya MSD, watoe taarifa ili wauzaji wachukuliwe hatua, kwa sababu ni sheria maduka hayaruhusiwi kuuza dawa zizizo na chata ya MSD.

### MWAKILISHI UNFPA

Jacqueline Mahon, ni Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA), anasema mkutano huo umezaa matunda ambayo katika sekta ya afya, maboresho makubwa yameonekana katika mnyororo wa upatikanaji dawa.

Anaisifu serikali kwamba imejipanga kuhakikisha mifumo ya upatikanaji dawa ipo na itasaidia kujua dawa zilikotoka na zinakopelekwa.

Mahon anasema, wataalamu mbalimbali wa afya na teknolojia ya mawasiliano wameshiriki katika mkutano huo, hivyo ni hatua itakayosaidia kuleta mabadiliko katika utoaji huduma za afya nchini na kuleta mafanikio katika utoaji wa dawa.





# Mil. 100/- za stendi zajenga hospitali

**Na Nebart Msokwa,**
MBARALI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mbarali imebadili matumizi ya Sh. milioni 100 ambazo awali zilitengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kituo cha mabasi eneo la Igawa na kuzielekeza kwenye ukamilishaji wa ujenzi wa hospitali ya wilaya.

Uamuzi huo ulifikiwa juzi kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo, ambacho kiliamua fedha hizo zitumike kukamilisha baadhi ya majengo ya hospitali hiyo ili ifunguliwe na kuanza kuhudumia wananchi.

Ujenzi wa hospitali hiyo ulikuwa ukitekelezwa kwa gharama ya Sh. bilioni 1.5 zilizotolewa na Serikali Kuu, lakini zimeshindwa kukamilisha kazi hiyo na kusababisha ujenzi kusimama baada ya fedha kumalizika.

Akiwasilisha maombi ya fedha hizo kwenye kikao cha Baraza la Madiwani, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Aswege Kaminyoge, aliomba kiasi kama hicho cha fedha kipunguzwe kwenye baadhi ya miradi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa ili zielekewezwe kwenye hospitali hiyo.

"Tunaomba kupunguza fedha kwenye baadhi ya miradi hasa ya elimu ili tukamilishe hospitali yetu ambayo tayari serikali ilishatusaidia Sh. bilioni 1.5 za ujenzi," alisema Kaminyoge.

Alisema halitakuwa jambo la busara kuiacha hospitali hiyo ikiwa haifanyi kazi wakati Serikali Kuu imetoa fedha za ujenzi hata kama fedha hizo zimeshindwa kumaliza kazi.

Hata hivyo, baadhi ya madiwani walikubaliana na wazo la kuendeleza ujenzi wa hospitali hiyo, lakini wakapinga vikali fedha kupunguzwa kutoka kwenye miradi ya elimu.

Diwani wa Igurudi, Hawa Kihwele, alisema haiwezekani kuondoa fedha kwenye ujenzi wa vyumba vya madarasa wakati mahitaji ya vyumba hivyo ni makubwa hasa mwakani kwa ajili ya kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza.

"Wananchi wanafanya kazi kubwa ya kuchangia ujenzi wa vyumba vya madarasa ili watoto wao wasipate shida wakati wa kuanza kidato cha kwanza mwakani, sasa haiwezekani halmashauri iachane na miradi hiyo kwani itawavunja moyo wananchi na kuwakosesha watoto fursa ya kuanza haraka masomo ya kidato cha kwanza mwakani," alisema Kihwele.

Badala yake alisema kuwa mradi wa ujenzi wa kituo cha mabasi katika mji wa Igawa ambao umetengewa Sh. milioni 100 unaweza kusubiri kidogo na fedha hizo zikaelekezwa kwenye hospitali bila kuathiri miradi mingine.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Brown Mwakibete, aliwahoji madiwani kama wanakubaliana na wazo la diwani huyo na wote kwa kauli moja wakaunga mkono wazo hilo la kutumia fedha za ujenzi wa kituo cha mabasi na kuzipeleka kwenye ujenzi wa hospitali.

Mei, mwaka huu, Rais John Magufuli aliagiza Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Wizara ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya kukamilisha ujenzi wa hospitali hiyo.

Awali, ujenzi wa hospitali hiyo ulikwama kutokana na nyaraka muhimu za mradi huo kupotea katika mazingira ya kutatanisha, hivyo kusababisha Mkuu wa Wilaya hiyo, Reuben Mfune, kuikabidhi Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) kufanya uchunguzi.



Mafundi wakiendelea na ukarabati wa barabara katika eneo la jirani na Uwanja wa Sokoine, jijini Mbeya jana, mahali ambapo ni makutano ya barabara za Karume na Mbeya-Chunya. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wanaswa tuhuma kuharibu miundombinu ya maji

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

WATU 69 wamekamatwa jijini Mbeya wakituhumiwa kuhujumu miundombinu ya maji ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (Mbeya- WSSA) ikiwa ni pamoja na kujiunganishia huduma hiyo kinyume cha sheria.

Aidha, hujuma hizo zinadaiwa kuisababishia mamlaka hiyo hasara ya zaidi ya Sh. milioni 76 ambazo zimetumika kuirejesha miundombinu hiyo katika hali yake ya kawaida.

Akizungumza na waandishi wa habari jana ofisini kwake, Mkurugenzi Mtendaji wa mamlaka hiyo, Mhandisi Ndele Mengo, alisema baadhi ya watu hao waliokamatwa bado kesi zao zinaendelea mahakamani na baadhi yao wamemalizana nje ya mahakama kwa kukubali kulipa gharama.

"Mpaka sasa fedha ambazo zimelipwa kutokana na uharibifu huo ni Sh. milioni 28 pekee na hawa waliobaki tunawapa siku saba walipe fedha zote maana hawa ni wezi kama wezi wengine. Endapo hawatalipa tutawachukulia hatua kali za kisheria," alisema.

Alisema mamlaka hiyo inatumia gharama kubwa kuzalisha maji kwa maelezo kuwa wana vyanzo vya maji 15 ambavyo vinatumia umeme na vituo vya kutibia maji 10 ambavyo vinatumia gharama kubwa, hivyo wanapotokea wahujumu wanasababisha hasara kubwa.

Mengo alisisitiza kuwa mamlaka hiyo haitatoa tena msamaha kwa wananchi watakaokamatwa wakiiba maji ama kuhujumu miundombinu yake kwa madai kuwa wanawasababishia wananchi wengine washindwe kupata huduma bora ya maji.

Katika hatua nyingine, Mhandisi Mengo alisema mamlaka hiyo inazidai taasisi za serikali zaidi ya Sh. bilioni 1.5 ambazo ni malimbikizo ya madeni kutokana na kutumia huduma ya maji kwa muda mrefu.

Mkurugenzi huyo alizitaja baadhi ya taasisi hizo kuwa ni pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama, vituo vya afya, taasisi za elimu na ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya.

Alisema Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) linadaiwa Sh. milioni 43.9, Jeshi la Polisi (Sh. milioni 657.9), Magereza (Sh. milioni 631.9) na Chuo cha Magereza Sh. milioni 225.8.

Aliwaomba wananchi kuendelea kutoa ushirikiano katika kulipa madeni wanayodaiwa ili kuiwezesha mamlaka hiyo kuendelea kujiendesha kwa faida

Pia aliwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa kutoa taarifa kwa endapo wanaona miundombinu ya maji imeharibika na maji yanapotea au miundombinu ya maji taka inayovuja.

# Walia na ukosefu mabweni wasichana

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WANANCHI wa Kata ya Ruiwa, Mbarali mkoani Mbeya, wameomba kujengewa mabweni katika Shule ya Sekondari ya Gwili kwa ajili ya watoto wa kike ili kuwaepusha na adha ya kutembea umbali mrefu kwenda shuleni.

Walitoa kilio hicho juzi wakati wa ziara ya Mbunge wa Mbarali, Haroon Piri Mohamed, aliyetembelea kata hiyo kusikiliza kero za wananchi hao.

Kutokana na tatizo hilo, wananchi hao walisema wanafunzi wa kike wanakabiliana na mazingira magumu ambayo yanaweza yakawasababishia kubakwa na kupata ujauzito, hivyo wakaomba wakae shuleni hapo ili kuepuka matatizo hayo.

Mmoja wa wananchi hao, Rosena Jumamosi, alisema mazingira wanayokabiliana nayo watoto wa kike katika shule hiyo ni magumu na kuna hatari wengi wao wakaacha masomo kwa kupata ujauzito.

Alisema shule hiyo ilijengwa na wananchi kwa kushirikiana na serikali lakini kwa sasa wanatamani iwe ya bweni ili kuwanusuru watoto wa kike na changamoto ya kupata mimba.

"Watoto wetu wa kike hawana mahali pa kulala, hawana bweni hata moja na wanatembea umbali mrefu ambao ni hatari kwao. Wanaweza wakabakwa na kupata mimba, kwa hiyo baba tunaomba utusaidie kujenga bweni," alisema Jumamosi.

Naye Castol Kassim alisema wananchi wa kata hiyo wako tayari kushirikiana na serikali kujenga bweni hilo kwa kuchangia nguvu kazi ikiwa ni pamoja na kufyatua matofali, kupeleka mchanga na mawe na kusaidia mafundi.

Alisema pamoja na tatizo hilo, pia kuna shida ya maji katika kata hiyo ambayo inawakabili pia wanafunzi wa shule hiyo kwa kutembea umbali mrefu kwenda kutafuta huduma hiyo.

Diwani wa kata hiyo, Kassim Mtale, alikiri kuwapo kwa changamoto hizo, huku akifafanua kuwa kero ya maji imesababishwa na ongezeko la watu ambao bado wanatumia vyanzo vile vile ambavyo vilikuwa vinatumika wakati watu wakiwa wachache.

Alisema maji wanayotumia wananchi hao si salama kwa matumizi ya binadamu, hivyo akamwomba mbunge huyo kuwasaidia kutatua kero hiyo ili kuwaepusha wananchi na magojwa ya mlipuko. "Maji ni machafu sana, ukifungulia bomba ni lazima watatoka vyura ambao wengine wanakuwa wamekufa na wengine wakiwa hai. Sasa kuna hatari ya kukumbwa na magonjwa," alisema Mtale.

Akijibu kero za wananchi hao, Pirimohamed alisema atawasaidia wananchi hao kukabiliana na shida ya maji kwanza kwa kuwachimbia kisima ambacho kitawasaidia badala ya kuendelea kutumia maji machafu.

Hata hivyo, aliwataka wananchi hao kuendelea kutumia nguvu zao kujenga mabweni katika shule yao kabla ya kuomba msaada kutoka serikalini.





# Waomba wamiliki vituo vya yatima wamulikwe

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SERIKALI imeombwa kuwachukulia hatua watu wanaowatumia yatima kama sehemu ya kujipatia mamilioni ya fedha huku wakiwaacha walengwa wakiishi maisha duni.

Ombi hilo lilitolewa jana na watoto yatima na wanaoishi katika mazingira hatarishi wa kituo cha shirika la malezi endelevu cha Shime kilichoko Dodoma Makulu jijini hapa.

Akizungumza na waandishi wa habari, mmoja wa watoto hao, Martha Nolo, alisema ni muhimu serikali ikaviangalia vituo vya watoto yatima kwa kuwa baadhi yao vipo kwa ajili ya kuwanufaisha wanaovianzisha.

Nolo alisema wanaomiliki vituo hivyo wanatangaza wapo kwa malengo ya kuwasaidia watoto yatima wakati si kweli wamekuwa wakiwatelekeza.

"Sisi watoto yatima wa kituo hiki kwa niaba ya wenzetu wanaohudumiwa na vituo vingine, tunaiomba serikali yetu tukufu kuwamulika matapeli hao na kuwachukulia hatua kali za kisheria," alisema.

Naye Reheli Raphael aliziomba taasisi, mashirika na wadau mbalimbali kukisaidia kituo hicho ambacho kina changamoto nyingi hali inayosababisha washindwe kutimiza malengo yao ya kimaisha.

Alisema kwenye kituoni hicho wanatakiwa kuondoka kwenye jengo wanaoishi kwa sasa kutokana na mwenye nyumba kuwapa notisi ya kuwataka wahame.

"Tunalazimika kuomba msaada katika maeneo mbalimbali zikiwamo taasisi za kifedha na mitandao ya mawasiliano na wadau wengine ili watusaidie fedha na mali ambazo zitatufanikisha kupata kituo chetu," alisema.

Mkurugenzi wa kituo hicho, Zawadi Mgeni, alisema Sh. milioni 200 zinahitajika ili kupata eneo ambalo wanaweza kujenga jengo lao. Alisema kiasi hicho kitasaidia kutatua changamoto waliyo nayo ambayo hivi karibuni wanatakiwa kukabidhi jengo hilo kwa mmiliki ambaye alikuwa amelitoa bure bila kulipa kodi.

"Tumekuwapo kwa miaka mingi kwenye jengo hili tukilitumia kama kituo kwa ajili ya kuwahudumia watoto hao kiroho na kimwili bila kulipishwa kodi na sasa tunatakiwa kuondoka," alisema.

Kituo hicho kina watoto yatima na wanaoishi katika mazingira hatarishi 68.



Watoto wa Kituo cha Shime, Makulu jijini Dodoma, wakinywa uji kwenye kituo chao kabla ya kuanza masomo, juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# NHIF yapewa somo kuhusu wataalamu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), umetakiwa kuwatumia maofisa maendeleo ya jamii kutoa elimu kwa wananchi juu ya kujiunga na Toto Afya ili kusaidia upatikanaji haraka wa matibabu kwa watoto.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alisema hayo juzi alipokuwa akifungua Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Maofisa Maendeleo ya Jamii unaoendelea jijini hapa.

Alisema NHIF wanapaswa kufanya kazi kwa ushirikiano na maofisa hao kwa sababu wao ndio wana uwezo wa kujua idadi ya watoto na watu katika maeneo ambayo wanawajibika kufanya kazi za jamii.

"Naomba NHIF mfanye kazi na maofisa maendeleo ya jamii. Nitawaandikia barua ya kuwataka mfanye hilo lengo ni kuona watoto wanakuwa na kadi za bima ya afya," alisema Waziri Ummy.

Alisema gharama za kadi ya Toto Afya ni Sh. 50,400 ambayo mtoto anapata huduma za afya katika hospitali za serikali na za binafsi, hivyo NHIF ambayo ni mhusika wa utoaji wa kadi hizo, wanapaswa kuwatumia maofisa maendeleo ya jamii kwa ajili ya kuwasaidia kutoa elimu hiyo kwa wananchi.

"Tunapokea maombi ya watu kutaka msaada wa matibabu ya watoto.

Ni vyema NHIF wakawatumia maofisa maendeleo ya jamii ambao watawasaidia kutoa elimu ya umuhimu wa bima ya afya," alisema.

Naye Rais wa Chama cha Maofisa Maendeleo ya Jamii Tanzania (Codepata), Sunday Wambura, aliahidi kuwa watafanya kazi kwa weledi huku wakizingatia sera na mwongozo.

Alisema kaulimbiu ya mkutano wa mwaka huu ni 'Maendeleo ya Jamii ni Chachu kwa Mabadiliko Chanya katika Zama za Teknolojia' na wataitumia ipasavyo ili kuhakikisha wanaamsha ari kwa wananchi katika kuchangia maendeleo nchini.

"Tumejipanga kwenda kuamsha ari ya maendeleo katika kila sehemu tunazotoka. Lengo ni kuona kila mwananchi anatambua umuhimu wa maendeleo katika jamii," alisema Wambura.

# TCRA yawapa elimu watu wenye ulemavu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WATU wenye ulemavu wa kutosikia ni miongoni mwa makundi ambayo yanakabiliwa na changamoto kubwa ya utapeli unaofanywa kupitia mitandao ya kijamii.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Ofisa wa Huduma kwa Wateja wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Walter Mariki, alipokuwa akitoa elimu kwa kundi hilo.

Alisema mamlaka hiyo imetoa elimu kwa watu hao kuhusu utumiaji wa huduma za mawasiliano na namna ya kukabiliana na changamoto wanazokumbana nazo katika huduma hiyo ikiwamo wizi na utapeli.

"Tulipewa ombi maalamu kwa ajili ya kutoa elimu kwa watu hawa wenye ulemavu wa kutokusikia na elimu hii ni mahsusi kwa sababu hawa ndio waathirika katika uhalifu wa mtandaoni," alisema Mariki.

Alisema kundi hilo kama wadau wao, wamekuwa na changamoto nyingi katika kutumia bidhaa za wasiliano kwa kuwa hawana uelewa katika kuhusu sekta hiyo.

"Tumetoa tahadhari ya changamoto zilizopo katika mawasiliano ambazo wengi wamekuwa wakikutana nazo hasa utapeli. Njia mojawapo ya kupunguza ni kumsaidia mtumiaji, mfano kapokea ujumbe wa kutakiwa kutuma fedha kwa namba usiyoifahamu usitekeleze kwanza na nini cha kufanya," alisema.

Aidha, aliwataka kuepuka kutoa siri zao za mawasiliano ili kuepuka vitendo vya wizi mitandaoni.

Kwa upande wao, baadhi ya washiriki wa semina hiyo alisema elimu waliyoipata itasaidia kuepuka kutapeliwa kwa mitandao.

"Mafunzo haya yametusaidia katika kutupatia uelewa juu ya huduma za mawasiliano na namna ya kuweza kukabiliana nazo," alisema Yusuph Mloli.

Naye David Chamela alisema wamefanyiwa vitendo vingi vya wizi kwenye mitandao ya simu.



# Awataka Watanzania kuheshimu madaktari

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

SPIKA wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar Zubeir Ali Maulid, amesema madaktari ni watu muhimu katika taifa lolote duniani, hivyo Watanzania wana kila sababu ya kuwaenzi na kuwapa ushirikiano katika harakati za kazi zao za kuokoa maisha.

Alisema fani ya udaktari ni wito licha ya kukumbwa na changamoto nyingi, hivyo kuna kila sababu ya wanafunzi wa kada hiyo ya udaktari kujua falsafa, miiko na masuala muhimu ya kazi hiyo.

Spika alieleza hayo jana mjini Zanzibar katika hafla ya kufungua mkutano mkuu wa chama cha madaktari wanafunzi wa Tanzania.

Aliwaambia kuwa taifa lolote ambalo halina madaktari au linakabiliwa na uhaba wa madaktari haliwezi kuendelea kutokana na wananchi wake walio wengi kukosa tiba na huduma muhimu za afya.

Alisema bila ya kuwapo huduma bora za wataalamu taifa halitapiga hatua za maendeleo kwa vile raia wake wengi watakuwa na hali mbaya za kiafya na kusababisha kupata maradhi mbalimbali tena mara kwa mara.

Aliwaeleza madaktari hao kuwa katika kufikia malengo ya kazi hiyo ni lazima wanafunzi kuujua umuhimu wa kada ya udaktari pamoja na umuhimu wa kuzingatia maadili ya kazi hiyo ili waweze kuwa madaktari watakaotoa huduma iliyo bora kwa maendeleo ya nchi.

Aidha, alisema serikali zote mbili ya Zanzibar na ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zimekuwa zikiwajali wanafunzi wote bila ya kubagua fani zao.

Alikumbusha kuwa ni kutokana na ukweli kuwa masomo yote yanayotolewa yana umuhimu kwa maendeleo ya nchi bila kujali kuwa ni udaktari au ualimu.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Tiba wa Wizara ya Afya Zanzibar, Dk. Juma Mambi, alisema kazi ya udaktari ni taaluma kama kazi nyingine zinazoongozwa na maadili kwa mfanyakazi, hivyo wanafunzi hao wanapaswa kujua wajibu wao ndani ya jamii.

Rais wa Chama cha Madaktari Wanafunzi, Dk. Mohammed Hassan Mohammed, alisema watakuwa wa kwanza kufuata maadili na miiko ya kazi ili kwenda kufanyakazi kulingana na utaratibu wa kazi hiyo na kuwajibika kwa misingi ya udaktari.

# SMZ yatoa msimamo uzazi wa mpango

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imeahidi kuendelea kuwahudumia na kuimarisha afya ya mama na mtoto, bila kujali kipato, imani, dini au mtazamo wa mhusika kuhusu uzazi wa mpango.

Hayo ameeleza Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Balozi Seif Ali Iddi, kwa niaba ya Rais wa Zanzibar, wakati akifungua kongamano la kitaifa la uzazi wa mpango katika mtazamo wa Kiislamu, jana.

Alisema suala la uzazi wa mpango litabaki kuwa ni uamuzi binafsi kwa wanandoa na familia kwa ujumla bila ya kuathiri afya ya mama na mtoto kabla na wakati wa kujifungua.

Alisema kupitia kongamano hilo serikali inategemea kupata mchango mkubwa wa kuelezea masuala ya uzazi wa mpango kwa misingi inayoikubalika katika Uislamu pamoja na dhamira za utekelezaji wa mipango iliyopo na inayofanywa na serikali katika kutoa elimu ya uzazi wa mpango, miongoni mwa wananchi.

Alisema wapo watu wanaopotosha maana ya uzazi wa mpango kwa kuvihusisha na vitendo vya utoaji mimba bila ya sababu zilizoruhusiwa za kiafya hali hiyo inayofanya baadhi ya wananchi wakose hamu ya kupata taaluma na ujuzi sahihi kuhusu njia na taratibu za uzazi wa mpango.

Aidha, Makamu wa Pili wa Rais, aliwasihi wazazi, madaktari, mashekhe, wanazuoni na wataalamu mbalimbali waendelee kushirikiana na serikali katika kutoa elimu ya uzazi wa mpango inayokubalika kulingana na utamaduni na imani ya dini ya Wazanzibari.

Kongamano hilo limewashirikisha watu mbalimbali wakiwamo viongozi wa dini, wanafunzi wa madrasa, mashekhe na wanazuoni limeandaliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Watu (UNFPA) kwa kushirikiana na wabobezi kutoka Chuo cha Kikuu cha Kiislamu cha Al-Azhar cha nchini Misri.



Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma (wa tatu kushoto mbele), Jaji Mkuu mstaafu, Mohamed Othman Chande (kushoto), pamoja na majaji na viongozi mbalimbali katika ufunguzi wa Mkutano wa Jumuiya ya Majaji na Mahakimu wa Afrika Mashariki (EAMJA), Zanzibar juzi. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Wapewa mikakati kufikia masoko EAC

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

WAZIRI wa Biashara na Viwanda, Balozi, Amina Salum Ali, ameishauri Jumuiya ya Wafanyabiashara, Wakulima na Wenye Viwanda Vidogo Zanzibar, kuitumia fursa wanazozipata kuingia katika ushindani wa kibiashara kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Balozi, alisema hayo ofisini kwake Migombani wakati akizungumza na Jumuiya ya Wafanyabiashara, Wakulima na Wenye Viwanda Vidogo, katika kujadili mikakati ya kujipanga namna ya kuikabili fursa za uwekezaji kwenye ukanda wa Afrika Mashariki.

Alisema serikali iko tayari kushirikiana na wafanyabiashara kuimarisha mikakati ya kibiashara kwa wafanyabiashara wakubwa, wakati na hata wadogo ili kuwainua kibiashara.

Alisema Wizara ya Biashara na Viwanda itafanya juhudi zote kushirikiana katika mipango ya kuzalisha bidhaa zilizo bora na zenye kiwango ili kusaidia kuwaongeza nguvu ya kuyatumia masoko ya Afrika Mashariki

Aidha, aliitaka jumuiya hiyo kuyatumia masoko hayo ikiwamo pia kufikisha bidhaa na huduma zao Kongo, Sudan na Msumbiji ili kukuza kiwango cha kibiashara hadi ikifika Julai mwakani , ili Zanzibar iwe imeshaonyesha matunda ya biashara hiyo.

Waziri alimpongeza Rais wa Jumuiya hiyo, Toufiq Turky, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa jumuiya kama hiyo ya Afrika Mashariki.

Naye Turky alisema gharama kubwa zinazotozwa kwenye mizigo ambazo zinafikiria zaidi ya mara tatu zinachangia kurudisha nyuma maendeleo ya kibiashara.

Alimfahamisha waziri kuwa iwapo matatizo ya usafirishaji wa bidhaa yatafanyiwa marekebisho yatasaidia kukuza kiwango cha kibiashara na kitafikia ushindani wanaoulenga.

# Polisi yatawanya madereva wa bajaji kwa mabomu

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi mkoani Iringa limetumia mabomu kutawanya vurugu za waendesha bajaji walioamua kuwarushia polisi mawe na kufanya uharibifu wa mali.

Kamanda wa mkoa huo, Juma Bwire, alisema jana kuwa vurugu hizo zilitokea eneo la Frelimo baada ya askari wa doria maarufu kama Tigo wakiwa kwenye operesheni maalum.

Alisema baada ya askari hao kumkamata dereva Alex Mgimwa kwa kosa la kupakia abiria sita kwenye bajaji yenye namba za usajili MC 186 CGQ na kumtaka waende kituo cha polisi, njiani alipindua ili kuzuia askari asifanye kazi yake.

Kamanda alisema kuwa dereva huyo alimtamkia askari huyo kuwa, atamfanyia kitu kwa sababu wamezoea kuwakamata kila siku.

"Wakiwa kijiwe chao cha maegesho, bajaji zikaungana wakaanza kumshambilia askari, wakirusha mawe askari aliomba msaada ikafika gari ya doria kutoka Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi wa Mkoa (RCO) wakajaribu kuzungumza nao bila muafaka wakazidi kurusha mawe na kuchoma matairi.

"Msaada wa pili uliotoka ni wa doria kutoka kwa ofisa wa operesheni, lakini licha ya kufika hawakutaka mazungumzo na hatimaye gari hiyo yenye namba za usajili PT 1404 ikavunjwa kioo cha mbele."

Kamanda Bwire alisema alitumwa Mkuu wa Upelelezi Makosa ya Jinai (OC CID), lakini madereva hao walikaidi ndipo Jeshi la Polisi lilipowatuma askari wa kutuliza ghasia ambao walilazimika kutumia mabomu kuwatawanya.

"Uharibifu uliofanyika eneo hilo ni wa gari hilo kuvunjwa kioo cha mbele, wamechoma matairi barabarani. Tunawashikilia watu watano na bajaji tano na pikipiki moja," alisema.



Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Kifedha wa Tigo Pesa, Angelica Pesha (kushoto), akizindua huduma ya kutoa fedha kwa njia ya ATM, jijini Dar es Salaam juzi. Wa pili kulia ni Ofisa Mkuu Mtendaji wa kampuni ya UmojaSwitch Ltd, Danford Mbilinyi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ndilikilo ajivunia mafanikio ya WCF

**Na Gwamaka Alipipi**

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, amesema tangu kuanzishwa kwa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), umekuwa faraja kwa wafanyakazi wengi hususani wa viwandani mkoani humo.

Amesema kuanzishwa kwa WCF kumesaidia kuongeza motisha kazini na kuimarisha uhusiano kati ya waajiri na wafanyakazi.

Mhandisi Ndikilo aliyasema hayo alipotembelea banda la WCF wakati wa Maonyesho ya Pili ya Viwanda mkoani Pwani, na kueleza kuwa mfuko huo umekuwa ukiwasaidia wafanyakazi wengi.

"Binafsi niwapongeze sana WCF kwa kuwa mnafanya kazi nzuri sana na hata wananchi wameendelea kuipongeza serikali kwa kuboresha sekta ya hifadhi ya jamii hususani malipo ya fidia kwa wafanyakazi," alisema na kuongeza:

"Hali hii imechangia kuongeza motisha kazini na kuimarisha mahusiano kati ya mwajiri na wafanyakazi wake."

Mhandisi Ndikilo aliwataka wananchi kutembelea banda la WCF ili kuongeza uelewa kuhusu majukumu ya mfuko huo ikiwamo taratibu za madai ili kuepukana na usumbufu unaoweza kujitokeza mfanyakazi atakapopata ajali, ugonjwa au kifo kutokana akiwa kazini.

Wananchi waliotembelea maonyesho hayo waliipomgeza serikali kwa maboresho ya fidia kwa wafanyakazi wa sekta binafsi na umma.

Nao baadhi ya waajiri walipotembelea banda la WCF walisema wameongeza uelewa kuhusu masuala ya fidia na mafao yanayotolewa na WCF.

"Binafsi nilidhani bima ya afya inagharamia matibabu yoyote ya mgonjwa hata yale yanayotokana na ajali au ugonjwa unaotokana na kazi, lakini leo nimefahamu WCF ndiye mwenye kulipa gharama za matibabu hayo," alisema Dk. Aden Mpangile alipotembelea banda la mfuko huo na kuongeza:

"Hapo awali sikufahamu kuwa kiwango cha fidia anachostahili kulipwa mfanyakazi hujulikana baada ya tathmini kufanyika kwa mfanyakazi aliyekamilisha huduma za matibabu ambayo kimsingi matibabu hayo hugharamiwa na mfuko."

Ofisa Uwekezaji Mwandamizi, Michael Semiono, alisema WCF ni mdau mkubwa wa maonyesho ya viwanda na ndio sababu mfuko umeamua kushiriki kwenye maonyesho hayo ili kukutana na wadau wake ikiwamo wafanyakazi na wamiliki wa viwanda nchini.

Semiono alisema WCF unatoa mafao ikiwamo huduma ya matibabu yanayotolewa kwa mfanyakazi aliyepata ajali, na ugonjwa utokanao na kazi.

## Watanzania wapata fursa umiliki nyumba

**Na Mwandishi Wetu**

WATANZANIA wamepata fursa zaidi ya umiliki wa nyumba za makazi, kutokana na mikopo ya riba ndogo.

Fursa hiyo itawawezesha kupata mikopo ya nyumba za majazi kwa riba ndogo ikilenga kurahisisha umiliki wa hitaji hilo muhimu.

Mpango huo umetangazwa na Benki ya Exim Tanzania baada ya kuzindua kampeni maalum ya miezi mitatu kuhusiana na ofa yake ya mikopo ya nyumba za makazi kwa riba ndogo kwa wateja wake na Watanzania kwa ujumla.

Kwa mujibu wa mkuu wa kitengo cha mikopo binafsi, biashara ndogo na za kati wa benki hiyo, Charles Kapufi, kampeni ya huduma hiyo inayofahamika kwa jina "Nyumba Yangu Loan" inahusisha utoaji wa mikopo mipya ya nyumba yenye riba ya asilimia 15 tu, ikiwa ni kiasi cha chini kutolewa kwa mikopo ya aina hiyo sokoni.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo jijini Dar es Salaam jana, Kapufi alibainisha kuwa kupitia huduma hiyo, walengwa watanufaika na mikopo sahihi kwa gharama nafuu na rahisi.

"Kununua nyumba ni uamuzi muhimu sana kwa mtu yoyote, iwe mara yako ya kwanza au la, ingawa mahitaji kati ya wanunuzi hawa yanatofautiana, umuhimu wake ni sawa. Ndio maana kupitia huduma hii mikopo ya ununuzi wa nyumba, kila mteja atapewa mkopo kulingana na hitaji lake na sio kwa kanuni jumuishi," alifafanua.

Zaidi alisema huduma hiyo inatoa suluhisho pia kwa wale wamiliki wa nyumba ambao wana mikopo yenye riba kubwa kwenye taasisi mbalimbali za fedha kwa kubadilishiwa mikopo yenye marejesho makubwa kwenda kwenye marejesho yenye riba nafuu na benki ya Exim.

"Kwa wateja ambao nyumba zao zimeongezeka thamani kutokana sababu kadhaa ikiwamo ongezeko la bei au uboreshaji walioufanya kwenye nyumba hizo tumejipanga kuwawezesha kubadilisha ongezeko hilo kuwa pesa kupitia mkopo maalumu ambao wanaweza kuutumia kujenga nyumba nyingine, kuboresha zaidi nyumba au kuwekeza fedha hizo kwenye uwekezaji wa mambo mengine," alisema.

# Chama tawala kwenye mtihani mzito

**GABORONE,** Botswana

WANANACHI wa Botswana wanatarajia kupiga kura katika uchaguzi mkuu ambao unatarajiwa kutoa ushindani wa kwanza kwa chama tawala cha Botswana Democratic (BDP) katika miongo yake mitano ya udhibiti wa taifa hilo.

Chama kitakachoshinda kitahitajika kuuimarisha haraka uchumi, ambao tangu uhuru kutoka kwa Waingereza mwaka 1966 umekua kwa asilimia nane kila mwaka na kuwa moja ya mataifa yenye mafanikio makubwa Afrika.

Lakini kwa sasa taifa hilo linakabiliwa na kitisho kwa sababu ya kutegemea rasilimali moja kwa muda mrefu ambayo ni almasi.

**Ili kupambana na hayo mshindi atahitaji kuchukua hatua zaidi za kuutanua uchumi.**

Huku akiahidi kuuimarisha uchumi wakati wa kampeni zake, Duma Boko, kiongozi wa chama cha Umbrella for Democratic Change, anamatumaini ya kukiondoa chama cha BDP cha Rais Mokgweetsi Masisi.

Boko anaungwa mkono na Rais wa zamani, Ian Khama, ambaye alimkabidhi madaraka Masisi mwaka jana, lakini sasa amejikuta katika mvutano mkali wa madaraka na rais huyo. Khama anamtuhumu Rais Masisi kuwa dikteta.

Kati ya idadi ya watu milioni 2.2 wa Botswana, watu 924,000 waliosajiliwa kupiga kura watawachagua wawakilishi 57 wa bunge la taifa na 490 wa serikali za mitaa. Mgombea wa chama kitakachoshinda kisha atakuwa rais mpya.

Masisi anajinadi kutokana na rekodi yake ya kupambana na rushwa, kama vile kufanya iwe lazima kwa maofisa wote wa sekta ya umma kutangaza mali zao, na kupunguza urasimu kwa biashara ndogondogo.

Khama, mtoto wa rais mwanzilishi wa taifa hilo Seretse Khama, aligombana na Masisi kuhusu nyadhifa za uwaziri na hatua tata ya rais mpya ya kufuta marufuku ya uwindaji wa tembo Mei, ambayo Khama alikuwa ameitangaza miaka minne iliyotangulia. Tembo hata hivyo hawajawa suala kuu katika kampeni hizi.

Wasiwasi mkuu kwa Wabotswana ni kiwango cha ukosefu wa ajira kuzungukia karibu na asilimia 20 na ukosefu mkubwa wa usawa licha ya hali ya ugavi sawa katika matumizi ya afya na elimu.

Ili kupambana na hayo mshindi atahitaji kuchukua hatua zaidi za kuutanua uchumi.

Uchimbaji wa almasi Botswana umeshuka kwa moja juu ya tano ya pato jumla la ndani katika mwaka wa 2018, ikilinganishwa na nusu katika miaka ya 1900, lakini bado inaunda robo tatu ya mapato ya fedha za kigeni, hata wakati sekta za benki na utalii zikinyakua sehemu kubwa ya mazao. **DW**




Wanamgambo wa Al-Shabab nchini Somalia. **PICHA: AFP**

## Waasi 14 wauawa katika mapigano

**BUJUMBULA,** Burundi

JESHI la Polisi nchini Burundi limesema limewaua wapiganaji 14 na kuwakamata wengine wengi.

Limesema limefanikiwa kuzikamata bunduki 11 na vifaa vingine vya kijeshi katika mapigano yaliyotokea wilayani Musigati katika mkoa wa Bubanza Magharibi mwa Burundi, kilomita zaidi ya 15 na mpaka na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Mapigano kati ya vikosi vya usalama na ulinzi dhidi ya kundi la wapiganaji yalianza mwanzoni mwa wiki katika mkoa wa Bubanza.

Lakini taarifa hiyo ya mapigano haikuweza kutolewa papo hapo, kulingana na kile jeshi limesema lilikuwa likisubiri kutokomeza kundi hilo. Hata hivyo, taarifa ya mapigano hayo ilienea kusambazwa kwenye mitandao ya kijamii, Facebook, Twitter na hasa Whatsapp, huku raia wakichukuliwa kama uvumi tu.

Kwa mujibu wa mashahidi walieleza kuwa mashambulizi hayo ni ya kwanza kutokea tangu mwanzoni mwa mwaka huu, yalidumu saa 13.

Wapiganaji wengi walionekana katika Wilaya za Mpanda, Gihanga na eneo la Mitakataka, mkoani Bubanza tangu mwishoni mwa wiki iliyopita wakijaribu kuingia katika msitu wa Kibira baada ya kuvuka Mto Rusizi unaotenganisha DRC na Burundi.

Kundi la waasi la Red-Tabara limekiri kwenye ukurasa wake wa Twitter kuwa wapiganaji wake ndio walikabiliana vikali na vikosi vya usalama na ulinzi vya Burundi katika mapigano hayo na kwamba wanaendelea kuingia nchini Burundi kwa lengo la kurejesha utawala wa sheria nchini Burundi. **RFI**

## Johnson atishia kuiacha Brexit

**LONDON,** Uingereza

WAZIRI Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, ametishia kuachana na makubaliano ya Brexit aliyofikia na Umoja wa Ulaya (EU) na kuelekeza nguvu katika maandalizi ya uchaguzi mpya, ikiwa bunge mjini London litapiga kura kuyakataa makubaliano hayo.

Johnson bado hajakata tamaa katika mvutano baina ya serikali yake na wabunge wanaompinga, ambao wamepania kuyazuia makubaliano yaliyofikiwa baina ya serikali ya Johnson na EU.

Akizungumza mwanzoni mwa mjadala wa bungeni mwanzoni mwa wiki Johnson aliwataka wabunge kuyaunga mkono makubaliano yake, ili kumaliza mkwamo uliopo na kusonga mbele.

"Kama bunge hili litayaridhia makubaliano haya, ambayo naamini ni mema kwa maslahi ya Uingereza na kwa Umoja wa Ulaya, tutaachana na maandalizi ya dharura kwa uwezekano wa kuondoka bila makubaliano, badala yake tuelekeze nguvu katika kujenga uhusiano wa baadaye na majirani zetu wa Ulaya," alisema Johnson.



Lakini pamoja na rai hiyo kwa wabunge, Waziri Mkuu Johnson ametoa onyo, akisema ikiwa bunge litaamua kurefusha muda wa mchakato wa Brexit hadi Januari au zaidi, atayaondoa makubaliano hayo na kujikita katika kuandaa uchaguzi mpya.

Johnson ambaye alichukua wadhifa wa waziri mkuu Julai, kwa ahadi ya kuiondoa Uingereza katika EU ifikapo Oktoba 31 kwa hali yoyote ile, amewaambia wabunge kuwa kamwe hatoruhusu mchakato huo kuendelea kwa miezi mingine.

Wabunge wanatarajia kupiga kura mbili; ya kwanza wakiulizwa kimsingi kuyakubali au kuyakataa makubaliano na EU na ya pili kuhusu ratiba inayopendekezwa na serikali kuyajadili makubaliano hayo na pengine kuyafanyia marekebisho.

Hata hivyo, Chama cha Upinzani cha Labour kimesema kitaridhia uchaguzi mpya, endapo Uingereza itaafikiana na EU kurefusha mchakato wa Brexit kwa muda wa kutosha kuandaa uchaguzi wa mapema, na kuhakikisha kuwa hakuna uwezekano wa Uingereza kuondoka kiholela katika umoja huo.

Kizungumkuti cha Brexit kimejitokeza pia katika bunge la Ulaya mjini Strasbourg katika kikao cha kutathmini muhula wa rais wa halmashauri ya Ulaya anayemaliza muda wake, Jean Claude Juncker.

Juncker alisema Brexit imekuwa homa kubwa katika kipindi chake ofisini.

"Kusema kweli imeniumizwa sana, kutumia muda wangu mwingi ofisini nikishughulikia Brexit, badala ya kuangazia masuala ya kuimarisha muungano wetu na kuboresha maisha ya watu, Brexit imekuwa kupoteza muda na nguvu," alisema Juncker.

Zimebakia siku tisa tu kisheria, hadi kumalizika kwa muda wa uanachama wa Uingereza katika EU. **DW**

# Ndugai aonya ubaguzi kijinsia katika uchaguzi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amewataka wananchi kuhakikisha wanapata viongozi bila kuwapo na ubaguzi wa kijinsia kwa kuwa ni miongoni mwa changamoto zinazowakwamisha wanawake kushiriki kwenye uchaguzi.

Aidha, amesema Bunge la 11 litatoa tathmini yake ya utendaji ili Watanzania wapime kama lilitimiza wajibu wake ama la kutokana na baadhi ya watu kubeza.

Kauli hiyo aliitoa jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu semina ya wajumbe wa Chama cha Wabunge wa Mabunge ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Madola Kanda ya Afrika itakayofanyika Oktoba 26-29, mwaka huu jijini Arusha.

Spika alisema semina hiyo itafunguliwa na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, Oktoba 27, mwaka huu na inalenga masuala mbalimbali yanayohusu wanawake husuan eneo la uchaguzi.

"Kuboresha ushiriki wa wanawake katika michakato ya uchaguzi ndio kauli mbiu ya semina lengo ni kuboresha ushiriki wao na hatimaye kuongeza idadi ya wanawake katika vyombo vya maamuzi hususan Bunge, jambo ambalo linazingatia misingi ya haki za binadamu," alisema.

"Zipo changamoto nyingi zinazokwamisha wanawake katika kushiriki michakato ya uchaguzi kama wapigakura na wagombea, changamoto hizi zote na namna ya kutatua zitajadiliwa katika semina hiyo," alisema.

Alisema semina hiyo itawashirikisha washiriki 50 kutoka nchi 18 za Jumuiya ya Madola.

Alizitaja ni Afrika Kusini, Botswana, Cameroon, Eswatini,

Ghana, Kenya, Lesotho, Malawi, Mauritius, Msumbiji, Nigeria, Namibia,

Rwanda, Sierra Leone, Seychelles, Tanzania, Uganda na Zambia.

"Pia mabalozi wa nchi 17 za Afrika, mawaziri na viongozi mbalimbali wanawake, viongozi wa dini, baadhi ya watendaji wa serikali za mikoa, wilaya na mwakilishi kutoka Umoja wa Mataifa nchini (UN Women)," alisema.

Kuhusu tathmini ya Bunge la 11, Ndugai alisema imebaki mikutano mitatu kabla ya kuingia katika Uchaguzi Mkuu 2020, hivyo atatoa tathmini ya utendaji wa bunge hilo kabla ya kuvunjwa na Rais.

"Ipo siku tutawaita tufanye tathmini ya Bunge letu la 11 tumefanya kazi vipi? Maana wapo watu walikuwa wanatubeza beza huko nyuma basi tutatoa akaunti ya mambo ambayo tumeweza kufanya kitu gani kama Bunge la 11 ambayo yataingia katika historia ya bunge hili katika kulijenga Taifa letu," alisema.

Spika huyo alisema tathmini hiyo itapima kama kweli Bunge hilo lilitimiza wajibu wake.




Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji (katikati), akishikana mikono na Mkurugenzi wa Kitengo cha Sheria wa Benki ya DCB, Regina Mduma, baada ya kumkabidhi tuzo ya benki hiyo, iliyoshinda mshindi wa tatu katika kitengo cha kampuni bora ya mwaka katika eneo la uwekezaji sekta za kibenki, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. Kulia ni Ofisa wa Kitengo cha Sheria wa DCB, Grace Ringo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Tisa wakiri kuiba katoni 700 za korosho

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imewahukumu washtakiwa tisa kulipa Sh. milioni 125 baada ya kukiri kutenda kosa la wizi wa katoni 700 za korosho.

Washtakiwa hao ni Robert Slaa, Isihaka Ngubi, Cathbert Mlugu, Mrisho Mindu, Mauridi Haji, Hamza Bunda, Kelvin Ngwandu, Joseph Robert na Joseph Mihayo.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi.

Alisema mahakama yake inawaachia washtakiwa wote huru kwa sharti la kutofanya kosa jingine kwa muda wa mwaka mmoja watakapokuwa nje.

Pia watimize masharti ya kifungu (b) katika hati ya makubaliano kinachowataka kulipa hasara ya korosho zilizoibwa ambayo ni zaidi ya Sh. milioni 125.

Katika kesi hiyo, washtakiwa hao wanadaiwa kuwa kati ya Januari 26 hadi Februari 6, mwaka 2018 katikà yadi ya Kampuni ya Zambia Cargo and Logistics Limited, waliiba katoni 700 za korosho zilizobanguliwa zenye thamani ya Dola za Marekani 54,180 sawa na zaidi ya Sh. milioni 125.

Ilielezwa kuwa korosho hizo zilikuwa mali ya Barabara Trading Tanzania Limited na zilikuwa zikisafirishwa kwenda nchini Vietnam.

Ilidaiwa washtakiwa waliiba maboksi ya korosho hizo zilizokuwa katika kontena na kisha kuyajaza mchanga na mengine kukutwa matupu.

# Kigogo Madini ahukumiwa kulipa mil. 300/-

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imemhukumu Meneja Ukaguzi na Shughuli za Maabara wa Wizara ya Madini, Donald Njonjo (30) na mfanyabiashara Gamba Muyemba (51), kulipa fidia ya Sh. milioni 300 ya hasara waliyosababisha baada ya kukiri kuuza madini ya dhahabu.

Kadhalika mahakama hiyo imewataka washtakiwa hao kulipa faini ya Sh. milioni tano au kutumikia kifungo cha miaka mitatu jela baada ya kukiri kuuza madini ya dhahabu yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 507.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Mkazi Mwandamizi, Mfawidhi Kevini Mhina, aliamuru viwanja viliwi vya Njonjo vilivyopo Manispaa ya Dodoma pamoja na gari kutaifishwa kuwa mali ya serikali.

Alisema washtakiwa wamefanya makubaliano na Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP), hivyo adhabu ya faini ni ya kwanza ili iwe fundisho kwa sababu haiwezekani wakaachwa bila kulipa faini.

"Mahakama yangu inawaamuru washtakiwa kulipa faini ya Sh. milioni tano au kutumikia kifungo cha miaka mitatu, makubaliano mliyoingia na DPP muyatekeleze kwa kufidia hasara mliyosababisha hivyo, mnatakiwa kulipa faini ya Sh. milioni 300 na mahakama imeshazingatia kwamba Sh. milioni 50 imeshalipwa na kiasi kilichobaki kilipwe ndani ya miezi 12, (mwaka mmoja)," alisema Hakimu Mhina.

Pia alisema mahakama inataifisha mali tatu ikiwamo viwanja viwili vilivyopo Block C na Uzunguni Manispaa ya Dodoma pamoja na gari vitakuwa mali ya serikali.

Kadhalika madini feki yakabidhiwe Tume ya Madini. Kabla ya kutolewa kwa adhabu, Wakili wa Serikali, Jacqueline Nyantori, alidai hawana kumbukumbu ya makosa ya nyuma ya washtakiwa na kuomba mahakama izingatie makubaliano waliyoingia.

Alidai katika sehemu ya makubaliano hayo ni kulipa fidia ya Sh. milioni 300, kutaifisha viwanja, gari na madini feki.

Nyantori aliiomba mahakama hiyo iwaadhibu washtakiwa kwa sababu makosa hayo yanadidimiza uchumi wa nchi na kuwa kama wangefanya shughuli hiyo kihalali nchi ingepata mapato ambayo yangewanufaisha Watanzania wote.

Hata hivyo, washtakiwa hao waliomba mahakama hiyo iwape adhabu ya faini kwa sababu ni kosa lao la kwanza na wameokoa gharama za uendeshaji wa kesi.

Walidai wameamua kuingia makubaliano na DPP baada ya kukiri kosa na kwamba wanafamilia zinazowategemea.

Akisoma maelezo ya awali, Wakili Nyantori, alidai Novemba 30, 2017 na Juni 29, mwaka huu Njonjo alikuwa mwajiriwa wa Wizara ya Madini akiwa na majukumu ya kuweka uangalizi mzuri wa madini yanayotakiwa kuletwa mahakamani kama kielelezo.

Alidai polisi walikamata dhahabu zenye uzito wa kilogramu 6.244 maeneo ya Feri ya Azam ambazo zilikuwa zikisafirishwa.

Kadhalika, alidai upelelezi ulianza na kufunguliwa kesi namba 67/2017 kwa washtakiwa waliokutwa na madini hayo na kukiri hivyo, walihukumiwa na mahakama iliamuru dhahabu hizo zitaifishwe na kuwa mali ya serikali.

"Madini hayo yalikabidhiwa Tume ya Madini kwa ajili ya uhifadhi maalum na mshtakiwa Njonjo alikuwa anajua funguo inapowekwa. Mshtakiwa aliwasiliana na Muyemba na kuingia makubaliano yasiyo ya kisheria kwa nia ya kujipatia faida na Muyemba alikuwa mtafutaji wa wateja," alidai Nyantori.

Aliendelea kudai kuwa walimpata mteja ambaye aliwahi kutiwa hatiani na kukubali kununua dhahabu zilizotoka kwa washtakiwa hao na kwamba baada ya kuuzwa waliwasiliana na watu wengine wakitaka watengenezewe dhahabu feki zenye uzito wa kilogramu 6.244.

Inadaiwa Majaliwa Shaban alitengeneza madini feki, lakini hakufanikiwa kuyapeleka katika tume hiyo baada ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kutaka madini hayo yapelekwe.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MCHANGANYIKO

**2 ACRE YARD FOR RENT**

Facing New Julius Nyerere International Airport.
Call: +255 754 375 967.
Email: gold@goldtz.net


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311**


### MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na TUJIJENGE TANZANIA LTD, JOSINA COMPANY LTD & AUCTIONEER tutauza kwa mnada wa hadhara Kiwanja cha mdaiwa sugu kilichopo Buswelu-Kahama jina ALFREDY ASAJILE KANDONGA (Tarehe 31/10/2019), PIA RAISA COMPANY LTD tutauza kwa mnada wa hadhara viwanja vya wadaiwa sugu, Jeska Salvatory Kokusima (Kiwanja Eka 1- Homboza 7/11/2019), Rukaiya Abdallah Udulele (Shamba - Msimbu Kisarawe (7/11/2019). Lengo ni kufidia/ kupunguza deni la mkopo wanalodaiwa. Mnada utafanyika kuanzia saa nne Asubuhi kama Tarehe zilivyo mbele ya majina na mahali dhamana zilipo. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**JOSINA COMPANY LTD & AUCTIONEER: 0713/0768203040**
**RAISA COMPANY LTD: 0652113262**

115476402

### KUPOTEA KWAKADI

**MOHAMED ENTERPRISES (T) LTD** anatangaza kupotea kwa kadi tano za pikipiki aina ya BAJAJ –BOXER zenye usajili wa namba zifuatazo MC759CCX, MC 666CCX,MC 971CCX, MC 682CFK, MC 681CFK.

Yeyote atakaeziona hizi kadi atoe taarifa kituo chcochocte cha Polisi.

Polisi Taarifa:
DAR/CEN/RB/851013/2013

---

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
IN THE DISTRICT COURT OF ILEMELA DISTRICT
AT ILEMELA

CIVIL CASE NO 2 OF 2018
HOPE CHIMBE……………DECREE HOLDER
VERSUS
SAMWEL HELMAN…..…………JUDGEMENT DEBTOR

**NOTICE OF DATE OF HEARING**

TAKE NOTICE THAT the above case has been fixed for HEARING on 5 day of NOVEMBER 2019

YOU ARE required to appear in this court without fail and you must produce on that day all the documents upon which you intend to reply upon in support of your case.

GIVEN UNDER my hand and the SEAL of the Court this 23 day of OCTOBER 2019.

TO BE SERVED UPON
SAMWE HELMAN – OF KITANGIRI

115476302

---

IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO…. OF 2019
IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE HERMAN ILDIFONCE HAULE OF DODOMA
AND
IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY CATHERINE MESHACK HAULE

GENERAL CITATION

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filled on or before the …01… Day of …11... 2019.

Dated at Dodoma this 19TH day of October, 2019.

……………………………………………
PETITIONER

Presented for filling this ...11…..day of October…2019

115475502

### KUPOTEA KWA VYETI



EDITH JEREMIAH anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba P1156-0050 kilichotolewa na TEMEKE TEACHER'S RESOURCES CENTRE mwaka 2014. Cheti cha Chuo chenye namba NP1156/0050/2014 kilichotolewa na SCHOOL OF LIBRARY, ARCHIVES AND DOCUMENTATION STUDIES (SLADS) mwaka 2018 pamoja na cheti cha kuzaliwa.

Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.
**Taarifa ya polisi: OB/RB/8802/2019.**

115470102

### KUPOTEA KWA CHETI




**ELIWAZA BRUNO KALOMBOLA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.3561-0016 kilichotolewa na SALMA KIKWETE SEKONDARI mwaka 2014.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi: **KW/RB/6808/2019.**

115474602

### KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**SHAMILI SHAIDU JOHN** anatangaza kupotelewa na Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba S.1871/0055 iliyotolewa na BERNARD SEKONDARI mwaka 2018.
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**DAR/TAB/RB/397265/2019.**

115475002

### KUPOTEA KWA CHETI



**ADAM DADI HITTU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.2626-0032 kilichotolewa na CHARLOTTE SEKONDARI mwaka 2015.
Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**MOR/MOR/RB/356484/2019.**

215475402

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO
Usimamizi wa mirathi No;215/2019
Ombi la RAMADHANI MAJIKATA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu NURU MANJOLE MAJIKATA
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 25/10/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 23/10/2019

115475202

---

RE; THE LAND ACT NO 4 OF 1999
LOSS OF ORIGINAL LETTER OF OFFER OF
REF NO; MMC/LD/8061
REGISTERED OWNER; MWAHIJA S.MKUNGUME

LAND; PLOT NO. 413 BLOCK 'J'KIHONDA MOROGORO MUNICIPALITY
APLICANT; MWAHIJA S.MKUNGUME
TAKE NOTICE that the ORIGINAL LETTER OF OFFER to the land described above is said to be lost and that I intend to issue a REPLACEMENT OF THE ORIGINAL LETTER OF OFFER in lieu thereof unless cause to the contrary is shown within thirty days (30) from the date of this pubication.

THE ORIGINAL LETTER OF OFFER is found,should be delivered to the office of the ;Municipal Director,Morogoro Municipal Council,P.o box 166 Morogoro.

115475102

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**MOHAMED ENTERPRISES (T) LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili MC 999 CGM BOXER.
Chassis namba MD2-B15-BY9KWB-89007.
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**KIJ/RB/404367/2019.**

154744


***Uza,***

***Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi***

***Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0767 223311***



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# DYBALA: JUVE IMEJIANDAA KUSHINDA UEFA

**TURIN,** Italia

PAULO Dybala amesisitiza kwamba Juventus imejipanga "kwenda njia zote" kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya mabao yake mawili ya dakika za mwisho kuwaweka kwenye nafasi nzuri ya kutinga hatua ya mtoano.

Dybala alifunga mara mbili ndani ya dakika mbili wakati mabingwa hao wa Ligi Kuu Italia, Serie A, Juventus wakitoka nyuma na kuifunga Lokomotiv Moscow mabao 2-1 juzi Jumanne kwenye mchezo wa Kundi D mjini Turin.

Matokeo hayo yameiacha Juve ikiwa pointi saba sawa na Atletico Madrid baada ya timu zote kuibuka na ushindi kwenye mechi zao za juzi.

Ikiwa imeshinda taji la Ligi Kuu Italia mara saba mfululizo, Juve haijawahi kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu mwaka 1996 na msimu uliopita ilitolewa na Ajax kwenye hatua ya robo fainali.

Dybala ambaye alifunga dakika ya 77 na 79, alibainisha kwamba, msimu huu wamejipanga kuhakikisha wanafika mbali kwenye mashindano hayo.

"Sisi ni timu ambayo ina wachezaji wenye uzoefu wa kutosha, tumejipanga kwenda njia zote kwenye mashindano haya," alisema Dybala.

"Nafikiri tuna kikosi chenye ubora wa hali ya juu na tutafanya vizuri zaidi kwa siku za hivi karibuni.

"Nina furaha kubwa, kwa uhakika nilikuwa nahitaji mabao mawili. Ulikuwa mchezo mgumu, lakini unaweza kuona kwa namna timu ilivyocheza na ina wachezaji wenye uzoefu. Mara zote tulitulia hadi tulipopata ushindi."

# Neuer ataka Bayern kuimarisha ulinzi

**MUNICH,** Ujerumani

GOLIKIPA wa Bayern Munich, Manuel Neuer ameitaka timu yake kuimarika zaidi kwenye safu ya ulinzi wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 3-2 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Olympiacos.

Mabao mawili kutoka kwa mshambuliaji, Robert Lewandowski yaliisaidia Bayern kushinda mchezo wake wa tatu mfululizo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya katika Kundi B, lakini mabingwa hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, walikuwa na mwisho mgumu.

Neuer ambaye alikuwa kwenye ubora wake aliokoa hatari mbili za dakika za mwisho.

Bayern imeruhusu kufungwa mabao 10 kwenye mechi nane za Ligi ya Mabingwa Ulaya, Bundesliga, na mabao manne katika mechi tatu za Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Tatizo kwa sasa ni kwamba tunahitaji kufunga mabao matatu katika kila mchezo ili kushinda, kwa sababu tumekuwa tukiruhusu mabao," alisema Neuer akiambia UEFA.com.

"Ilikuwa ngumu kwa upande wetu na hatukuwa na safu imara ya ulinzi.

"Tunahitaji kuendelea kufanyia kazi hilo, na kuangalia namna gani tunavyoweza kufanya vizuri zaidi."






# Thiago Motta awa kocha mpya Genoa

**ROME,** Italia

KLABU ya Genoa imemteua kiungo wa zamani, Thiago Motta kuwa kocha wake mpya wa kikosi cha kwanza, kwa mujibu wa ESPN.

Kipigo cha wiki iliyopita cha mabao 5-1 kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A, kutoka kwa Parma kikailazimu Genoa inayoshika nafasi ya 19 kwenye msimamo kumfukuza kocha wake, Aurelio Andreazzoli.

Motta amerudi Genoa, ambako mchezaji huyo wa zamani wa timu ya Taifa ya Italia aliichezea klabu hiyo msimu wa 2008-09, wakati klabu hiyo ilipofuzu kwenye Ligi ya Europa.

Motta mwenye umri wa miaka 37 alikuwa kocha wa timu ya vijana chini ya umri wa miaka 19 ya Paris Saint-Germain tangu alipomaliza kipindi chake cha uchezaji akiwa na mabingwa hao wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, mwaka 2018.

Motta alishinda mataji na lile la Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Barcelona na Inter kabla ya kutua PSG mwaka 2012, ambako alishinda mataji 18 kwa kipindi cha miaka sita aliyokaa hapo.

Ataingoza Genoa kwa mara ya kwanza wakati itakapokutana na Brescia kwenye Ligi Kuu Italia, Jumamosi hii.

Genoa imepoteza mechi tano kati ya sita zilizopita kwenye Serie A na ipo kwenye hatari ya kushuka daraja.

## Simeone: Atletico wamemaliza ukame

**MADRID,** Hispania

DIEGO Simeone amesema ameridhishwa na kiwango kilichoonyeshwa na Atletico Madrid wakati kikimaliza ukame wa kutoshinda mechi nyumbani kwa kuifunga Bayern Leverkusen katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Atletico ilicheza mechi nne katika mashindano yote bila ushindi na ushindi wao wa juzi Jumanne wa bao 1-0 dhidi ya Wajerumani hao ulikuwa ni wa furaha kwao mjini Madrid.

Kikosi hicho cha kocha, Simeone pia kilifunga mara moja tu katika mechi zake tatu zilizopita kwenye dimba lake la Wanda Metropolitano, ambapo Alvaro Morata alifunga dakika ya 78.

"Najisikia vizuri ninapoona hamasa na timu ikicheza soka la kuvutia," alisema Simeone akiwaambia waandishi wa habari baada ya mechi wakati Atletico ikiungana na Juventus kuwa na pointi saba kwenye Kundi D.

"Timu ilijua inatakiwa kucheza kwa namna gani. Tungeweza kucheza vibaya au vizuri, lakini walijua wanatakiwa kuchezaje. Tulikuwa na wakati mzuri wa kucheza vile tunavyotaka."



# MADRID YASAKA MRITHI WA COURTOIS



**MADRID,** Hispania

REAL Madrid imetajwa kuanza maandalizi ya kumwania golikipa wa Atheltic Bilbao, Unai Simon ili kumrithi Thibaut Courtois.

Uamuzi wa kuacha mchakato huo, unatokana na kiwango cha Mbelgiji huyo kushuka msimu huu na amepoteza mapenzi kutoka kwa mashabiki wa timu hiyo tangu alipojiunga na klabu hiyo akitokea Chelsea mwaka 2018.

Na kwa sababu hiyo, Courtois ameanza kutafutiwa mrithi wake na Madrid imeweka wazi kwamba Simon anaweza kutua klabuni hapo, gazeti la El Desmarque limeandika.

Golikipa huyo chaguo la kwanza wa Bilbao, ambaye pia anavaa jezi namba moja, ana mkataba na klabu hiyo hadi mwaka 2023 huku ikielezwa kwamba dau lake la kumnunua lililotajwa kwenye mkataba wake ni pauni milioni 43.

Katika mechi 10 alizocheza Courtois msimu huu, ameruhusu mabao 12 na amemaliza mechi tatu bila kufungwa wakati nyavu za Simon zimetikiswa mara nne na akicheza michezo minne bila kufungwa kwenye mechi nane alizoidakia timu yake.

Courtois alimaliza bila kuruhusu bao katika kikosi cha Zinedine Zidane kilichopata ushindi dhidi ya Galatasaray kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyochezwa Jumanne usiku wiki hii.

## *Guardiola amvulia kofia Sterling*

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola hana shaka kwamba mfungaji wake wa mabao matatu 'hat-trick', Raheem Sterling anaweza kuimarika zaidi, lakini akamsifia nyota huyo wa Manchester City wakati timu yake ikiibuka na ushindi wa mabao 5-1 dhidi ya Atalanta kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

City walianza kufungwa kwa bao la penalti la Ruslan Malinovskiy kwenye mchezo uliopigwa dimba la Etihad juzi Jumanne, lakini Sterling alicheza vizuri na Sergio Aguero na kuweza kupata ushindi huo mtamu jijini Manchester.

Sterling alipata penalti iliyofungwa na Aguero kabla ya mapumziko kwenye mchezo huo wa Kundi C kabla ya yeye kufunga dakika 11 baada ya mapumziko.

Na baada ya mchezo huo, Guardiola alimsifia nyota huyo wa timu ya taifa ya England kwa kufikisha mabao 12 aliyofunga kwenye mashindano yote msimu huu.

"Tulikuwa pamoja kwa miaka minne na nimejibu mara nyingi swali hili, kwamba Sterling ni mchezaji muhimu kwenye kikosi chetu," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari.

"Yeye ni mchezaji wa daraja la juu. Alikuwa kwenye kiwango cha kuvutia na nina uhakika atakuwa kwenye ubora zaidi kwa katika mechi zinazokuja."



# DONDOO Z... A MAGAZETI Y... YA




# SILVA AMEVUNJA REKODI YA MESSI

**●●● Ni baada ya kufunga "hat-trick" akiwa na umri mdogo zaidi ya ...**

**PARIS,** Ufaransa

NAHODHA wa Paris Saint-Germain, Thiago Silva, amemsifia mfungaji wa mabao matatu 'hat-trick', Kylian Mbappe, baada ya kuvunja rekodi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**Mbappe alitokea benchi na kufunga mabao matatu wakati PSG ikiifumua Club Brugge mabao 5-0, juzi Jumanne.**

Nyota huyo wa PSG sasa ameweka rekodi ya kuwa mchezaji mdogo zaidi kufunga mabao 15 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, akiwa na umri wa miaka 20 na siku 306, akiivunja rekodi ya mkali wa Barcelona, Lionel Messi ambaye aliweka rekodi hiyo wakati akiwa na umri wa miaka 21 na siku 288.

Silva alimsifia Mbappe, na kuwaambia waandishi wa habari: "Yeye ni mchezaji wa kweli, yupo tayari, ana zawadi, siwezi kuwaambia zaidi kwa sababu yeye ni mchezaji wa aina yake.

"Nina furaha kubwa kwa ajili yake, kwa timu, na kwa namna alivyocheza leo (juzi). Katika kipindi cha kwanza, ilikuwa ngumu, tulijua hilo, lakini kipindi cha pili tulikuwa imara zaidi.

"Tulikuwa na nafasi, na tulifunga. Hasa Kylian ni mchezaji wa maajabu."

PSG walikuwa na wakati mzuri zaidi dhidi ya Brugge, ambapo mabingwa hao wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, wameshinda mechi tatu za Kundi lao A. Mauro Icardi alianza kwa kufunga bao la uongozi dakika ya saba, kabla ya Mbappe kufunga la pili dakika ya tisa baada ya mapumziko.

Mbappe alitoa pasi ya mwisho kwa Icardi kwa bao lake la pili katika dakika ya 63, kabla ya yeye kufunga mabao yake mawili.

## ZISIKUPITE

### UNITED YAMBANA MANDZUKIC

MANCHESTER United imesema kuwa itaendelea na mchakato wa kumsajili Mario Mandzukic (30), baada ya straika huyo wa Juventus na Timu ya Taifa ya Croatia kupunguza kiwango cha mshahara ambacho amesema anahitaji kulipwa. ***(Sun)***

### ALENA ANUKIA SPURS

TOTTENHAM imeweka wazi nia yake ya kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya Vijana ya Hispania (U-21), na Barcelona, Carles Alena katika dirisha la usajili la Januari. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### MADRID KUMUUZA DIAZ

REAL Madrid imemweleza mshambuliaji wa zamani wa Manchester City, Brahim Diaz, ambaye ana umri wa miaka 20, kuwa inataka kumuuza ikiwa ni sehemu ya kukamilisha mchakato wa kuachana naye. ***(Mail)***

### ISCO AKUBALI KUONDOKA

KIUNGO wa Real Madrid, Isco ambaye ana umri wa miaka 27, amekubali uamuzi uliofanywa na mabosi wa klabu hiyo, ambao wamemtaja kuwa ni mmoja wa wachezaji watakaoondoka kwenye kipindi cha usajili cha dirisha dogo hapo Januari. ***(Mail)***

### VALVERDE AMPIKU ERIKSEN

REAL Madrid imetajwa kuachana na mpango wa kumsajili kiungo wa Tottenham na Timu ya Taifa ya Denmark, Christian Eriksen (27), baada ya kiungo wa Timu ya Taifa ya Uruguay, Federico Valverde (21), kuonyesha kiwango kizuri hivi karibuni. ***(Sun)***

### LIVERPOOL ILIMHITAJI SANCHO

KIUNGO wa zamani wa Liverpool, Dietmar Hamann, amesema kuwa aliwahi kusikia kuwa klabu hiyo ilikuwa na mpango wa kumsajili winga wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho (19). (***Sky Germany - via Mirror***)

### VILLA, PALACE VITANI

CRYSTAL Palace itachuana na Aston Villa katika mbio za kuwania saini ya straika wa Timu ya Taifa ya Colombia, Alfredo Morelos (23), ambaye anaichezea Rangers ifikapo Januari. ***(Express)***

### STAM: NILIIKACHA NEWCASTLE

BEKI wa zamani wa Manchester United, Jaap Stam, amesema kuwa alikataa ofa ya kutua Newcastle na kuamua kujiunga na Feyenoord katika kipindi cha majira ya joto. ***(Voetbal International - in Dutch)***

### MAGUIRE RASMI UNITED

MANCHESTER United imeilipa Leicester kiasi cha pauni milioni 80 ikiwa ni malipo ya awali kwa ajili ya kumsajili beki wa kati wa Timu ya Taifa ya England, Harry Maguire, ambaye ana umri wa miaka 26. ***(Telegraph)***

### ZLATAN KUREJEA ITALIA

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Manchester United, Paris St-Germain na Juventus, Zlatan Ibrahimovic amesema kuwa anataka kurejea Italia kucheza Ligi ya Serie A. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 38 anatarajia kumaliza mkataba wake wa kuitumikia LA Galaxy mwishoni mwa mwaka huu. ***(CalcioMercato)***

# YANGA SC YAENDELEZA 'DOZI' CCM KIRUMBA

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

WAWAKILISHI pekee wa Tanzania waliobakia katika mashindano ya kimataifa, Yanga, wameendelea kufanya vema wakiwa jijini hapa baada ya kuifunga Pamba SC mabao 2-1 katika mechi ya kirafiki iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini hapa jana.

**Yanga ilicheza mechi hiyo kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya kuwakaribisha Pyramids kutoka Misri, katika mchezo wa kwanza wa hatua ya mtoano wa mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika utakaochezwa Jumapili jijini hapa.**

Ushindi huo umepatikana siku moja baada ya Yanga kupata ushindi wa bao 1-0, dhidi ya Mbao FC, katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye uwanja huo huo hapo juzi na kufikisha pointi saba.

Mabao ya Yanga katika mchezo huo wa kirafiki, yalifungwa na Mnyarwanda Patrick 'Papy' Sibomana dakika ya 21 na mshambuliaji wake Mganda Juma Balinya dakika ya 56, huku lile la kufutia machozi la Pamba SC , ambayo inashiriki Ligi Daraja la Kwanza lilipachikwa na mkongwe, Shija Mkina dakika ya 26.

Hata hivyo, Yanga ilipata pigo baada ya mshambuliaji wake wa kimataifa kutoka Zambia, Maybin Kalengo, kukimbizwa Hospitali ya Bugando kufuatia kuumia na nafasi yake kuchukuliwa na kipa, Metacha Mnata aliyekwenda kusimama langoni huku Ramadhani Kabwili, akihamia kwenye nafasi ya ushambuliaji.

Ikumbukwe pia, bao lililoipa Yanga pointi tatu katika mchezo wa juzi dhidi ya Mbao FC, lilifungwa pia na mchezaji wa kigeni kutoka Namibia, Sadney Urikhob.

Kikosi cha Yanga kilichocheza katika mchezo huo ni ; Ramadhani Kabwili, Mustafa Suleiman, Jaffar Mohammed, Said Juma 'Makapu', Lamine Moro, Abdulaziz Makame, Deus Kaseke, Raphael Daudi/Gustavo Simon, Juma Balinya, Maybin Kalengo/Metacha Mnata na Patrick Sibomana.

Baada ya mechi ya Jumapili, Yanga itasafiri kwenda Misri kwa ajili ya mchezo wa marudiano ambao unatarajiwa kuchezwa Jumapili na mshindi wa jumla atakuwa amefanikiwa kutinga hatua ya makundi.

Yanga ilihamia katika mashindano hayo, baada ya kuondolewa na Zesco ya Zambia katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa kufungwa jumla ya mabao 2-1.




Balozi wa SportPesa, Haji Manara, akimkabidhi zawadi ya simu mshindi wa wiki iliyopita wa Promosheni ya Faidika na Jero, Khatibu Shabani (katikati) baada ya kutangazwa kuwa mmoja wa washindi wa wiki ya nne. Kulia ni Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Kidigitali wa Tigo, Ikunda Ngowi. **PICHA: SPORTPESA**

# *Kaseja awanoa makipa Twiga Stars*

**Na Somoe Ng'itu**

GOLIKIPA wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Juma Kaseja, ameshiriki kuwanoa walinda mlango wa Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), ambayo inajiandaa na mashindano ya Kombe la Chalenji yanayotarajiwa kufanyika kuanzia Novemba 14 hadi 23 mwaka huu, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza jana jijini, Kaseja, alisema kuwa kama Mtanzania anawajibika kuwaongezea mbinu wachezaji hao wa Twiga Stars ili waweze kufanya vema katika mashindano hayo yanayoshirikisha timu kutoka Afrika Mashariki na Kati.

Kaseja alisema kuwa kikosi hicho kina wachezaji wenye vipaji, na anaamini wana nafasi ya kutetea taji la mashindano hayo, ambalo wanalishikilia.

"Mimi ni Mtanzania, na nina jukumu la kuisaidia Tanzania, nimemaliza majukumu ya Stars, jana (juzi) nimecheza mechi (JKT Tanzania vs KMC), na leo nimeamua kuja kufanya mazoezi na dada zetu, mara nyingi nimekuwa nikiwasaidia, ili waweze kutimiza ndoto zao," alisema Kaseja.

Naye Katibu Mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wilfred Kidao, alisema kuwa anaridhishwa na maandalizi yanayoendelea na anaamini wachezaji hao wataendelea kupeperusha vema bendera ya nchi katika mashindano hayo.

"TFF imewekeza katika kiwango kikubwa kwenye timu za Taifa, hicho ndicho kipaumbele tulichonacho na ndio sababu zinafanya vizuri," Kidao alisema.

Twiga Stars ndio mabingwa watetezi wa mashindano hayo yanayoandaliwa na Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa).

## Mbao FC walia kukosa bahati

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kupoteza mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Yanga, Kocha Mkuu wa Mbao FC, Hemed Morocco, amesema kuwa kikosi chake kilipambana kusaka ushindi, lakini hakikuwa na bahati na kuondoka na pointi katika mchezo huo.

Mbao FC ililala bao 1-0, katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Yanga, ambao ulichezwa juzi kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Morocco aliliambia gazeti hili jana kuwa wachezaji wake walipoteza umakini kila walipokuwa wako jirani ya lango la wapinzani wao, na endapo wangekuwa makini, wangepata ushindi katika mchezo huo.

"Kuna mapungufu machache ambayo nimeyabaini katika kikosi changu, kupitia mchezo huo, nitaendelea kuyafanyia kazi ili michezo ijayo tufanye vizuri," alisema Morocco.

Kocha huyo aliwataka mashabiki wa Mbao FC waendelee kuwapa ushirikiano ili wafanye vizuri katika michezo inayofuata ya ligi hiyo.

## Mshindi wa gari Sportpesa anukia

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya burudani na michezo ya kubashiri SportPesa kwa kushirikiana na kampuni ya mtandao wa simu ya Tigo jana walichezesha droo ya kuwapata washindi wa wiki ya tano wa simu janja aina ya Samsung A10s na kuwakabidhi washindi wanne wa wiki iliyopita kutoka hapa jijini Dar es Salaam.

Promosheni ya Faidika na Jero ilizinduliwa rasmi siku Septemba 20 mwaka huu, ambapo SportPesa kwa kushirikiana na Tigo waliahidi kuwazawadia wateja wake simu janja mpya aina ya Samsung A10s kwa siku 40 na gari mpya aina ya Renault Kwid.

Akizungumza baada ya droo ya wiki ya tano, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas, alisema kuwa promosheni hiyo bado inaendelea ambapo wiki ijayo wanatarajia kuwapa washindi watakaomaliza promosheni na mshindi wa gari mmoja.

"Mpaka sasa tumepata washindi kutoka mikoa mbalimbali ikiwamo Dar es Salaam, Pwani, Dodoma, Iringa, Morogoro, Mbeya, Lindi, Tunduma na Zanzibar."

"Kupitia huduma zetu kama Jackpot ambayo kwa sasa iko zaidi ya milioni 250 baada ya kubashiri mechi 13 kwa usahihi zinaweza kumwinua Mtanzania kiuchumi, na kumwezesha kushinda fedha kila siku.

"Napenda kuchukua nafasi huu kuwapongeza washindi wa wiki hii ambao ni Sadick Mihambo, Shazili Sambi kutoka DSM, Mussa Hassan kutoka Mbeya, Chawedi Saidi kutoka Lindi, Mwate Mohammed kutoka Morogoro na Regan Yusto kutoka Zanzibar.

# Michezo

Alhamisi Oktoba 24, 2019

Nipashe





Silva amevunja rekodi ya Messi UKURASA 30



Wachezaji wa Simba wakishangilia baada ya kupata bao katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Azam FC, iliyochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba haikamatiki

## ●●● Yapeleka tena kilio kwa Azam FC, huku Kagere akizidi kung'ara...

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuwafunga na kubeba Ngao ya Jamii, Simba imeendeleza ubabe kwa Azam FC kwa kupata ushindi wa bao 1-0 katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

**Mabingwa hao watetezi waliondoka na pointi tatu baada ya mshambuliaji wake Mnyarwanda Meddie Kagere kufunga bao pekee katika mchezo huo na kuifanya timu hiyo ifikishe pointi 15 na kujiimarisha katika msimamo wa ligi, baada ya kushuka dimbani mara tano.**

Kagere alifunga bao hilo kwa kichwa, kufuatia krosi safi kutoka kwa pacha wake aliyekuwa naye Gor Mahia, Francis Kahata na kuujaza wavuni huku kipa, Mwadini Ally, akiruka bila mafanikio ikiwa ni dakika ya 49 na kufikisha bao la saba kwenye kibindo akikifukuzia tena kiatu cha dhahabu.

Kwa upande wa Azam yenyewe imekamilisha mechi ya nne, ikishinda tatu, na kufungwa mchezo mmoja, ikikamata nafasi ya sita.

Kipindi cha kwanza timu hizo zilionekana kucheza kwa kukamiana na ubabe, lakini hali ikabadilika kipindi cha pili, kila timu ilipoamua kutandaza kandanda safi. Kashikashi kwenye mechi hiyo ilianza dakika ya kwanza tu wakati Msudan Sharaf Eldin Shiboub, alipoachia shuti kali akiwa nje ya eneo la hatari, lakini mpira ulipaa kidogo kwenye goli la Azam.

Sekunde chache baadaye, Shiboub nusura aipatie Simba bao la mapema baada ya kuunganisha kona iliyochongwa na Gadiel Michael, lakini kabla haujavuka mstari wa goli iliokolewa kwa kichwa na mlinzi wa Azam, Bruce Kangwa na kuwa kona nyingine ambayo haikuzaa matunda.

Dakika ya tatu, aliikosesha Azam bao baada ya kupiga kombora kali lililotemwa na kipa Aishi Manula na baadaye kuudhibiti tena kwenye mikono yake. Azam ilipata tena nafasi safi ya kupata bao kwenye dakika ya 37 wakati straika wake raia wa Ivory Coast, Richard Djodi alipoukuta mpira unazagaa kwenye eneo la hatari, akaachia shuti kali lililookolewa na Manula.

Kipindi cha pili kila timu ilifanya mabadiliko, Simba ikiwatoa Shiboub, Kahata na Hassan Dilunga, nafasi zao kuchukuliwa na Clatous Chama, Miraji Athumani na Ibrahim Ajibu, huku Azam ikiwatoa Domayo, Joseph Mahundi, nafasi zao kuchukuliwa na Donald Ngoma na Selemani Idd "Nado", na kuufanya mpira uchangamke zaidi.

Baada ya mchezo wa jana, mabingwa hao watetezi wanatarajia kusafiri kuelekea Arusha, kuwafuata Singida United, katika mchezo mwingine wa ligi hiyo utakaochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini humo.

Matokeo ya mechi nyingine za Ligi Kuu Tanzania Bara zilizochezwa jana ni Alliance imefanikiwa kuichapa Ruvu Shooting bao 1-0 kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza wakati Coastal Union imelazimishwa suluhu Uwanja wa Mkwakwani dhidi ya Singida United, Polisi Tanzania ikawachapa Mwadui FC bao 1-0 kwenye Uwanja wa Chuo cha Ushirika mjini Moshi na Namungo ikiendelea kung'ara kwenye Uwanja wa Kassim Majaliwa mjini Lindi kwa kuifunga Mtibwa Sugar bao 1-0.

Tanzania Prisons yenyewe imelazimishwa sare ya bila kufungana dhidi ya Biashara United Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, na Ndanda ikabanwa mbavu nyumbani, Uwanja wa Nangwanda Sijaona kwa kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Lipuli FC ya Iringa.

# Mbao yaipa kiburi Yanga

**Na Shufaa Lyimo**

ZIKIWA zimebakia siku mbili kabla ya kuwavaa Pyramids kutoka Misri, uongozi wa Yanga na benchi la ufundi, wamesema kuwa wako tayari kuwavaa Waarabu hao katika mchezo wa Kombe la Shirikisho Afrika utakaochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, alisema kuwa matokeo ya ushindi dhidi ya Mbao FC hapo juzi, yamewapa taswira kuelekea katika mchezo huo wa kimataifa.

Mwakalebela alisema kuwa matokeo waliyopata dhidi ya timu hiyo yamewaongezea molari kwenye timu yao, na wanaamini watapata matokeo mazuri katika mchezo huo wa kwanza na kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kusonga mbele katika mashindano hayo.



"Mikakati yetu ni kuhakikisha Jumapili tunapata matokeo mazuri kwenye Uwanja wetu wa CCM Kirumba, tunataka kumaliza kazi hapa hapa nyumbani," alisema Mwakalebela.

Kiongozi huyo aliwataka mashabiki wao Yanga waliopo Mwanza pamoja na mikoa ya jirani wajitokeze kwa wingi Jumapili ili kushuhudia mchezo huo, ambao wanaamini watawapa furaha.

Vile vile Mwenyekiti huyo alisema, mapungufu machache ambayo kocha ameyabaini katika mchezo huo anaendelea kuyafanyia kazi ili yasijirudie katika mchezo wao huo wa Kimataifa.

Naye Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Noel Mwandila, alisema kuwa mchezo wa juzi ulikuwa mgumu kutokana na wapinzani wao kuonyesha kiwango kizuri katika mechi hiyo.

"Haikuwa mechi rahisi, tulijua itakuwa ngumu na yenye ushindani, ninawapongeza vijana kwa kupambana ili kupata ushindi, napenda pia kuwapongeza Mbao kwa kucheza vema," Mwandila alisema.

Wakati huo huo, Maybin Kalengo, ameumia katika mchezo wa kirafiki dhidi ya Pamba na taarifa za awali zinaeleza kuwa mchezaji huyo atakaa nje kwa muda wa wiki nane.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >